# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NANE

**Kikao cha Thelathini na Mbili – Tarehe 26 Julai, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:-**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

**MHE. IDD MOHAMED AZZAN – (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI)**:

Taarifa ya Kamati ya Kilimo na Ardhi, kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2007/2008.

**MHE. JOHN M. CHEYO (MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI):**

Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2007/2008.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 292

**Athari za Mafuriko Wilaya Kilosa**

**MHE. MUSA ZUNGU AZZAN (K.n.y. MHE. CLEMENCE BEATUS LYAMBA)** aliuliza:-

Kwa kuwa kero kubwa sana iliyojirudia kila mwaka Wilayani Kilosa ni mafuriko makubwa na korofi yanayotokea nyakati za mvua za vuli na masika na kuharibu mazao, makazi ya watu na kusababisha vifo vya watu na mifugo na kwa kuwa mafuriko hayo yanayotokana na mito mbalimbali kama vile mto Mkondoa ambao hufurika na kuharibu vijiji vya Tindiga, Malui, Malui, Kondoa, Muungano kwa Lukwembwe na Malangali katika kata ya Mabwerebwere, mto Ngadu, Nyamvisi, Kifinga, Mhovu, Tundu, Kidoli na Msowero ambayo huathiri vijiji vya Ruaha, Iwemba na Kifinga katika Kata ya Kidodi na mito mbalimbali inayoanzia hifadhi ya taifa ya wanyamapori ya Mikumi ambayo huporomosha maji na mchanga bondeni kwenye vijiji vya Kikwaraza, *Green* na kadhalika katika Kata ya Mikumi.

Je, Serikali inazifahamu kero hizo na jinsi zinavyorudirudia na kusababisha maafa makubwa kwa wananchi kila mwaka na ni hatua gani za kudumu zimechukuliwa kuondoa kero hizo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali inazifahamu kero hizo na jinsi zinavyojirudia na kusababisha maafa makubwa kwa wananchi kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na hali hiyo Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

- Kuwaelimisha wananchi waishio mabondeni kuhama na kuepuka madhara yanayoweza kuletwa na maafa.
- Kuendelea kusimamia na kuchukua hatua kwa wanaokiuka sheria za udhibiti wa uharibifu mazingira wa maeneo ya miinuko na kingo za mto.
- Kurejesha huduma katika maeneo ambako miundombinu imeharibiwa pamoja; na
- Kuhamasisha wakulima kutumia unyevunyevu uliopo sasa kwa kulima mazao ya jamii ya kunde na viazi ili kuchukua nafasi ya mazao mengine yaliyoharibiwa na mvua za masika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali za kudhibiti kero ya mafuriko, Mheshimiwa Mbunge, ambaye ni mwakilishi naye ni mdau katika kero hiyo. Tunamwomba aweze basi kutumia fursa hiyo zaidi kuwahamasisha wananchi hao kutokujenga maeneo ya mabondeni na pia kushirikiana na viongozi wa Hifadhi za Mikumi na Ruaha kwa lengo la kupata ufumbuzi wa pamoja kuhusu udhibiti wa mafuriko katika mito mbalimbali inayopitisha maji katika maeneo hayo. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED RICHARD ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa kuwa hali ya mafuriko inayojitokeza kilosa ni pamoja na nchi nzima na vile vile hali hii sasa hivi imekuwa ni ya kawaida duniani kote kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa. Je, Serikali sasa hivi ina mikakati gani na mipango gani ya uhakika kabisa kuhakikisha kwamba wananchi wetu sasa hivi tutumie sheria kali kuwaondoa katika maeneo hayo kwa sababu hayo mambo ni ya kurudiarudia kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge, kwamba sasa hivi kumekuwa na wimbi la mafuriko maeneo mbalimbali na hata wengi tutakuwa tumeona mafuriko ambayo yako sasa hivi katika nchi ya Uingereza. Kwa hiyo, Serikali katika jitihada kama mlivyoona kwamba tumepitisha sera na mikakati mahususi kabisa ya mazingira tutasimamia kuhakikisha kwamba tunatekeleza mikakati hii na nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tushirikiane kuhamasisha wananchi ili wale wanaoambiwa wahame katika maeneo yenye madhara waweze kuhama kuweza kuepusha vifo na madhara mbalimbali yanayoweza kutokea.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kero ya mafuriko ya Kilosa, ndiyo yanayochangia kusababisha treni ya abiria isifike Dar es Salaam na kuwaletea matatizo makubwa wananchi wa Mikoa ya Singida, Tabora, Shinyanga, Mwanza na Kigoma kuteremkia Dodoma. Je, Serikali, haioni kwamba sasa umefika wakati wa kutafuta njia maalum kukomesha haya mafuriko ili wananchi hawa wasiendelee kupata tabu? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli wote tunajua kwamba masuala ya mafuriko kwa kiasi kikubwa ni mambo ambayo yako nje ya uwezo wetu. Kuna yale ambayo yanasababishwa na watu kuharibu mazingira, lakini kuna yale ambayo yanatokea kutokana na mabadiliko ya tabia ya hali ya nchi na mabadiliko katika mfumo mzima wa josho. Kwa hiyo, mimi namuomba Mheshimiwa Mbunge, tushirikiane kuhamasisha wananchi pale panapotokea mafuriko na maafa mbalimbali waweze wakahama kama wanavyoelezwa. Lakini pia pale panapotokea athari katika miundombinu Serikali inaendelea kurekebisha madhara haya.

Na. 293

**Ukarabati wa Barabara – Wilaya za Bariadi, Bunda na Magu**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA (K.n.y. MHE. DR. RAPHAEL MASUNGA CHEGENI)** aliuliza:

Kwa kuwa, barabara za Nyashimo, Nyametembe, Shigala, Nyangili – Malili hadi Ngasamo na ile ya kutoka Lamadi – Mkula hadi Sapiwi ambazo ni kiungo muhimu kati ya Wilaya ya Bariadi, Bunda na Magu na kufuatia mvua zilizonyesha hivi karibuni kuharibiwa na kuzolewa na maji na kusababisha shida kubwa ya usafiri na usafirishaji wa bidhaa na kwa kuwa, barabara hizo ni za Mkoa, kinyume na zile za Mkoa wa Shinyanga ambazo ni barabara kuu hivyo kutokuwa na uwiano wa ubora na uwezo wa kustahimili magari ya mizigo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzikarabati barabara ahizo japo kwa kiwango cha Changarawe ili zifae kupitika nyakati zote?

(b) Je, ni lini mpango wa kuziwekea lami utakamilika?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Raphael Masunga Chegeni Mbunge wa Busega lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa mvua kubwa zilizonyesha kati ya Novemba mwaka jana na Machi mwaka huu, zimesababisha uharibifu mkubwa kwenye barabara nyingi hapa nchini zikiwemo barabara za Nyashimo, Nyamatembe, Shigala, Nyangili, Malili hadi Ngasamo na ile ya Lamadi – Mkula hadi Sapiwi. Wizara yangu kupitia bajeti ya fedha za dharura zilizotolewa na Serikali hivi karibuni imeanza matengenezo ya barabara hizo kwa lengo la kuzifanya zipitike nyakati zote kama ifuatavyo ;

Barabara ya Lamadi – Mkula hadi Sapiwi yenye urefu wa kilometa 17 imetengenezwa na Mkandarasi *M/s Kashere Enterprises* kwa kuchonga barabara hote *(Heavy Grading)* na kuweka Changarawe kwenye maeneo korofi, kazi hii imegharimu jumla ya shilingi 47,056,000 na kazi imekamilikia mwezi Juni, mwaka huu. Barabara ya Nyashimo – Nyamatembe, Shigala, Nyangili – Malili hadi Ngasamo yenye urefu wa kilometa 40 inatengenezwa na Mkandarasi huyo huyo kwa gharama ya shilingi milioni 76,660,080. Kazi inafanyika sambamba kwa kuchonga barabara pamoja na kuweka changarawe kwenye maeneo korofi.

(b)Mpango wa kuweka lami upo kwenye barabara ya Lamadi – Mkula hadi Sapiwi na kuendelea hadi Mwigumbi Mkoani shinyanga. Kwa sasa Mhandisi Mshauri *M/s Crown Tech* anaendelea na upembuzi yakinifu na mara kazi hiyo itakapokamilika kazi ya kutangaza zabuni kwa ajili ya usanifu na ujenzi wa barabara hiyo kwa lami itaanza.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA :** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kuhakikisha kwamba matengenezo madogo yalifanyika. Lakini naomba basi Mheshimiwa Naibu Waziri atuthibitishie kwa kuwa barabara hii ni muhimu sana kutoka Lamadi inafungua Mkoa wa Mwanza na Shinyanga. Je, mtaliwekea kipaumbele zaidi katika Bajeti ijayo ili iweze kutengenezwa kwa lami?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru kwa pongezi alizotupatia kwa kazi ambayo tumeifanya, lakini pili nataka nimhakikishie kwamba barabara hiyo itapewa kipaumbele ili ianze kujengwa kwa kiwango cha lami mara kazi za awali zitakapokuwa zimekamilika. (*Makofi*)

Na. 294

**Matatizo Yanayoikabili Sekta ya Kilimo Nchini**

**MHE. ROSEMARY KIRIGINI** aliuliza:-

Kwa kuwa, ni ukweli usiopingika kwamba, sekta ya mifugo imeshindwa kupata Maendeleo kutokana na matatizo kadhaa yakiwemo yale ya uwezo mdogo wa uzalishaji wa mifugo, mifumo duni ya uzalishaji, utafiti na ugani kutopewa umuhimu unaostahili na ufugaji wa kuhamahama usiozingatia malisho na ukosefu wa mbegu bora za mifugo.

(a) Je, Serikali hadi sasa imetengeneza taratibu zipi za kisheria za kuwawezesha wafugaji kumiliki maeneo yao?

(b) Je, Serikali imebuni taratibu zipi za kuwahamasisha wafugaji na wadau wa sekta ya mifugo wawekeze kwenye uchimbaji wa malambo, visima na kuhifadhi malisho?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kwamba sekta ya mifugo inakabiliwa na changamoto nyingi ili kuweza kutoa mchango mkubwa zaidi katika uchumi wa nchi. Pamoja na changamoto hizo, sekta hii imeendelea kutoa mchango mkubwa kwenye pato la mfugaji na Taifa kwa ujumla na kuliwezesha Taifa kutoagiza mazao mengi ya mifugo kutoka nje. Aidha, Sekta hii imeendelea kutoa ajira kwa Watanzania wengi na kuchangia nguvu kazi na mbolea ya samadi katika kilimo ambapo mchango wake katika pato la sekta kuu ya kilimo umefikia asilimia 13. Hii si haba.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inazo sera, sheria taratibu na kanuni mbalimbali kuwawezesha wananchi, wakiwemo wafugaji, kupata na kumiliki ardhi. Kupitia taratibu hizi Halmashauri za vijiji huandaa mapendekezo ya mipango ya matumizi bora ya ardhi, kugawa ardhi, kutoa hati miliki za ardhi za kimila na kuunda kamati za kusimamia matumizi ya ardhi hiyo. Wafugaji wanayo haki na wanahimizwa kupeleka maombi yao ya ardhi kwa Serikali za vijiji ili yajadiliwe na kutolewa maamuzi na mikutano mikuu ya vijiji hivyo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imebuni utaratibu wa kushirikisha wafugaji na Halmashauri zao, kuchangia uchimbaji wa malambo, mabwawa na visima ambapo Wizara huchangia asilima 50 ya gharama za uchimbaji, Halmashauri asilimia 30 na wafugaji asilimia 20. Kupitia ushirikiano huu, kuanzia mwaka 2001/2002 hadi sasa, Wizara imewezesha uchimbwaji wa malambo 364. Pia, kati ya mwaka 2004/2005-2005/06, Mipango ya Maendeleo ya Kilimo Wilayani, (*DADPs*) imewezesha uchimbwaji wa malambo 47 na mradi shirikishi wa Maendeleo ya kilimo na uwezeshaji *PADEP* malambo 182.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa malisho, wananchi sasa wamehamasika na kuanzisha mashamba ya uzalishaji wa mbegu bora za malisho na hei iliyoboreshwa. Hali hii imeongeza matumizi ya mbegu bora za malisho kiasi kwamba, mashamba mawili yaliyokuwepo ya vikuge (Pwani) na Langwira (Mbeya) yameshindwa kutosheleza mahitaji yao. Ongezeko hili la mahitaji limeilazimisha Serikali, pamoja na kuhimiza sekta binafsi kuzalisha mbegu bora za malisho, kuongeza idadi ya mashamba kufikia manane.
Mashamba mapya ni pamoja na *Sao Hill* liliko (Iringa), Kizota na Kongwa (Dodoma), Mivumoni na Buhuri (Tanga) na Mabuki (Mwanza) yenye jumla ya hekta 969 na uwezo wa kuzalisha tani 25 za mbegu na marobota 150,000 ya hei kwa mwaka. Aidha, katika Mikoa ya Pwani na Tanga, kuna mashamba 16 ya watu binafsi yenye jumla ya ekari 622 zenye uwezo wa kuzalisha tani 11 za mbegu bora na marobota 58,500 ya hei kwa mwaka.

**MHE. ROSEMARY KIRIGINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana aliyonipatia. Lakini pamoja na majibu hayo mazuri bado ninayo maswali mawili.

(a) Kwa kuwa suala la majosho limekuwa ni tatizo kubwa sana na kero kubwa kwa wafugaji kwa nchi nzima. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza idadi ya majosho kwa ile Mikoa yenye idadi kubwa ya mifugo ukiwemo Mkoa wangu wa Mara? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa Mkoa wangu wa Mara ni moja ya Mikoa ambayo ina idadi kubwa ya ng'ombe kwa kuwa na idadi ya ng'ombe milioni 1,298,000. Je, katika mwaka wa fedha 2006/2007 ni mabwawa mangapi mapya yalichimbwa na ni mangapi ya zamani yalikarabatiwa na yapo katika vijiji vipi? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ile ya vijiji vipi hutajibiwa kwa sababu haiwezekani.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Kirigini kama ifuatavyo:-

Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Rosemary Kirigini kwa kutumia fani yake ya mifugo kwa kuwa Mkoa wa Mara unapata huduma za mifugo inavyopaswa. Kuhusu suala la majosho mkakati uliopo ni ule ambao tumekuwa tukiuelezea kila siku kwamba kwa kuwa madaraka yamerudishwa kwenye Serikali za Mitaa inahimizwa wananchi waibue miradi ya ujenzi na ukarabati wa majosho kupitia mpango wa sekta ya maendeleo ya kilimo vijijini (*DADPs*). Lakini Wizara inafahamu kuwa wananchi bado hii ni changamoto kubwa ya kuibua. Juzi wakati najibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, niliahidi kuja Mkoa wa Mara ili kushughulikia pamoja na mambo mengine masuala ya majosho ikiwa ni pamoja na Wilaya Mpya ya Rolya naahidi kutembelea Mkoa mzima ili kuhusu tuweze kuhakikisha kuwa mkakati huu wa kuibua miradi ya ujenzi wa majosho inaiweka vizuri zaidi ili kusudi tujitosheleze majosho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili nakushukuru umenisaidia lakini naomba niseme tu kidogo kuwa mwaka 2006/2007 hakuna lambo jipya au liliokarabatiwa kwa Mkoa wa Mara kwa bahati mbaya.

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, vijiji havina hata sababu.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni kweli Halmashauri pamoja na wananchi wanaweza wakashirikiana kuchimba malambo tatizo ni zana za kuchimbia. Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuwezesha Halmashauri ambazo hazina hizo zana ili wapate wananchi waweze kuchimba malambo hayo kwa kushirikiana na Halmashauri?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuibua mradi wa kujenga majosho/malambo utaratibu ni kwamba wanatafutwa wakandarasi kwa njia ya zabuni wakandarasi hao wanakuwa na uwezo wa kuifanyakazi na kwa hiyo, suala la kusema zana linazingatiwa na kuwa mwisho wa siku huwa ni majosho au malambo yanajengwa.

Na. 295

**Uanzishwaji wa SACCOS**

**MHE. HAFIDH ALI TAHIRMHE (K.n.y. MOSSY SULEIMAN MUSSA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imekuwa ikihamasisha uanzishwaji wa *SACCOS* na wananchi wanawajibika kwa hilo:-

(a) Je, ni *SACCOS* ngapi kwa ujumla zimeanzishwa nchi nzima?

(b) Je, ni Mkoa gani unaoongoza kwa kuwa na *SACCOS* nyingi?

(c) Je, ni *SACCOS* gani inayoongoza kwa kufuata utaratibu unaostahili?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID M. DAVID)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kufikia Februari, 2007 kulikuwa na jumla ya Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (*SACCOS*) 3,469 nchi nzima. Idadi hiyo inajumuisha ongezeko la asilimia 71 ya vyama 2,028 vilivyokuwepo kufikia Juni, 2006.

(b) Mkoa unaongoza kwa kuwa na vyama vingi vya *SACCOS* ni Mkoa wa Mwanza, wenye jumla ya *SACCOS* 529.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu zinazopaswa kuzingatiwa na *SACCOS* ili kufanikisha malengo yake ni kama ifuatavyo:-

· Utunzaji wa kumbukumbu za hesabu kwa kuzingatia viwango vya ubora (*best a practices)*;

· Kuwepo kwa viongozi wanaozingatia maadili ya uongozi uwajibikaji uwazi na kadhalika;

· Kuwepo kwa sera mbalimbali na miongozo ya chama kwa mfano, sera ya akiba na mikopo, miongozo ya uhasibu na kadhalika;

· Kuwa chama endelevu kwa wanachama kulipia hisa zao, kuweka akiba/amana, utoaji wa mikopo kwa muda muafaka na urejeshaji kwa kiwango kisichopungua asilimia 95;

· Chama kuitisha mikutano yake na utoaji wa taarifa za hesabu kwa wakati;

· Chama kutoa huduma mbalimbali kutegemeana na mahitaji ya wanachama;

· Kuwa na waajiriwa wenye sifa za kutoa huduma za kifedha; na

· Kwa ujumla kuzingatia maelekezo ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 20 ya mwaka 2003 na kanuni zake za 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia vigezo hivyo hapo juu, kuna *SACCOS* nyingi katika uendeshaji wake mathalan posta na simu *SACCOS* ya Dar es Salaam, Kibaigwa *SACCOS* ya Dodoma, Tazara ya Mbeya na Mwashita ya Dodoma.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu yake Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini ningependa alifahamishe Bunge hili pamoja na wananchi walioanzisha *SACCOS* hasa kule Zanzibar hivi Mheshimiwa Waziri Serikali inafuatiliaje utekelezaji wa suala hili la *SACCOS* kwa sababu kule Zanzibar ni geni.

(a) Je ni nini matokeo ya ufuatiliaji huo katika kipindi hiki alichozungumza?

(b) Kwa kuwa kule Zanzibar vyama vya ushirika hakuna sasa anashauri vipi Mheshimiwa Naibu Waziri katika kuvianzisha hivyo vyama vya ushirika tukiunga pamoja na wananchi wa Tanzania katika suala hili la *SACCOS*?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID M. DAVID):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Serikali yenyewe inatoa miongozo na sera za ushirika, wanachama wenye malengo fulani wanaungana kwa kuanzisha ule ushirika. Lakini wakati huo huo *SACCOS*, halafu wakati huo huo Serikali inakuwa na maafisa Ushirika katika kila Wilaya kwa ajili ya ukaguzi wa mara kwa mara pamoja na kuangalia kwamba wanafuata zile taratibu za ushirika kwa hiyo, tunao maafisa Ushirika kwa kila Wilaya ambao wanaangalia kwamba *SACCOS* zile zinafuata taratibu kwa mujibu wa sheria na kanuni zake zilizowekwa.

Pili, katika uanzishwaji wa *SACCOS* ama wafanyeje ili waweze kuanzisha *SACCOS* kwanza kuwepo na *formation committee* kutoka eneo ambalo wanataka kuanzisha *SACCOS* wanakwenda kwa Afisa ushirika wa Wilaya wanamueleza nia yao ya kuanzisha *SACCOS* wakishamweleza basi watajadiliana naye kwamba *SACCOS* yetu ina malengo haya na faida yake kwa mwaka itakuwa hii na interest zake kwa mwaka zitakuwa hizi na tunategemea kwamba baada ya miaka miwili tutaendelea hivi na hivi. Kwa hiyo, baada ya hapo wanaandaa zile kanuni. Kanuni zipo lakini watajadiliana na Afisa Ushirika kwamba hizo kanuni zitakuwa ni zipi wataziwasilisha pale halafu ripoti inapelekwa kwa wanachama kwa sababu ile *committee* yenyewe inayozungumzwa tuna Afisa ushirika lakini wanachama lazima waelezwe kwamba tumepewa majibu haya na haya na Afisa Ushirika. Wale wanachama ndiyo sasa wanaandaa *minutes* za kuomba kusajiliwa chama chao kwa mrajisi wa Mkoa.

Sasa kwa *SACCOS* za kawaida zinasajiliwa Mikoani na zile *SACCOS* kubwa za kitaifa zinasajiliwa na mrajibu mkuu Dodoma.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge itabidi ukapeleke semina hiyo Zanzibar maana swali lilikuwa je, Zanzibar? (*Makofi*)

**WAZIRI WA CHAKULA, KILIMO NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu fasaha na kwa elimu juu ya *SACCOS*.

Pili, ningependa kusema ya kwamba Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo ya Zanzibar tulifanya mkutano kule Zanzibar katika hoteli ya bwawani na tukakubaliana kwamba idara ya ushirika itatoa ushauri kwa watalaam kwenda Zanzibar ili kuisaidia Serikali ya Zanzibar katika uanzishaji wa *SACCOS* na utekelezaji wa kazi hiyo unaendelea. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Nafikiri Naibu Waziri anaweza kwenda kutoa mada katika mafunzo hayo. (*Makofi*)

Na. 296

**Wakulima Wadogo wa Mkonge**

**MHE. ENG. LAUS O. MHINA** aliuliza:-

Kwa kuwa zao la mkonge ni kati ya mazao makuu yanayoliingizia Taifa fedha za kigeni; na kwa kuwa wakulima wadogo wadogo wa Wilaya ya Korogwe, wameitikia wito wa kulima zao hili kama zao la biashara katika mashamba yaliyokuwa yakimilikiwa na *Katani Limited:-*

(a) Je, Serikali haioni kuwa ni muhimu kuwapimia na kuwamilikisha mashamba ya mkonge hao wakulima wadogo wanaolima mkonge katika mashamba hayo?

(b) Je, Serikali iko tayari kuwapatia wakulima hao mikopo ya riba ndogo na ya muda mrefu ili wakulima hao wamudu kilimo hicho na hasa ikizingatiwa kuwa uvunaji wa zao hilo unaanza baada ya miaka isiyopungua mitatu (3)?

(c) Je, Serikali haioni kuwa ni vyema kujenga korona katika maeneo yaliyo karibu na wakulima hawa kwa vile gharama hivi sasa hutumika kusafirisha majani ya mkonge hadi kwenye korona?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID M. DAVID)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Laus O. Mhina, Mbunge wa Korogwe Vijijini, lenye sehemu (a), (b) na (c) naomba nitoe maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mashamba ya mkonge manne yaliyokuwa yameuzwa kwa kampuni ya *Katani Ltd*. Mwaka wa 1998 yamekwisharudishwa rasmi Serikalini mwezi Juni 2005 baada ya Serikali na *Katani Ltd* kukubaliana Aprili, 2005.

Aidha, ilikubalika kuwa mashamba ya Hale, Magunga, Magoma Ngombezi na Mwelya yamilikishwe kwa wakulima wadogo wa Mkonge. Mashamba ya Kibaranga, Kingolwira, Kilosa/Miyombo na sehemu ya Mswaha ya shamba la Ngombezi iliamuliwa yauzwe kwa wawekezaji wapya ingawa wawekezaji ambao tayari wanayokodisha walipendekezwa kupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Laus O. Mhina, kama ifuatavyo:-

(a) Katika kutekeleza maamuzi ya Serikali ya mwezi Juni, 2005, wakulima wadogo watamiliskishwa mashamba ya Hale, Magunga, Magoma, Ngombezi na Mwelya. Aidha, *PSRC* ikishirikiana na Bodi ya Mkonge tayari wameweka wataalam ambao wanapima mashamba na maeneo ya miundombinu na kuandaa mikataba ya ukodishaji wa mashamba kati ya wakulima na Bodi ya Mkonge.

(b) Wakulima binafsi au kupitia vikundi, wanashauriwa kuomba mikopo ya pembejeo na zana za kilimo kupitia mfuko wa taifa wa pembejeo. Aidha, namwomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kuwahamasisha wakulima wajiunge katika vyama vya kuweka na kukopa (*SACCOS*) ili kuwarahisishia kupata mikopo.

(c) Umiliki wa korona utawahusisha wakulima na *Katani Ltd.,* kwa uwiano wa hisa za asilimia 40 kwa wakulima na *Katani Ltd.* asilimia 60.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya Serikali ni kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji kwa maeneo yote ya kilimo likiwemo zao la Katani ni matumaini ya Serikali kwamba pamoja na ukarabati wa korona zilizopo, korona mpya zitanunuliwa na wawekezaji na kufungwa kwenye mashamba karibu na wakulima ili kupunguza gharama za usafirishaji.

Na. 297

**Ada kubwa Zinazotozwa Mashuleni**

**MHE. PASCHAL C. DEGERA (K.n.y. MHE. JOB Y. NDUGAI)** aliuliza:-

Kwa kuwa ni jambo baya sana na lisilokubalika kulangua elimu kama ambavyo baadhi ya shule binafsi za awali, msingi na sekondari zinavyofanya kwa kutoza ada kubwa mno na kwa kuwa baadhi ya shule hizo pia hupata ruzuku ya Serikali:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti kupanda ada za kiholela kwa lshule binafsi nchini?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, viwango vya ada vilivyoruhusiwa na Serikali kutozwa katika shule zisizo za Serikali ni kama ifuatavyo:-

Shule za Msingi darasa I-VII kutwa 210,000/=, Bweni 350,000/= Shule za sekondari Kidato cha kwanza hadi cha sita kutwa 150,000/=, bweni 380,000/=. Vyuo vya Ualimu Daraja la IIIA na Stashaha kutwa 130,000/=. Bweni 175,000/=.

Ili shule au chuo kiweze kupewa ruzuku ya Serikali ni lazima ifuate viwango vya ada vilivyowekwa na pia isichangishe michango isiyokuwa na kibali cha Afisaelimu Kiongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kudhibiti viwango vya ada zinazotozwa katika shule zisizo za Serikali kwa kutoa Nyaraka za Wizara za kuwakumbusha wenye shule viwango vilivyowekwa na kufanya ukaguzi katika shule hizo.

Aidha, Serikali imekuwa ikichukua hatua za kukutana na wenye shule kuwashawishi na kuwataka wapunguze viwango vya ada wanavyotoza. Pamoja na hatua hizo kumekuwepo na matatizo katika kuchukua hatua dhidi ya wenye shule hao pale ambapo wazazi wa wanafunzi kwa kupitia Kamati au Bodi za Shule wanaporidhia ada hizo, hasa pale michango inapohusisha huduma zitolewazo katika shule hizo kama vile Mafunzo ya Kompyuta, Chakula na Usafiri.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pia napenda nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa gharama ya elimu ni kubwa na kwa kuwa shule hizi binafsi ama vyuo binafsi wanatoza ada kubwa kutokana na gharama kubwa ya kuendesha shule hizo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza ruzuku ili kuweza kupunguza gharama hizo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli gharama za kuendesha shule ni kubwa. Lakini kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi uwezo wa Serikali kutoa ruzuku kwa shule hizo ni mdogo sana. Mwaka huu tumetenga kiasi kidogo ambacho hatuna hakika kama kitakidhi kwa shule zote ambazo zimeleta maombi.

Ninachoomba ni kwa wenye shule kuweza kufanya mazungumzo na asasi za fedha kuona ni kwa namna gani wanaweza wakapunguzia riba ili na wao waweze kutoa huduma hiyo na elimu iweze kutolewa kwa wengi watakaopenda kwenda kwenye shule hizo. *(Makofi)*

Na. 298

**Gereza la Watoto – Upanga**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA (K.n.y. MHE. RICHARD M. NDASSA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jansia na Watoto katika awamu ya tatu ya uongozi alitembelea gereza la watoto lililopo Upanga Dar es Salaam kuona hali halisi ya mazingira wanayoishi watoto hao:-

Je, Serikali kupitia Wizara husika sasa imeshatembelea gereza hilo kuona ni makosa gani waliyoyafanya na chanzo cha makosa hayo ni nini hata kusababisha watoto hao kufungwa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ndassa, Mbunge wa Sumve, ningependa kufanya masahihisho kidogo kwenye swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu wanapohifadhiwa watoto watuhumiwa huitwa Mahabusi ya Watoto na siyo gereza la watoto. Baada ya masahihisho hayo madogo sasa napenda kujibu swali la msingi la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii alitembelea Mahabusi ya watoto iliyopo Upanga Dar es Salaam tarehe 15/11/2006 kuona hali halisi ya Mahabusi hao. Vile vile mimi mwenyewe nilitembelea kituo hicho tarehe 15/12/2006 kwa madhumuni hayo hayo ikiwa pamoja na kuongea na watoto (mahabusi) na watumishi katika Mahabusi hiyo.

Baadhi ya makosa wanayotuhumiwa nayo watoto hao ni:- wizi, kubaka, watoto hao kupatikana na kutumia madawa ya kulevya, shambulio, mauaji, ukabaji, kujeruhi, kuharibu mali, kulawiti, utoro shuleni, lugha za matusi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya sababu zinazoonekana kuwa chanzo cha watoto (wa kike na kiume) kuingia katika mkinzano na sheria ni pamoja na:-

- Mmomonyoko mkubwa wa maadili katika jamii;
- Kuvunjika kwa ndoa nyingi;
- Umaskini uliokithiri;
- Utandawazi – hivyo watoto kuiga mila na desturi za kigeni na kudharau mila na desturi zetu;

- Ø Watoto kukosa uangalizi na matunzo kutokana na vifo vya wazazi kwa sababu ya ugonjwa wa UKIMWI, ajali na magonjwa mengine;

- Ø Mgawanyo mbaya wa rasilimali kati ya mijini na vijijini unawafanya watoto kukimbilia mijini;

- Ø Watoto kulelewa na mzazi mmoja; na

- Ø Uelewa mdogo wa jamii kuhusu haki za mtoto.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake ya kuelezea suala la mahabusi ya watoto kule wanakowekwa. Watoto hao wakiwa bado wanasubiri kesi zao kuhukumiwa wanawekwa pamoja na watu wazima. Je, huoni kwamba sasa hao watoto watakapotoka pale hawatarekebika. Je, Serikali haioni sasa kuleta mbadala badala ya kuandaa magereza ya watoto tukaandaa mashule ya kuhakikisha kwamba watoto hawa wanaofanya makosa haya wanawekwa mahali pamoja wakajifunza elimu kuliko tunapowaweka kwenye magereza? *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza si sahihi kusema kwamba hawa watoto wanawekwa katika mahabusi pamoja na watu wazima. Mahabusi ambayo imeulizwa katika swali la msingi ni la watoto wadogo kati ya miaka minane na miaka 16. Na pale wanakaa kwa muda wakisubiri hukumu ya Mahakama. Wakihukumiwa wanapelekwa katika shule ya maadilisho ambayo iko Irambo Mbeya. Kule wanaendelea na shule kama alikuwa darasa la tatu, anaingia darasa la tatu na wale waliomaliza shule za msingi wanafundishwa *skills* mbalimbali. Kwa hiyo, nilitaka kusahihisha tu kwamba hiyo mahabusi tunayoizungumzia ni ya watoto chini ya miaka 16 hawachanganywi na watu wazima.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Nashukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa kwenye jibu lake Mheshimiwa Naibu Waziri, amesema watoto wenye makosa mbalimbali wanachanganywa kwenye mahabusi moja na kwa kuwa umri wa utoto ni umri ambao mtoto hujifunza kwa kuona au kusimuliwa na mwenzake. Na kwa kuwa watoto wanakuwa na makosa mbalimbali ambayo mengine yanakuwa hayahusiani kabisa na hivyo watoto wanaweza wakajifunza makosa mengine ambayo hata hawakuwa wametuhumiwa nayo.

Kwa mfano, watoto wa makosa ya madawa ya kulevya kuwekwa pamoja na watoto ambao wanatuhumiwa kwa utoro shuleni. Je, Serikali haioni kwamba kuwaweka kwenye mahubusi moja, watoto wenye makosa tofauti ya namna hiyo, ni kuwafanya hata wale wasio na tabia hizo kuambukizwa tabia zingine ambazo hazifai? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mahabusi ya watoto mara nyingi kunakuwa na uangalizi mkubwa sana. Watoto wanaochanganywa kule wakiwa na makosa mbalimbali haiwezekani kabisa kwamba watoto wale watakuwa wanafundishana kwa sababu kwa kutofautiana na

makosa waliyoyafanya. Kwa sababu pale watoto waliokuwepo pale wanaendelea kupata elimu kama ni mwalimu anakwenda kuwafundisha na kwa maana hiyo kwa sababu ya utoto wao wanakaa katika uangalizi wa mtu ambaye amebobea katika masuala haya hivyo kuangalia kwamba tabia wanapatiwa ushauri nasaha wakati wakiwa wanasubiria kesi zao. Kwa hiyo, siyo rahisi kwa watoto ambao wamewekwa katika gereza lile wakawa na makosa ya tofauti tofauti kuweza kuiga kwa wale ambao wengine wana makosa makubwa kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge.

Na. 299

**Utekelezaji wa Sera mpya ya Afya**

**MHE. MBARUK K. MWANDORO** aliuliza:-

Kwa kuwa uhaba wa huduma za afya ni moja ya kero kubwa, lakini wananchi wamefarijika kutokana na sera mpya ya kuwa na angalau zahanati moja kwenye kila Kata kutasaidia kuleta mafanikio makubwa ya huduma za afya kwa wananchi:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani mahsusi kwa ajili ya Maendeleo ya Sekta ya Afya yanayotarajiwa?

(b) Je, kuna mipango gani iliyoandaliwa ya kuhakikisha kuwepo kwa Madaktari, Wauguzi na Wataalam wengine wa Afya watakaokidhi mahitaji makubwa yatakayotokana na utekelezaji wa sera mpya ya Afya?

(c) Je, maeneo ya pembezoni na yaliyo nyuma kimaendeleo kama vile Wilaya ya Mkinga yatafikiriwa kupiata kipaumbele maalum katika utekelezaji?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro, Mbunge wa Mkinga, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali imeandaa mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) utakaotekelezwa katika vipindi viwili vya miaka mitano mitano kuanzia mwaka 2007 – 2017.

Lengo la mkakati huu ni kuongeza kasi ya kusogeza huduma bora ya Afya ya Msingi kwa kila mwananchi. Ili kutekeleza tamko lililoko katika Sera ya mwaka 1990 na Agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kusogeza huduma za afya karibu na wananchi kwa kuwa na zahanati kwa kila kijiji, kituo cha afya kwa kila Kata, hospitali kwa kila Wilaya, hospitali ya rufaa kila Mkoa na hospitali maalum ngazi ya Taifa kwa kushirikiana na wadau na wananchi.

(b) Mpango wa raslimali watu wa MMAM kwa mwaka 2007/2008 umebainisha mikakati ya kuhakikisha kuwepo kwa Madaktari, Wauguzi na Wataalam wengine wa afya watakaokidhi mahitaji yatakayotokana na utekelezaji wa marekebisho ya Sera ya mwaka 1990. Baadhi ya mikakati itakayotumika ni kuongeza idadi ya watarajali ambao ni muhimu sana katika kuongeza idadi ya watumishi, kutoa ajira kwa wahitimu wote wanaotarajiwa kuhitimu katika vyuo vya afya, kuajiri kwa mkataba wastaafu walio na uwezo wa kufanya kazi ili kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais na kukarabati, kupanua na kufungua vyuo vilivyokuwa vimefungwa ili kuongeza uwezo wa kuchukua wanafunzi wengi zaidi.

(c) Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Afya na Msingi utaanza na maeneo ambayo hayafikiki kwa urahisi na yaliyo duni kimaendeleo. Aidha, utategemea upatikanaji wa raslimali, hususan raslimali fedha na raslimali watu.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Na pia vile vile namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri na fasaha. Swali la kwanza, kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Mkinga walifanya jitihada kubwa sana kujenga zahanati nyingi pamoja na nyumba za madaktari lakini papo hapo wakapata matatizo makubwa sana ya kupata madaktari na waugaji na wataalam wengine. Je, chini ya utaratibu huu mpya Serikali inaweza kutuhakikishia kwamba kasoro hiyo itaondolewa na kuanza kupatiwa wataalam hao haraka iwezekanavyo?

Pili, kwa kuwa Wilaya hii mpya ni kama zilivyo Wilaya nyingine mpya nyingi hazina hospitali ya Wilaya. Je, kwa kutumia utaratibu wa *D by D* Serikali itatoa kipaumbele maalum katika kuisaidia Wilaya hii kupata hospitali ya Wilaya haraka iwezekanavyo? Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mwandoro kwa kufuatilia jimbo lake hasa Wilaya ya Mkinga ili kuweza kuona huduma za afya zinatolewa. Suala la wataalam linafahamika na kwa sababu Mkinga ni sehemu mojawapo ambayo iko katika maeneo ambayo yako nyuma kimaendeleo. Serikali itajitahidi kupeleka wataalam wale ambao wamehitimu kuweza kuona kwamba tunakidhi haja. Lakini vile vile nataka kumfahamisha tu Mheshimiwa Mbunge kwamba si Mkinga peke yake, hospitali nyingine nyingi zina upungufu mkubwa. Kwa jinsi tutakavyokuwa tunapata wataalam ndiyo jinsi ambavyo tutakuwa tunawapeleka katika maeneo yale husika.

Pili, swali lake kuhusu hospitali ya Wilaya ni kweli Wilaya ya Mkinga ni mpya na kama alivyosema katika mpango wa *D by D* namshauri Mheshimiwa Mbunge na kwa vile Mkinga sasa hivi imeshapata Halmashauri yake waweze kukaa na kupanga kuweza kuona ni jinsi gani wataanza kujenga hospitali ya Wilaya na sisi kama Wizara tutatoa ushauri na pale tutakapohitajika tutatoa msaada kama uwezo utakidhi.

**MHE. LUHANGA J. MPINA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Serikali katika mpango wake wa ujenzi wa zahanati kila kijiji utaanza mwaka 2008 na kwa kuwa tayari wananchi wameitikia wito na kuanza ujenzi huo na tayari ujenzi uko kwenye hatua mbalimbali. Mfano katika kijiji cha Mwagai, Isangijo, Mwaukoli, Mwamhongo na Mwasengela wanaendelea na ujenzi wa zanahati mpaka sasa. Je, Serikali itakuwa tayari ku-*support* nguvu za wananchi hao kabla ya mwaka 2008? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuwapongeza wananchi wake katika jimbo lake ambao wanaendelea kujenga zahanati ili kuweza kupata huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kujenga zahanati hili ni suala ambalo wananchi tunashirikiana pamoja na TAMISEMI na Wizara sisi tunatoa wataalam na vitendea kazi. Lakini napenda nimfahamishe tu Mheshimiwa katika mpango huu siyo yeye peke yake ambao wana shida hii. Kwa sababu bado tutatekeleza na tutasaidiana na TAMISEMI kuweza kuona kwamba tunasaidia vile zahanati ambavyo vinajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba tunao upungufu mkubwa sana ambao tutatakiwa kwamba tuutimize kwa mfano tunahitaji vituo 5,162 zahanati na vyuo vya afya 2,074 na hospitali 8 za Wilaya. Kwa hiyo, yote ni mahitaji ambayo Serikali inabidi tuyafanyie kazi kupitia mpango huu tukishirikiana na TAMISEMI.

Na. 300

**Mwendo wa kasi wa Mabasi ya Abiria**

**MHE. LUCY F. OWENYA** aliuliza:-

Kwa kuwa pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kujenga barabara nzuri na kutunga sheria ya kutumia vidhibiti mwendo kwenye mabasi ya abiria kama njia mojawapo ya kuokoa maisha ya abiria na mali zao kutokana na ajali zinazoweza kusababishwa na mwendo wa kasi na kwa kuwa hali halisi ni kwamba mabasi hayo yanashindana yenyewe kwa yenyewe hata kuyapita magari madogo yakiwa kwenye mwendo wa kasi licha ya kuwepo kwa askari wa usalama barabarani:-

(a) Je, Serikali imefuta utumiaji wa vidhibiti mwendo kwenye mabasi hayo?

(b) Je, *speed limit* ya mabasi na magari madogo katika *highways* ni ngapi?

(c) Je, Serikali iko tayari kuweka matangazo barabarani yenye kuashiria kwamba kuna polisi wa kucheki mwendo *(speed)* huko basi linakoelekea na sio mtindo wa sasa askari anakurupuka tu kutoka kichakani na kusimamisha gari/basi ghafla?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 51 (5) cha Sheria ya Usalama Barabarani Na. 30 ya mwaka 1973, Sura ya 168 *R: E Revised Edition, 2002* magari yote ya abiria isipokuwa *Tax-Cabs* hutakiwa kufunga vidhibiti mwendo *(Speed Governor)*. Sheria hii ilianza kutumika Aprili Mosi, 1997. Serikali haijafuta utumiaji wa vidhibiti mwendo kasi kwenye mabasi ya abiria.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Usalama Barabarani Na. 30 ya mwaka 1973, Sura ya 168, Sura ya 168 *R: E Revised Edition 2002,* kifungu cha 51 kifungu kidogo cha (1) na cha (2), kiwango kikubwa cha mwisho cha mwendo kasi wa mabasi ya abiria kwenye barabara kuu *(highways)* ni kilometa 80 kwa saa. Aidha mwendo kasi wa magari mengine ambayo si ya abiria wala mizigo unategemea alama zilizowekwa kisheria katika barabara husika.

Hata hivyo madereva wanatakiwa kuendesha magari kwa umakini na kwa kuzingatia Sheria za Usalama Barabarani ili kuepuka kusababisha ajali.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuweka matangazo barabarani yenye kuashiria kuwepo kwa askari polisi kwenye *(check points)* itakuwa ni kukwamisha azma nzima ya kudhibiti mwendo kasi wa mabasi na magari mengine barabarani.

Askari wa Usalama Barabarani hulazimika kubadilisha *(cehck points)* mara kwa mara ili kuwafanya madereva wasitambue mahali walipo na hivyo madereva kuendesha kwa kuzingatia sheria za usalama barabarani wakati wote wanapoendesha magari yao. *(Makofi)*

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Nashukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini sijaridhika na jibu lake la swali Na. 3 (c) kwa kuwa askari *traffic police* hawakai barabarani kwa masaa 24. Mheshimiwa Naibu Waziri alivyojibu amesema kwamba wakiweka matangazo barabarani kuonyesha kwamba kuna askari polisi mbele itazuia kudhibiti mwendo. Na askari polisi hawa wanajitokeza tu wakati gari tayari iko kwenye mwendo mkali.

Je, haoni ni wakati muafaka sasa kuhakikisha kwamba wanaweka alama hizi ili wale madereva wawe na utamaduni wa kuendesha magari kwa mwendo ambao siyo wa kasi? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa kamera wanazozitumia hawa askari polisi hazichukui picha wala namba ya gari husika.

Je Jeshi la Polisi halioni kwamba ni wakati muafaka sasa kuwapa kamera ambazo zinaweza zikachukua namba ya gari pamoja na lile gari ili kuwa na ushahidi kamili?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano wa kawaida unapoamua kwenda kumfumania mtu huwezi kumwambia nakwenda kufumania. Nia yetu sisi ni kuwakamata wale wanaondesha mbio. Kwa hiyo, tukiwaambia tuko mahali hapa, kwa vyo vyote vile hatutaweza kuwakamata na watajua tuko wapi.

Kwa hiyo, ile sehemu ambayo tupo watapunguza mwendo. Wakiondoka hapo watazidisha. Lakini wakiwa wanajua kwamba hawajui wapi wapo, saa yoyote unashitukiziwa ndiyo maana hatuwezi kuweka mabango yale ya kuashiria. Kuhusu kamera za kisasa. Hili namwunga mkono Mheshimiwa Mbunge na tutafanya kila jitihada kutafuta kamera ambazo zitafanya kazi vizuri ili kuhakikisha tunawadhibiti hawa wote wanaoendesha magari kwa mwendo wa kasi.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba niulize swali moja kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa kiwango cha kilomita 80 kiliwekwa enzi ile Haroun Rashid wakati tulipokuwa tunatumia magari yale ya *Bedford* ya *Austin* kabla ya magari mapya ya Shangingi. Je, Serikali haioni kwamba kilomita 80 imepitwa na wakati ukizingatia kwamba mashangingi yetu haya ukikanyaga tu kidogo umefika kilomita 100. Haingekuwa vizuri sasa wakafikiria angalau kilimita 100 ndiyo iwe ya chini kabisa kulikoni hiyo ya 80?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa tunaona umuhimu wa kuweka *speed* ya 80 kwa saa. Hata hivyo ushauri wake ni nzuri, tunaupokea kwenda kuufanyia kazi ili tuone kama kutakuwa na mabadiliko yoyote tutaeleza ipasavyo. Lakini kwa sasa hivi tuendelee kufuata sheria kwa sababu sheria inazungumzia *speed* 80 kwa saa.

Na. 301

**Uendelezaji wa Viwanda vidogo vya Wajasiriamali**

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH** aliuliza:-

Kwa kuwa nchi yetu imejaliwa kuwa na watu wenye vipaji mbalimbali vikiwemo vya kuunda vitu na vikafanana ama kuzidi zana halisi za mtengenezaji *(genuine)* na kwa kuwa vijana wengi sasa wanao uwezo mkubwa; kwa mfano kikundi cha wahunzi cha Kibaya kilichopo katika jimbo la Iramba Magharibi na vingine vingi vilivyoonekana katika maonyesho ya *SIDO* yaliyofanyika Dodoma mwaka jana:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuviendeleza viwanda hivyo vidogo vidogo vya wajasiriamali ili kuwa na mipango endelevu na hata kuongeza ajira?

(b) Je, Serikali kupitia *SIDO* inaweza kutaja idadi ya vikundi vyenye taaluma mbalimbali na vitu wanavyotengeneza na katika ubora upi?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) pamoja na masahihisho kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza mipango ya kuvisaidia viwanda vidogo vidogo vya wajasiriamali ili kuviwezesha kuwa na mipango endelevu na kuongeza ajira, shirika la kuhudumia viwanda vidogo vidogo *SIDO* hutoa ushauri na mafunzo katika nyanja za teknolojia na manejimenti, utoaji wa mikopo au kuwaunganisha na taasisi za kifedha, utoaji wa huduma za kimasoko, kuwezesha upatikanaji wa taarifa za kibiashara na kuwezesha uanzishaji na uimarishaji wa vikundi vya wazalishaji. Huduma hizi zimekuwa zikiwalenga wajasiriamali katika mikoa yote ya Tanzania Bara na kugusa sekta zote.

Kwa mfano mwaka 2005/2006 wajasiriamali 6845 walipewa mafunzo ya aina mbalimbali kulingana na mahitaji yao, ambapo kwa upande wa Mkoa wa Singida wajasiriamali 689 walipata huduma ya mafunzo na ushauri katika kipindi hicho.

Katika Wilaya ya Iramba vikundi vya uhunzi vya *Umade Group*, Nguvu mali, *Ndago Group, Shati Group* na *Kisimba Group* vilipewa mafunzo ya aina mbalimbali ambapo mpaka sasa Serikali imekwishavitambua jumla ya vikundi 146 vya wahunzi vinavyoendelea kupewa huduma hatua kwa hatua kadri mahitaji na uwezo unavyoruhusu.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa sasa inafanya maandalizi ya kufanya utafiti ili kuweza kutambua kwa uhakika idadi ya wajasiriamali na bidhaa/kazi wanazoshughulika nazo. Kwa hiyo, idadi yo yote ya vikundi inayoweza kutajwa kwa hivi sasa haitakuwa kamilifu.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Ninaomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa kikundi hiki nilichokitaja hasa cha Kibaya kilichopo Ndago, ni kikundi kinachotengeneza bidhaa bora sana na bidhaa hizo zinaendana hasa kwa kilimo kwa wakazi wa Iramba na bei yake ni nafuu. Sasa swali langu liko ifuatavyo:-

Kwa kuwa hiki kikundi hakina uwezo wa kupata malighafi na ili kikaweza kikatengeneza bidhaa nyingi zaidi. Je, Wizara kupitia *SIDO* inaweza ikatoa msaada huo kupata malighafi ili sasa kikafanya kazi vizuri zaidi?

Lakini la pili, kwa kuwa wale vijana wa pale Kibaya wana uwezo mkubwa sana, na wanaweza wakatoa hiyo elimu hasa kwa jimbo zima na kwa hasa vijana wengine ambao wako wilaya ya Iramba na hata kwa mkoa mzima. Je, Wizara kupitia *SIDO* ipo tayari kuwawezesha na ili wakatoa elimu kwa vijana wengine wakapata ujuzi kwa ajili uhunzi?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza kuhusu mahitaji ya malighafi katika kikundi hiki cha Kibaha kilichoko Ndagu, nilisema hapa kwamba huduma mojawapo zinazotolewa na *SIDO* ni pamoja na utoaji wa mikopo lakini pia kuviunganisha vikundi hivi vyenye uhitaji na taasisi mbalimbali za fedha. Kwa hiyo, kwa tatizo hili la upatikanaji wa malighafi namshukuru tu Mheshimiwa Mbunge akubali kwamba huduma zinazotolewa na *SIDO* za kuunganisha vikundi hivi na taasisi za fedha ndiyo jawabu pekee ambalo linaweza kusaidia vikundi hivi kupata hiyo malighafi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kuhusu uwezo wa vijana hawa kutoa elimu kwa wenzao kwanza nakipongeza kikundi hiki ambacho kinauwezo mkubwa sana na nisema tu kwamba katika mafunzo mbalimbali ambayo yanatolewa na *SIDO* pamoja na maonyesho ambayo yanaandaliwa mara mara ni sehemu ya kusaidia maeneo mengine ambayo ya wananchi ambao hawana ujuzi huo. Kwa hiyo, vijana hawa wanaweza wakatumika vilevile katika maeneo kama haya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha na muda umekwisha. Waheshimiwa Wabunge tumebahatika sana tuna wageni wengi na mnavyoona mpaka *gallery* yenyewe imeshajaa, lakini wageni maana yake baraka. Kwa hiyo, wengine nitawatambulisha watakaokuwa sijawatambulisha wote wamekaribishwa.

Kwanza kabisa mimi nina wageni wangu Mheshimiwa Mama Asha Shamsa Naodha, mke wa Waziri Kiongozi Serikali ya Zanzibar yuko na msaidizi wake, karibu sana mama tumefurahi kukuona. (*Makofi*)

Halafu ninao wageni wengine wanaongozwa na Mwenyekiti wa TUGHE Taifa Dr. Diwani Mrutu, hawa ni wageni kama mnavyojua wa Waziri wa Kazi Ajira na

Maendeleoya Vijana, Mheshimiwa Chilligati, naomba wageni wote hawa wasimame huko waliko, karibu sana hawa ni wageni ni wale wanachama wa TUGHE. Kwa hiyo tunashukuru sana nadhani Wabunge wenu wanawawakilisha vizuri sana. Halafu tuna wageni wengine sasa nitawataja wageni hawa ni wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa wa UWT na ni wageni wa Wabunge walioko huku. Wageni wa Wabunge wa Mikoa ya Kagera wako 35 wasimame, karibuni Kagera ni mbali, wageni wa Wabunge wa Shinyanga wako 50 wasimame. (*Makofi*)

Halafu pia nina wageni wa Wabunge wa Manyara wasimame walivyo, karibuni na nawatakia mkutano mwema. Halafu na Katibu wa CCM wilaya ya Magharibi Zanzibar, Ndugu Ali Pira. Halafu nina wageni wa Naibu Waziri wa Usalama wa Raia, Mheshimiwa Asha Bakar Makame, mjumbe wa *NEC* huyu na mimi namfahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Adamu Ngalawe, Katibu wa CCM Mkoa wa Kusini Pemba asimame na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi na Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Rita Mlaki, anayo furaha kubwa sana kumkaribisha mume wake leo Wizara yake inapowasilisha Hoja, Mheshimiwa Theoth Mlaki, *Director* wa Tume ya Sayansi na Teknolojia, wamefuatana na watoto wao. Yuko mtoto wake Michael Mlaki - *Engineer* yeye na yuko Lawrence Mlaki, karibuni sana. Sasa Mheshimiwa John Pombe Magufuli patina wake hakuweza kuja kwa sababu anahangaika na baba yake mgonjwa. Mheshimiwa Waziri baba yake ni mgonjwa kwa hiyo patina wake hakuja. Kwa hiyo, tunamwombea Mwenyezi Mungu baba yake aweze kupata nafuu mapema na wewe uweze kufanya kazi yako kwa amani.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Phillipo Marmo kutoka Mbulu wako sita, nafikiri ni wale wale wa mkoa wa Manyara. Mheshimiwa Esterina Kilasi, Mbunge wa Mbarali pia ni Kamishina wa Bunge ana wageni wake madiwani wa Mbarali Halmashauri naomba wasimame waliko, wameongozana na Mkurugenzi, Mkurugenzi ndiyo yuko wapi halafu na Katibu Tarafa yuko, asanteni sana karibu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Kilasi anafanya bidii sana kutetea eneo lake, tunavyofahamu mbalimbali walikuwa na matatizo, nina wageni mashuhuri sana wanafunzi wa kutoka shule ya Uwata Mbeya kilomita zote hizo wamekuja watoto kama 80 na walimu wao nane. Karibu sana leo uwanja wetu umebanana kwa hiyo mmekaa kwa shida maana yake sisi kwetu ni neema. Katika hawa watoto kuna mtoto wa Mheshimiwa Jenista Mhagama, karibuni sana nawatakia kukaa kwema hapa, nadhani wageni niliopewa nimemaliza.

Nina matangazo ya kazi, kwanza kabisa Mheshimiwa Sophia Simba, Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto anaendelea kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba zile fomu za benki ya wanawake za kununua hisa bado zinaendelea kupatikana chumba 227 jengo la utawala na mwisho wa shughuli hii ni tarehe 27 Julai, 2007 siku ya Ijumaa, kesho. Maana yake, Waheshimiwa Wabunge mnakaribishwa kuchukua zile fomu na kununua *share.*

Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi kuwa leo hii kutakuwa na

kikao chumba 231 saa tano asubuhi. Kwa hiyo, mnaombwa kuhudhuria. Baada ya kusema hivyo Katibu tuendelee na shughuli zingine, Katibu endelea na *Order Paper.*

## HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Matumizi Kwa Mwaka 2007/2008**
**Wizara ya Ardhi, Nyumba Na Maendeleo ya Makazi**.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasilisha ndani ya Bunge hili na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo na Ardhi sasa Bunge lako Tukufu na kujadili mapitio ya utekelezaji wa kazi kwa mwaka 2006/2007 pamoja na mpango wa kazi wa Mwaka wa Fedha wa 2007/2008 wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kutoa pole kwanza kwa familia ya Marehemu Juma Jamaldin Akukweti na Marehemu Amina Chifupa Mpakanjia, kwa kupoteza waliokuwa wenzetu hapa Bungeni.

Pili kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliofiwa na ndugu zao katika mwaka wa fedha wa 2006/2007 tunamuomba Mwenyezi Mungu atupe moyo wa subira sisi sote pamoja na ndugu wa marehemu Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie nafasi hii kuishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo na Ardhi chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo, Mbunge wa Ileje kwa ushauri maoni na maelekezo ambayo yamesaidia kwa kiasi kikubwa katika maandalizi ya hotuba hii ikiwemo uwekeji wa vipaumbele katika bajeti ya mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana hapa leo ikiwa ni Bunge la Bajeti la Pili kwa Serikali ya awamu ya nne. Naipongeza Serikali na Bunge lako tukufu kwa kusimamia kwa mafanikio majukumu ya Serikali. Nachukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa ushirikiano ambao Kamati ya Kilimo na Ardhi imekuwa ikinipatia katika kutimiza majukumu na uendelezaji wa Sekta ya Ardhi. Kwa ujumla ninawashukuru waheshimiwa wabunge kwa kutunga Sheria tatu zinazohusu uendelezaji wa makazi katika kikao cha nane cha Bunge Mwezi Aprili, 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako Tukufu limekwishaelekezwa na kuzingatia misingi ya Jumla ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2007/2008, kama zilivyowasilishwa Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimwa Waziri Mkuu. Nawapongeza na

kuwashukuru wote kwa Hotuba zao nzuri. Baada ya kuzingatia misingi hiyo ya jumla, hotuba yangu mliyogawiwa imejielekeza katika kuainisha malengo na mikakati ya utekelezaji katika Sekta ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo Wizara itaendelea na kutekeleza majukumu yake ya msingi ambayo ni kusimamia sera na sheria za ardhi zinazohusu utoaji uhifadhi, na utumiaji endelevu wa ardhi nchini kusimamia sera na sheria ya uendelezaji makazi miji na vijijini, na kusimamia upimaji wa ardhi na utayarishaji wa ramani kwa matumizi mbalimbali.

Majukumu mengine ni pamoja na kupima na kuhifadhi alama za mipaka katika nchi yetu na nchi tunazopakana nazo, kutafasiri mipaka katika nchi yetu na nchi tunazopakana nazo, kutafasiri mipaka ya maeneo mbalimbali ya kiutawala mikoa, wilaya, tarafa, kata na vijiji ndani ya nchi yetu na kuwaendeleza kiutaaluma na kiutumishi wafanyakazi wa sekta ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kutekeleza shughuli zake kulingana na miongozo ya Serikali kama vile Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupuguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA), Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Ilani ya CCM ya uchaguzi ya mwaka 2005 pamoja na maagizo mbalimbali yanayotolewa na viongozi wa Kitaifa, wakiwemo wabunge yanayogusa sekta zaidi ya moja.

Ardhi ni mojawapo ya rasilimali za msingi kwa uhai wa binadamu na viumbe vyote juu yake. Ardhi hubeba raslimali zingine zote asili na miundo mbinu. Kwa bahati mbaya ardhi haiongezeki lakini wategemezi wa ardhi na mahitaji yao huongezeka kila siku. Mbaya zaidi, baadhi ya mahitaji hayo hukinzana. Mkulima anahitaji ardhi yenye rutuba kuzalisha mazao, wakati huo huo mfugaji anahitaji ardhi hiyo kwa malisho ya mifugo yake na mwanamazingira anahitaji kilimo na mifugo katika hali ambayo hifadhi ya mazingira inazingatiwa ambayo pia ni muhimu kwa uhai wa binadamu na viumbe vinginevyo. Mkanganyiko huu hauna jibu sahihi na la haraka. Njia muafaka ya kushughulikia mkanganyiko huu ni kuhakikisha kuwa kila kipande cha ardhi nchini kinapimwa, kinapangwa na kusajiliwa. Hii ndiyo dhana madhubuti ya uendelezaji endelevu wa ardhi kwa faida ya kizazi kilichopo na kijacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, naomba kutoa Hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Bajeti katika Mwaka 2006/2007, Ukusanyaji wa Mapato, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Wizara ilikuwa na lengo la kukusanya jumla ya Shilingi 10,747,833,000 kutokana na vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia Juni 2007, Wizara imekusanya jumla ya Shilingi 10,087,865,007 ambazo ni sawa na asilimia 94 ya lengo. Kati ya makusanyo hayo, Shilingi 8,598,450,357 ambazo ni sawa na asilimia 85 ya makusanyo, ni kodi ya pango la ardhi itokanayo na viwanja pamoja na mashamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imekuwa ikitekeleza mikakati mbalimbali kwa lengo la kuboresha ukusanyaji wa mapato, utaona kwamba Wizara imeweza kuongeza makusanyo ya kodi ya pango la ardhi toka Shilingi milioni 230 tu kwa mwaka hadi Shilingi bilioni 8.37 kwa mwaka 2006/2007. Mikakati hiyo ni pamoja na kuboresha ukusanyaji wa kumbukumbu za ardhi za wamiliki wa viwanja na mashamba, kuhamasisha ukusanyaji wa kodi kwa njia ya matangazo ya televisheni, radio na magazeti. Aidha, katika mwaka wa fedha 2007/2008 kituo cha Dar es Salaam kitatoa huduma ya ukadiriaji na ulipaji kodi ya pango la ardhi katika sehemu moja, badala ya utaratibu uliopo sasa unaowalazimu wateja kupita ofisi zaidi ya moja. Hatua hiyo itapunguza msongamano na kuongeza ufanisi.

Matumizi, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Wizara yangu iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 18,274,683,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, kati ya hizo Shilingi 3,666,109,000 zilitengwa kwa ajili ya Mishahara na Shilingi 12,542,580,000 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Miradi ya maendeleo ilitengewa Shilingi 2,065,994,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi muhimu zilizotekelezwa na Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2006/2007 ni pamoja na:-

· Tulipima mipaka ya vijiji 2,668 ilikilinganishwa na wastani wa kupima vijiji 110 ambao umekuwa ukipimwa katika miaka nyuma tangu tupate uhuri. Vijiji hivyo vimepimwa katiak mikoa tisa ya Pwani, Lindi, Iringa, Mbeya, Rukwa, Kigoma, Kagera, Shinyanga na Tanga; kwa urahisi wa rejea nimewaambatanishia pamoja na katibu cha hotuba yangu mliyogawiwa kitabu kinachoonyesha orodha ya vijiji vya mikoa hiyo. Pia ndani ya kitabu hicho kuna orodha ya vijiji ambavyo tumepima na kuweka mpango wa matumizi bora ya ardhi.

· Tulifanya mawasiliano ya kuimarisha mipaka ya Kimataifa kati ya Tanzania na Kenya, Uganda, Burundi, Malawi, Msumbiji na Comoro.

**NAIBU SPIKA:** Kunahitajika utulivu Bungeni.

· Tulichora na Kuhakiki ramani za miji 41 ya Kanda ya Ziwa;

· Tulisambaza *Government Notices (GN)* zinazoonyesha mipaka ya Wilaya kwa Wakuu wa Wilaya na Mikoa yote nchini;

· Tulisimamia upimaji wa viwanja katika miji ya Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya na Morogoro. Hadi sasa jumla ya viwanja 49,228 katika miji hiyo vimepimwa;

· Tulisajili hatimiliki na nyaraka nyingine za kisheria 22,139. Aidha, vyeti vya ardhi ya vijiji 211 na Hatimiliki za kimila 3,944 zilitolewa;

· Tulitwaa ardhi kwa manufaa ya umma na kubatilisha miliki 637 katika mikoa mbalimbali hapa nchini;

· Tulitoa vibali vya uwekaji rehani hakimiliki 594 na uhamisho wa miliki 1,352;

· Tulitoa elimu kwa umma juu ya Sera na Sheria za ardhi katika wilaya 23 na vijiji 172;

· Tulihakiki miliki na kutatua migogoro ya ardhi;

· Tulifanya Uthamini wa nyumba na mali 2,800;

· Tuliandaa mipango ya muda mrefu ya miji miwili ya Mwanza na Mtwara/Mikindani na mipango ya muda mfupi ya Miji minane ambayo ni Tandahimba, Tunduru, Namtumbo, Masasi, Babati, Mererani, Ushirombo na Misungwi;

· Tulitayarisha miswada ya Sheria ya Mipango miji na Vijiji, na Sheria ya kusimamia maadili ya Maafisa Mipangomiji;

· Tuliandaa mipango ya uendelezaji upya maeneo ya kati ya miji miwili ambayo ni Tanga na Singida, na eneo la upanga Jijini Dar es salaam. Vile vile utekelezaji wa mpango wa uendelezaji upya eneo la Kurasini;

· Tulitambua miliki 10,842 kwenye maeneo yaliyojengwa kiholela na kupanga maeneo ya pembezoni mwa jiji la Dar es salaam. Hadi sasa jumla ya miliki 230,000 zimetambuliwa na leseni za makazi 75,000 zimetolewa;

· Tuliandaa Rasimu ya Sera ya Maendeleo ya Nyumba;

· Tulitayarisha Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi, Mipango ya Matumizi ya Wilaya 13 na Mipango ya Matumizi ya Vijiji 172 nchini;

· Tulisikiliza na kuamua mashauri ya ardhi na nyumba 4,180;

· Tuliunda mabaraza ya ardhi na nyumba katika wilaya 10;
· Tulikarabati majengo kwa ajili ya ofisi za mabaraza katika wilaya 5;

· Tulitoa elimu ya Sheria ya Mahakama za Ardhi kwa kusambaza Mwongozo wa Sheria hiyo katika mikoa 8 ya Mara, Mwanza, Morogoro, Tanga, Ruvuma, Arusha, Manyara na Dar es Salaam;

· Tulifanya utafiti kuhusu vifaa vya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu, teknolojia rahisi za ujenzi na kusambaza matokeo yake kwa kuendesha semina katika wilaya 4 na mafunzo kwa vitendo katika wilaya 7;

· Tulikusanya kodi ya pango la nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)* ya jumla ya Shilingi bilioni 17.5. Tulijenga nyumba mpya za kuuza au kupangisha katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma na Kigoma kwa kushirikiana na sekta binafsi

au kwa mtaji wa shirika la nyumba la taifa. Tulizifanyia matengenezo nyumba zapatazo 2728 za National Housing;

· Tuliimarisha ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi na maduhuli yatokanayo na huduma za ardhi katika vituo 117;

· Tulirudisha asilimia 20 ya makusanyo kwenye vituo vya Makusanyo kwenye Halmashauri za miji na Wilaya na kukagua vituo 73 vya makusanyo;

· Tuliingiza kwenye Kompyuta Viwanja 300,820 na mashamba 5,233 katika Halmashauri 85 nchini ili kurahisisha utoaji wa huduma katika Halmashauri husika;

· Tulikamilisha ujenzi wa mfumo wa masjala ya Ardhi unaotumia teknolojia ya kompyuta *(Computerised Movable Shelves);*

· Tulikamilisha ujenzi mfumo wa Menejimenti ya Mifumo ya Habari za ardhi *(Management of Land Information Systems (MOLIS)* umekamilika;

· Tulikamilisha ujenzi wa tovuti ya Wizara *(www.ardhi.go.tz);*

· Tulikamilisha ujenzi wa mtandao wa mawasiliamo ya Wizara unaounganisha Ofisi za Usajili wa Hati za kanda kati ya miji ya Mwanza, Mbeya, Dodoma, Moshi na Ofisi za Ardhi katika manispaa za Kinondoni, Ilala na Temeke;

· Tuliboresha mazingira ya kazi na kuwezesha watumishi 272 kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi. Pia, tuliajiri watumishi wapya 93 ambapo kati ya hawa wanawake ni 37 na kupandisha vyeo watumishi 109;

· Tulikamilisha ujenzi wa jengo la Idara ya Mifumo ya Habari *(Management Information Systems);*

· Tuliimarisha na kujenga nidhamu na uadilifu kwa lengo la kuleta ufanisi katika kazi; na

· Tuliendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanya mengi lakini kama nilivyosema awali hizo ni baadhi tu ya kazi tulizozifanya mwaka 2006/2007. Aidha tumefafanua zaidi katika kitabu cha hotuba yangu mliyogawiwa baadhi ya kazi tulizofanya Mwaka wa Fedha wa 2006/2007 katika majedwali namba 1 – 12.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwelekeo wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2007/08, mwelekeo wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2007/08 umelekezwa kwa kina kuanzia aya ya 11 – 89 katika hotuba yangu. Mwelekeo huu umelenga katika kutekeleza, Ibara ya 42 na 68 za Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi Mkakati wa Kukuza na

Kupunguza Umaskini yaani Tanzania (MKUKUTA) hususani malengo ya Milleneum katika sekta Ardhi na Makazi na pia Mkakati wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA). Hivyo kazi zifuatazo zitapewa kipaumbele katika utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka huu wa fedha.

- Upimaji wa mipaka ya vijiji; uimarishaji wa mipaka ya Kimataifa; utoaji wa hati za kumiliki ardhi kimila;

- Uhamasishaji ujenzi wa masjala za ardhi kwa ajili ya usajili wa hati katika ngazi za vijiji na wilaya; uchoraji wa ramani za msingi;
- Uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya miji ya muda mrefu na mfupi;

- Ujenzi wa nyumba kwa ajili ya uuzaji na upangishaji;

- Uandaaji wa Kanuni na utekelezaji wa Sheria za Kupanga Miji na Vijiji na Sheria ya Maadili ya Maafisa Mipango Miji; na

- Uelimishaji wa umma kuhusu Sera na Sheria za Ardhi na uongezaji makusanyo yatokanayo na pango la ardhi.

Mhehsimiwa Naibu Spika, katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka wa Jana 2006/2007 nilieleza bayana kazi ambazo zingetekelezwa na Wizara. Mafanikio yaliyopatikana na Ambato nimeyaeleza katika aya ya 8 ya hotuba yangu, yanatokana na Wizara kutengewa bilioni 18,274,683,000 katika mwaka wa fedha 2007/2008 Serikali imetenga shilingi bilioni 14,691,991,000. Kiasi hiki kimepungua kwa asilimia 19, upungufu huu unatoka na Serikali kuamua kuelekeza nguvu zake katika shughuli kikamilifu vipaombele ambavyo matokeo yake baada ya kutekelezwa vitapunguza kero zinazowakabili moja kwa moja wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa kuzingati tengeo hilo la bajeti ya Serikali kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, katika mwaka wa fedha 2007/2008 naomba nieleze kwa muhtasari kazi zitakazotekelezwa kazi hizo ni pamoja na Idara ya Huduma na Maendeleo ya Ardhi tutasajili hati na nyaraka mbalimbali zipatazo 20,000; Tutatoa mafunzo ya Sera sheria ya Ardhi ujenzi ukarabati na uzinduzi wa masjala ya ardhi katika wilaya 16 na vijiji 78.

Katika jukumu hili ningependa nisisitize kuwa utekelezaji wa sheria za ardhi wa vijiji namba 5 ya mwaka 1999 unatakiwa ufanywe na Halmashauri, hivyo nazikumbusha kwa mara nyingine tena Halmashauri zote nchi kutimiza wajibu huu kwa kutumia fulsa zilizopo kuanzisha masjala za ardhi za vijiji na wilaya na kutoa elimu ya sera na sheria hii kwa wananchi na watendaji katika maeneo yao.

Waheshimiwa Wabunge nia na lengo la Serikali ni kufungua masjala za vijiji na wilaya ili kurahisisha mchakato na kuwamilikisha wananchi hati miliki za mila ambazo ni dhamana tosha ya kuwawezesha kupata mikopo kutoka taasisi fedha hapa nchini.

Wakipata mikopo hii itawasaidia quinua maisha yao na hivyo kutekeleza azma ya Serikali ya kumpatia mtanzania maisha bora. Tutatoa huduma ya uthamini itakayoliingizia taifa karibu shilingi bilioni 250, tutakusanya maduhuli ya Serikali kiasi cha shilingi bilioni 11, 091,832,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili pia natoa rai kwa Halmashauri zote nchini kutoa kipaumbele kazi za kukusanya na kudhibiti kodi ya pango la ardhi, kazi hii ni muhimu sana kwa kuongeza pato la Serikali kama mnavyofahamu mapato haya ni lazima asilimia 20 irejeshwe kwenye Halmashauri kwa ajili ya shughuli za sekta ya ardhi na makazi. Kwa hiyo asilimia hii 20 ni chanzo kingine cha mapato kwa Halmashauri kwa ajili ya sekta ya ardhi na makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma Za Maendeleo Ya Ardhi, Ardhi ni rasilimali muhimu katika kuwapunguzia wananchi umasikini. Kwa kutambua hilo, Wizara yangu imeendelea na utoaji wa hatimiliki, utwaaji ardhi kwa manufaa ya umma, ukaguzi na uhakiki milki kwa ajili ya utatuzi wa migogoro kiutawala, usajili wa hatimiliki pamoja na nyaraka mbalimbali, utoaji vibali vya uwekaji rehani hakimiliki za ardhi na uhamisho wa milki, uthamini wa mali, uasisi wa masjala za Wilaya na Vijiji sambamba na utoaji elimu kwa umma kuhusu Sheria za Ardhi.

Vilevile Wizara imeendelea na jukumu lake la kuchapisha na kusambaza fomu za aina mbalimbali za kisheria kwa ajili ya umilikishaji ardhi katika Halmashauri zote nchini.

Pamoja na kutoa huduma hizo, Wizara iliendelea na ukusanyaji wa maduhuli kutoka vyanzo mbalimbali vinavyohusiana na huduma za ardhi hususan kodi ya pango la ardhi na ushuru au ada za miamala ya ardhi kama vile uhamisho na uwekaji rehani wa milki za ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa Fedha 2006/2007, jumla ya hati 9,107 zilitayarishwa. Kati ya hizo 6,610 zilitoka Halmashauri na 2,497 ziliandaliwa na Wizara chini ya mradi wa viwanja 20,000 Dar es Salaam (Jedwali Na. 1). Vilevile mashamba 87 yako katika hatua mbalimbali za uhawilishaji kwa mujibu wa Sheria ya ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999 (Sura 114).

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza uhakika wa Watanzania kumiliki ardhi yao na kuitumia kujipatia mitaji, Wizara katika mwaka wa fedha 2007/2008 itaendelea kuweka mazingira bora ya utayarishaji hati ikiwa ni pamoja na kuboresha uwekaji wa kumbukumbu za umilikaji ardhi ambapo lengo litakuwa ni kutayarisha hati zipatazo 8,000. Kwa lengo hili Wizara itaendelea kuhakikisha nyaraka muhimu za kutayarisha hati zinapatikana hadi kwenye Halmashauri kwa wakati.

Ukaguzi na Uhakiki Miliki kwa Ajili ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Kinondoni ilibuni mkakati maalum wa kuhakiki miliki na maendelezo katika maeneo yasiyoendelezwa kwa muda mrefu. Malengo ya mkakati huu ni kujenga hazina ya kumbukumbu sahihi na salama, kuboresha ukusanyaji kodi na kuandaa hatimiliki.

Mkakati huo unatekelezwa katika maeneo ya Mbezi, Jangwani Beach, Tegeta, Ununio na Boko yenye jumla ya viwanja 14,531 vilivyopimwa. Licha ya viwanja hivyo kumilikishwa kuanzia mwaka 1986 idadi kubwa ya viwanja hivyo havijaendelezwa kikamilifu. Mpaka sasa viwanja 10,031 vimehakikiwa kwa kutumia picha za anga na ukaguzi. Kati ya hivyo, viwanja vilivyoendelezwa ni 5,014, vyenye maendelezo hafifu ni 2,497 na ambavyo havijaendelezwa kabisa ni 2,520. Uhakiki huu umesaidia Wizara kutatua migogoro ya muda mrefu na kuchochea kasi ya uendelezaji wa maeneo hayo. Aidha, napenda kuwakumbusha na kuwatahadharisha wavamizi wa viwanja kuwa kwa mujibu wa kifungu cha 175 cha Sheria ya Ardhi Na.4 ya Mwaka 1999, kufanya maendelezo kwenye kiwanja chenye miliki halali ya mtu bila ridhaa yake ni kosa. Hivyo, mvamizi anatakiwa ama abomowe jengo lake ili kumpisha mmiliki halali au afanye makubaliano ya Kisheria na mmiliki halali wa kiwanja husika. Hii ndiyo Sheria na ni lazima ifuatwe na itekelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2007/2008 Wizara inakusudia kukamilisha uhakiki wa miliki za viwanja 4,500 vilivyobaki na kuendelea kubadilisha hati katika viwanja husika toka hati ya miaka 33 hadi kufikia miaka 99. Aidha, katika mwaka 2007/08 Wizara yangu itatengeneza baadhi ya barabara katika maeneo husika. Natoa wito kwa Halmashauri zote nchini kuendelea kuhakiki miliki za viwanja na mashamba katika maeneo yao ili kupunguza migogoro ambayo inaweza kuepukika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara yangu imebatilisha miliki za viwanja na mashamba 637 katika mikoa mbalimbali hapa nchini, imeidhinisha vibali vya uhamisho wa miliki 1,352 na vibali vya rehani 594. Pia katika kipindi hicho mashauri 61 yanayohusu ardhi yalishughulikiwa na Mahakama. Katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri zote nchini itaendelea kuwahamasisha wamiliki kuendeleza viwanja na mashamba yao. Hata hivyo pale ambapo watashindwa kufanya hivyo wizara yangu itachukua hatua za kupendekeza kwa Mheshimiwa Rais kufuta miliki hizo na kisha kumilikisha wananchi wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Usajili wa Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2006/2007, Wizara ilikuwa na lengo la kusajili hatimiliki na nyaraka za kisheria 12,000. Lengo hilo limevukwa kwa kusajili hatimiliki na nyaraka za kisheria zipatazo 22,139. Kati ya hizo, hatimiliki na nyaraka 16,090 zimesajiliwa chini ya Sheria ya Usajili Ardhi (Sura 334) (Jedwali Na. 2); Nyaraka 5,423 zimesajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Nyaraka (Sura 117) (Jedwali Na. 3); na dhamana 626 zimesajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Dhamana zihamishikazo (Sura 210).

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mwamko wa wananchi kusajili hati na nyaraka mbalimbali, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2007/2008 Wizara yangu itaendelea kuongeza kasi na idadi ya kutoa hatimiliki kwa wananchi kwa kuimarisha ofisi ya Msajili wa Hati kuwezesha kusajili hatimilki za ardhi na nyaraka za kisheria ambapo lengo ni kusajili hati na nyaraka 20,000. Pia, kufanya mapitio Sheria za usajili ardhi na

nyaraka kwa lengo la kuziboresha ili kwenda na wakati na kutoa huduma kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Wizara yangu inawajibika kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka 1999 inayohusika na umilikishaji wa ardhi vijijini. Chini ya Sheria hiyo Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri imekuwa ikitoa elimu kuhusu miliki ya ardhi vijijini, ujenzi na ukarabati wa Masjala za Ardhi za Wilaya na za Vijiji, kutoa vyeti vya Ardhi ya Kijiji na kusajili Hatimiliki za Kimila. Tangu zoezi lilipoanza mwaka 2003/2004 jumla ya masjala 7 za ardhi za Wilaya na 37 za Vijiji za mfano zimeanzishwa. Katika mwaka wa fedha 2006/2007 Masjala za Wilaya 7 na Vijiji 14 ziko katika hatua mbalimbali za ujenzi, Wilaya 53 na Vijiji 412 vimekaguliwa kwa lengo la kuhamasisha ujenzi wa masjala. Aidha, Vyeti vya Ardhi ya Vijiji 211 na Hati za Hakimiliki za Kimila 3,940 zimetolewa kwa wanavijiji na hivyo kufanya idadi kamili ya vyeti ambavyo vimetolewa kuwa 402 na Hati za Hakimiliki za Kimila 5,202.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua kwamba hati za kumiliki ardhi zinamwezesha mwananchi katika kujiletea maendeleo yake wizara itaendelea kushirikiana na Halmashauri kuhakikisha wananchi wengi zaidi vijijini wanamilikishwa ardhi yao. Katika mwaka wa fedha 2007/2008 Wizara ina lengo la kuendelea kutoa elimu, kuhamasisha ujenzi, ukarabati na uzinduzi wa masjala za Ardhi za Wilaya 16 na Vijiji 78.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeendelea kutoa elimu ya Sera, Sheria za Ardhi na matumizi bora ya ardhi katika Wilaya mbalimbali. Mfano Wizara imekuwa ikisisitiza kuwa, kwa mujibu wa Sera ya Ardhi ya Mwaka 1995 kila kipande cha ardhi kina thamani na kwamba kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya Mwaka 1999 kifungu cha 3 (g) na kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na.4 ya Mwaka 1999 kifungu cha 3 (g) ardhi yote inayotwaliwa kwa mtu yeyote kwa ajili ya matumizi yoyote ni lazima mhusika wa ardhi hiyo alipwe fidia. Katika mwaka 2006/07 Wizara imeendesha mafunzo katika wilaya 23 na Vijiji 172. Utayarishaji wa vipindi na makala ya elimu ya Sera na Sheria za Ardhi kupitia *Television*, radio na magazeti ulifanyika. Aidha, nakala 2,012 za Sheria ya Ardhi ya Vijiji na kanuni zake na vijarida 5,270 vya Mwongozo wa kutoa Elimu ya Sheria ya Ardhi ya Vijiji zilisambazwa sehemu mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaona kuwa utekelezaji wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji bado unaenda kwa kasi ndogo sana. Hii inatokana na Halmashauri kutotimiza majukumu yao katika kutekeleza Sheria hii. Pia, Halmashauri hazitumii fursa zilizopo za asasi zisizo za kiserikali katika kutekeleza sheria hii. Ningependa kusisitiza kuwa jukumu la utekelezaji wa Sheria hii ni la Halmashauri. Hivyo Wizara yangu inazikumbusha Halmashauri kutimiza wajibu wao na kutumia fursa zilizopo kuanzisha Masjala za Ardhi za Vijiji na Wilaya na kuendelea kutoa elimu ya Sera na Sheria ya Ardhi ya Vijiji kwa wananchi na watendaji katika maeneo yao. Katika mwaka wa 2007/08 Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Halmashauri zote nchini kutoa elimu ya mafunzo ya sera na

sheria za ardhi. Aidha, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uthamini wa Mali, Wizara imeendelea na majukumu ya kuthamini nyumba na mali nyinginezo kwa madhumuni ya kulipa fidia, kutoza kodi ya ardhi, mauzo *(transfer),* mizania *(balance sheet)*, kuweka rehani, kuomba mikopo, mirathi na bima. Katika mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara iliweka lengo la kuthamini nyumba na mali nyinginezo 2000. Hadi kufikia Juni 2007 jumla ya nyumba na mali nyinginezo zipatazo 5,519 zilithaminiwa na kuingizia serikali jumla ya shillingi 240,825,800. Katika Mwaka 2007/2008 Wizara itaendelea kutoa huduma za Uthamini ambazo zinakadiriwa kuingizia serikali jumla ya shilingi 200,000, 000. Pamoja na kazi za kutoa huduma za Uthamini, Wizara inaandaa sheria ya kusimamia kazi za Uthamini na Wakala wa Miliki *(Real Estate Agency).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ina wajibu wa kuandaa kumbukumbu ya viwango vya uthamini *(Valuation Data Bank)* kwa lengo la kuwezesha uthamini wa mali mbalimbali kufanyika kulingana na bei ya soko. Hadi Juni 2007 idadi ya kumbukumbu za taarifa za uthamini wa mali mbalimbali imefikia 821,973 ambazo tayari zimeingizwa kwenye kompyuta. Kwa vile thamani ya ardhi na nyumba kimsingi hupanda kutokana na mabadiliko ya hali ya uchumi wa nchi mwaka hadi mwaka zoezi hili litaendelea kuwa la kudumu ili kuwa na viwango vinavyoendana na thamani ya soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukusanyaji wa Maduhuli katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 Wizara yangu ina lengo la kukusanya kiasi cha Shilingi 11,091,832,000; Maduhuli haya yatakusanywa kwa kutumia mikakati ifuatayo:-Kuelimisha wananchi kwa kutumia matangazo kwa njia ya televisheni, radio na magazeti; kufuatilia kwa karibu vituo vya makusanyo katika Halmashauri za Miji na Wilaya ili kuthibiti mapato na sheria za fedha; kujenga uwezo na kuboresha vituo vya makusanyo kwa kuvipatia vifaa mbalimbali zikiwemo Kompyuta na programu ya kukadiria kodi, kutunza kumbukumbu na kujibu hoja mbalimbali; na, kuboresha hazina ya kumbukumbu za ardhi. Natoa wito kwa Halmashauri kutoa kipaumbele katika suala la ukusanyaji na udhibiti wa kodi ya pango la ardhi kwani hayo ni mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kumbukumbu za Ardhi na Mawasiliano, Wizara yangu imetoa kipaumbele katika kuboresha mifumo ya habari na mawasiliano kwa lengo la kuboresha huduma kwa wananchi. Katika jitihada za kuimarisha hazina ya kumbukumbu, kazi ya kuingiza kumbukumbu kwenye kompyuta inaendelea. Hadi kufikia mwezi Mei 2007, taarifa za viwanja 300,820 na mashamba 5,233 zilibainishwa na kuingizwa kwenye kompyuta (Jedwali Na. 4.).

Pamoja na juhudi za kuimarisha matumizi ya kompyuta na kuboresha mawasiliano Makao Makuu na ofisi za Kanda za Usajili wa Hati, Wizara yangu imeazimia kuendelea kusambaza taaluma na matumizi ya kompyuta katika Ofisi za Ardhi za Halmashauri. Hadi sasa Wizara imepeleka taaluma na kompyuta katika Halmashauri 5 ambazo ni Manispaa za Morogoro, Moshi, Arusha na jiji la Mwanza na Mbeya. Katika mwaka wa fedha 2007/2008 Wizara itaendelea kuboresha kumbukumbu za ardhi pamoja na mkakati wa kuziwezesha ofisi za Ardhi za Halmashauri nyingine 6 katika matumizi ya

teknolojia ya habari na mawasiliano. Lengo ni kuboresha huduma na kupanua wigo wa makusanyo. Natoa wito kwa Halmashauri zote nchini kuwasilisha takwimu za viwanja na mashamba ili ziweze kuingizwa kwenye Hazina ya kumbukumbu za Wizara na hivyo kuboresha huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mabaraza Ya Ardhi Na Nyumba Wizara yangu ina jukumu la kusimamia Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na.2 ya mwaka 2002. Baada ya kuanza kutumika kwa sheria hiyo mwaka 2003 kumekuwa na ongezeko la mashauri yanayofunguliwa katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kutokana na wananchi kuelewa thamani ya ardhi. Kati ya Julai, 2006 na Mei 2007, mashauri 10,382 yalifunguliwa. Ongezeko hili limesababisha kuwepo kwa mlundikano wa kesi. Ili kukabiliana na tatizo hili Wizara katika mwaka 2006/2007 imeendelea kuunda Mabaraza mengine katika wilaya 10 zenye migogoro mingi ya Ardhi. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru viongozi wote wa mikoa na wilaya waliotoa majengo/ofisi kwa ajili ya Mabaraza hayo. Pamoja na kuunda Mabaraza mapya, Wizara imejitahidi kupata ufumbuzi wa tatizo la mlundikano wa kesi kwa kuongeza idadi ya vikao katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya katika Mkoa wa Dar es Salaam. Jitihada hizo zimewezesha kuamua jumla ya mashauri 4,180 katika mwaka 2006/2007 (Jedwali Na. 5). Aidha, Baraza la Rufaa la Ardhi (ambalo liliongezewa muda) limeamua jumla ya rufaa 61.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika mwaka 2007/08 Wizara itaendelea kuunda Mabaraza mengine katika wilaya 5 kwa kujenga na kukarabati majengo ambayo yanatolewa na Wilaya, ili kuongeza idadi ya Mabaraza kulingana na fedha iliyotengwa katika mwaka huu. Pia, utaratibu uliotumika Dar es Salaam wa kuongeza idadi ya vikao utatumika katika mikoa mingine yenye mlundikano wa kesi. Natoa wito kwa uongozi wa Mikoa na Wilaya kutoa majengo yatakayotumika kwa uendeshaji wa Mabaraza hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo mpya wa utatuzi wa migogoro ya Ardhi na Nyumba unaoanzia ngazi ya Kijiji na Kata una lengo la kuwapunguzia wananchi gharama za kusafiri umbali mrefu kupata haki zao. Katika mwaka 2006/2007 kumekuwa na jitihada za kuanzisha Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Kata katika Halmashauri mbalimbali nchini. Pamoja na kuanzishwa Mabaraza hayo kuna upungufu katika uendeshaji wake. Kwa sababu hiyo, katika mwaka wa fedha 2007/2008 Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, itaandaa mkakati wa kuimarisha utendaji wa kazi katika Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Kata ili mashauri yasiyo na ulazima wa kwenda ngazi za juu yasikilizwe na kutolewa uamuzi katika ngazi hizo. Natoa wito kwa viongozi wa Halmashauri za Wilaya ambazo hazijaunda mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Kata wayaunde ili kutatua migogoro mingi ya ardhi na nyumba katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma za Upimaji na Ramani, Wizara yangu inaendelea na utekelezaji wa majukumu yake ya upimaji ardhi na utayarishaji wa ramani za msingi kwa nchi nzima ambazo huonyesha hali halisi ya sura ya nchi na maendelezo yaliyo juu yake. Ramani hizo ni chanzo muhimu cha taarifa zinazohitajika katika kubuni na kutayarisha mipango ya matumizi mbalimbali ya ardhi. Utayarishaji wa ramani za

msingi ni ghali na zinachukua muda mrefu kwa kuwa huhitajika ndege maalumu ya kupiga picha za anga. Vile vile utayarishaji wa ramani unahitaji vifaa vya kisasa ambavyo ni ghali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utayarishaji wa Ramani katika mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara yangu ilipanga kupiga picha za anga na kutayarisha *digital orthophotos* za miji ya Mbeya na Morogoro kwa ajili ya kuendeleza Mradi wa kupima viwanja na kudhibiti ujenzi holela. Vile vile, Wizara yangu iliahidi kupiga picha za anga katika Kanda ya Mashariki inayojumuisha miji 128 katika Mikoa ya Pwani, Tanga, Kilimanjaro, Manyara, Arusha, Singida, Dodoma na Morogoro. Kazi hizo hazikufanyika kutokana na mawingu kuendelea kutanda angani katika maeneo hayo, inatarajiwa kazi hizo zitafanyika katika mwaka wa fedha 2007/2008.

Aidha, uchoraji na uhakiki uwandani wa ramani za miji 41 kanda ya ziwa inayojumuisha mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Kagera na Mara umekamilika. Aidha, uchoraji wa ramani za miji 47 Kanda ya Magharibi inayojumuisha mikoa ya Kigoma, Tabora, Rukwa, Mbeya na Iringa uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji baada ya kazi ya uwianishaji wa ardhi *(Ground Photo Control)* na picha za anga za mwaka 2006 kukamilika. Upigaji wa picha za anga na utayarishaji wa *digital orthophoto* katika Jiji la Dar es salaam, umeendelea kusitishwa kutokana na hali ya mawingu kuendelea kutanda angani. Kazi hii itafanyika katika mwaka wa fedha 2007/08 kutegemea hali ya hewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ili kuhakikisha kuwa miji yetu inatayarishiwa mipango bora ya kuiendeleza kabla haijajengwa kiholela hatuna budi kuandaa ramani za msingi mapema. Katika mwaka wa 2007/08 Wizara yangu imepanga kupiga picha za anga na kuchora ramani za msingi katika miji ya Mbeya na Morogoro. Vile vile kwa lengo la kuwezesha mipango mingine ya maendeleo, ramani za uwiano wa 1:50,000 zitahuishwa kwa kutumia *satellite images* na kuingizwa kwenye mfumo wa kompyuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Upimaji Majini *(Hydrographic Surveying)* Wizara yangu ina jukumu la kupima na kuandaa ramani za maeneo ya ardhi kwenye maji ndani ya Bahari na Maziwa makubwa kwa nia ya kuimarisha usalama wa vyombo vya usafiri majini pamoja na kuainisha rasilimali zilizomo. Ili kufanikisha azma hiyo Wizara kwa kushirikiana na Shirika la *International Hydrographic Organisation (IHO)* imeendelea na hatua ya kujenga uwezo wa kitaalamu na vifaa. Katika ushirikiano huo Wizara imepokea ramani za majini *(Hydrographic Charts)* za baadhi ya bandari zilizopo mwambao wa bahari ya Hindi kwa ajili ya uhuishwaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeridhia mkataba wa Kimataifa wa Sheria za Bahari *(The United Nations Convention on the Law of the Sea (UNCLOS)* wa kutambua na kudai eneo la nyongeza nje ya eneo la ukanda wa kiuchumi *(Exclusive Economic Zone)* lijulikanalo kitaalam kama *Extended Continental Shelf*. Eneo hilo ni muhimu kwa maliasili zilizopo baharini kutokana na ongezeko la miliki ya nchi. Tafiti zilizofanyika na taasisi mbalimbali katika maeneo kama hayo zinaashiria upatikanaji wa raslimali mbalimbali. Ili Serikali iweze kumiliki eneo hilo ni lazima lipimwe na ramani zake kuwasilishwa Umoja wa Mataifa kabla ya mwaka 2009. Katika kazi hii, Wizara yangu

inahusika na masuala ya Haidrografia *(Hydrography)* na Jiodesia *(Geodesy).* Wadau wengine ni Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Shirika la Maendeleo ya Petroli ambao wanahusika na Jiofizikia *(Geophysics)* na Jiolojia *(Geology).* Hivyo, Wizara yangu itashirikiana na wadau wengine ili tusipoteze fursa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Upimaji MilikiWizara yangu katika mwaka 2006/2007 iliendelea kushirikiana na Halmashauri mbalimbali ili kuzijengea uwezo wa kutoa huduma za upimaji miliki na kuweka kumbukumbu za ardhi kwa kutumia teknolojia ya kisasa. Mikoa ya Mwanza, Arusha, Shinyanga, Iringa, Mbeya na Ruvuma imeanza kuhifadhi kumbukumbu za upimaji katika kompyuta. Pia mikoa hii imepatiwa software kwa ajili ya kurahisisha kazi za upimaji ardhi na uandaaji ramani. Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam zimepatiwa plani pepe *(digital survey plans)* zisaidie katika kuandaa plani za hati *(deed plans).* Warasimu ramani kutoka Halmashauri hizo wamepata mafunzo ya kutumia plani pepe na namna ya kuandaa plani za hati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara yangu imeidhinisha plani za upimaji zenye jumla ya viwanja 16,312 na mashamba 712 kutoka kwenye Halmashauri mbalimbali. Kasi ya upimaji viwanja na mashamba ni ndogo ukilinganisha na mahitaji kutokana na Halmashauri nyingi kutokuwa na wataalamu na vifaa vya kutosha. Ili kuimarisha shughuli za upimaji nchini natoa wito kwa Halmashauri kuajiri wataalamu na kutenga fedha katika bajeti zao kwa ajili ya kununulia vifaa vya kisasa vya Upimaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miji yetu inaendelea kukua hivyo mahitaji ya viwanja mijini nayo yanaongezeka. Kwa kutambua mchango wa ardhi katika maisha, wananchi wengi wanajitokeza kuchangia gharama za upimaji wa viwanja na mashamba. Hati miliki za ardhi zimewasaidia wananchi kwa shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na dhamana kwa mikopo. Haya ni mafanikio ya utekelezaji wa dhati wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania. Katika mwaka 2007/2008 Wizara yangu itasimamia upimaji miliki wa viwanja 18,000 na mashamba 1,000 katika Halmashauri mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Upimaji Viwanja Mijini, Wizara yangu itaendelea kutekeleza Mradi wa Upimaji wa Viwanja katika miji ya Dar es Salaam, Mwanza, Morogoro na Mbeya. Hadi sasa jumla ya viwanja 49,228 katika miji hii vimepimwa. Katika Jiji la Dar es Salaam, jumla ya Viwanja 34,314 vimepimwa kwa gharama ya Shilingi bilioni 30.31 tangu mradi ulipoanza mwaka 2002/2003. Katika Jiji la Mwanza jumla ya viwanja 9,800 vimepimwa kwa Shilingi milioni 830. Halmashauri ya Jiji la Mbeya imepima viwanja 2,350 kati ya viwanja 5,000 kwa Shilingi milioni 600. Vile vile Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro imepima viwanja 2,764 kati ya viwanja 4,000 kwa gharama ya Shilingi milioni 400. Hii inaonyesha kuwa dhana ya uchangiaji gharama za upimaji imeeleweka vizuri kwa wananchi na hivyo kuufanya Mradi huu kuwa endelevu. Wizara yangu itaendelea kuziwezesha Halmashauri zilizo tayari kuanzisha na kutekeleza miradi ya upimaji viwanja mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika mwaka wa fedha 2006/2007 nililitaarifu Bunge lako tukufu juu ya Mfuko Maalum wa Kupima Viwanja (*Plot Development Revolving Fund (PDRF*) ulioanzishwa mwaka 1993. Hadi Juni, 2006 jumla ya Halmashauri 32 zilikopeshwa jumla ya Shilingi 399,112,613 (Jedwali Na.6) na hadi kufikia Julai 2007 Halmashauri 14 za Ileje, Nkasi, Mpanda, Sumbawanga, Kibaha, Hanang, Kondoa, Njombe, Hai, Bukoba Vijijini, Kigoma Vijijini, Manispaa ya Mtwara, Jiji la Mbeya na Tanga zilikamilisha marejesho yenye jumla ya Shilingi 143,597,115. Nazipongeza sana halmashauri hizi, hata hivyo bado Halmashauri na Taasisi 18 hazijakamilisha marejesho yenye jumla ya Shilingi 255,515,498, Halmashauri na Taasisi hizo ni pamoja na Monduli, Babati, Kondoa, Maswa, Tarime, Iringa (V), Mufindi, Mbalali, Mwanga, Songea (V), Tunduru, Masasi, Newala, Ruangwa, Liwale, Bagamoyo pamoja na *CDA,* na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Napenda kutoa wito kwa wahusika wote kurejesha fedha walizokopa mapema. Bado nasisitiza kuwa lengo la Wizara ni kuufanya Mfuko uwe endelevu ili kuziwezesha Halmashauri kupima viwanja mijini. Kutorejesha kunazinyima fursa halmashauri nyingine kunufaika na Mfuko huu. Katika mwaka 2007/2008 Halmashauri 19 zitakopeshwa jumla ya Shilingi 416, 002,381 kwa ajili ya upimaji viwanja mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Upimaji wa mipaka ya vijiji ni hatua ya kwanza ya utekelezaji wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya Mwaka 1999 (sura 114). Sheria hii iliandaliwa ili kuwezesha upangaji wa matumizi endelevu ya ardhi na uhifadhi wa mazingira. Idadi ya vijiji nchini inakadiriwa kufikia 13,000. Hadi Juni 2006 takriban vijiji 6,000 vilikuwa vimepimwa. Katika Mwaka 2006/2007 Wizara yangu iliahidi kupima mipaka ya vijiji 3,104. Hadi Juni 2007 jumla ya Vijiji 2,524 (Jedwali Na. 7) sawa na asilimia 81 vimepimwa mipaka yake katika mikoa ya Pwani, Lindi, Iringa, Mbeya, Rukwa, Kigoma, Kagera, Shinyanga na Tanga. Kutokana na tengeo la fedha la mwaka 2006/2007 kazi iliyofanyika ni kubwa ikilinganishwa na upimaji uliofanywa kwa kipindi cha zaidi ya miaka 20 iliyopita. Ni dhahiri kuwa tukiendelea kutengewa fedha za kutosha tunaweza kukamilisha kazi iliyobakia katika muda wa miaka mitatu hadi minne.

Katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu itaendelea na upimaji wa mipaka ya vijiji katika Mikoa sita. Natoa rai kwa mamlaka za Mikoa, Halmashauri za Wilaya na Serikali za Vijiji ambako vijiji vimepimwa, kuchukua hatua za makusudi na kujenga tabia na utamaduni wa kulinda na kutunza mipaka yao ili idumu na kuzuia kuzuka kwa migogoro ya mipaka hapo baadae. Mipaka ya vijiji ni msingi wa mipaka ya Wilaya, Mikoa na Taifa, kwa hiyo uimara wake unachangia kuimarisha amani na utulivu na ni ufumbuzi wa migogoro ya mipaka yote nchini. Ni vema ilindwe na kutunzwa wakati wote kwani imeigharimu Serikali fedha nyingi kuipima.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa wananchi wanaoishi katika maeneo yaliyo na Madini hawabughudhiwi, wizara yangu itaendelea kupima maeneo yanayotumiwa na wachimbaji wa Makampuni makubwa ili kuondoa migogoro inayojitokeza kati ya Makampuni hayo na wananchi katika maeneo husika. Kwa kushirikiana na *Tanzania Investment Centre (TIC)* na mikoa Wizara itapima maeneo yanayofaa kwa kilimo cha mashamba makubwa na kuwa na *Land Bank* katika Mikoa yote. Hii itasaidia wawekezaji wanaohitaji mashamba makubwa kuyapata bila usumbufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii Wizara itaandaa mpango utakaowezesha kupima Hifadhi za Taifa zote na hivyo kupunguza migogoro inayojitokeza kati Mamlaka za Hifadhi hizo na wananchi. Aidha, Wizara itaendelea kutoa hati kwa mashamba na ranch zilizokuwa mali ya Serikali ambazo kwa sasa ranch hizo zimemilikishwa kwa watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mipaka ya Kimataifa, Wizara yangu inalo jukumu la kukagua na kupima mipaka ya kimataifa. Ili kutekeleza jukumu hili, Wizara yangu ilifanya mawasiliano na nchi jirani za Kenya, Uganda, Burundi, Malawi, Msumbiji na Comoro kwa lengo la kupanga ukaguzi na uimarishaji wa mipaka hiyo. Katika mwaka wa fedha 2006/2007 Tanzania na Msumbiji zilifanya ukaguzi wa pamoja wa mpaka wa nchi kavu kutathmini gharama za kuimarisha mpaka huo kwa kusimika mawe ya ziada. Pia, mikutano kati ya Tanzania, Uganda na Kenya ilifanyika kujadili jinsi ya kurudishia baadhi ya mawe ya mipaka yaliyoharibiwa na kuandika upya protokali za mipaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kutokana na uamuzi wa Viongozi wa nchi zinazounda Umoja wa Afrika (*African Union)* kuwa mipaka ya kimataifa ya nchi hizo iwe imetambuliwa, kuainishwa, kuhakikiwa na kupimwa ifikapo mwaka 2012, Wizara yangu itahakikisha kwamba mipaka yote na nchi jirani inashughulikiwa ipasavyo kabla ya muda huo. Natoa wito kwa wadau wote katika suala hili kushirikiana kukamilisha jukumu hili. Katika kipindi cha mwaka 2007/2008, Wizara yangu itaendeleza juhudi za kufanya mashauriano ya pamoja kati ya Tanzania, Comoro na Msumbiji ili kukamilisha mpaka katika Bahari ya Hindi. Aidha, Mawasiliano na serikali za Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Rwanda yatafanyika ili kuanza kushughulikia mipaka hiyo ikiwa ni pamoja na uendelezaji wa programu inayohusu mpaka kati ya Tanzania na Malawi katika Mto Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika Mipaka ya Ndani ya Nchi, Mwaka jana nililitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa chanzo kikubwa cha migogoro ya mipaka ni mamlaka za utawala za Wilaya kutokufahamu wala kujishughulisha na mipaka rasmi ya maeneo yao. Ili kutatua migogoro hiyo, Wizara yangu imesambaza nakala za Tangazo la Serikali *(GN*) la mipaka ya Wilaya kwa Wakuu wote wa Mikoa na Wilaya nchini kote. Pia, nilitoa rai kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya nchini kuwa mara wakipata nakala ya *GN* ya mipaka ya wilaya zao, wafanye mikutano ya ujirani mwema ili kujifahamisha na kutambua mipaka rasmi ya Wilaya zao na kujiridhisha na tafsri zake. Kama *GN* ni ya zamani na haitafsiriki, hoja ijengwe na kuwasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI, yenye dhamana ya *GN,* kuomba zihuishwe ili ziendane na hali halisi na kurahisisha tafsiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafurahi kuliarifu Bunge lako kuwa katika mwaka 2006/2007 baadhi ya wilaya zimeanza kushughulikia utatuzi wa migogoro yao. Kwa mfano, taarifa rasmi ya kumalizika kwa mgogoro wa mpaka kati ya Wilaya ya Bukombe na Biharamulo iliwasilishwa. Ninaupongeza uongozi wa Mikoa ya Shinyanga na Kagera kwa hatua hiyo na ninaomba Mikoa na Wilaya nyingine kuiga mfano huo. Vile vile Wizara imepokea nakala za barua kutoka Mikoa na Wilaya kadhaa za kuiarifu TAMISEMI upungufu katika maelezo ya *GN* hasa za zamani na kuomba zihuishwe.

Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI kushughulikia *GN* hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majukumu mengine ya Wizara niliyoyazungumzia awali, Wizara ina jukumu la kusimamia uendelezaji wa makazi hapa nchini kwa kuzingatia Sera ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 na Sheria ya Mipangomiji na Vijiji (Sura 378) ya mwaka 1956 ambayo imerekebishwa na kupitishwa na Bunge lako tukufu mwezi Aprili 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, miji ya Tanzania inakua kwa kasi. Idadi ya watu katika miji yetu imekuwa ikiongezeka kwa wastani wa asilimia 4.5 kwa mwaka. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2002, Tanzania ilikuwa na watu 34,443,603 kati ya hao asilimia 23 walikuwa wanaishi mijini. Hivi sasa nchi yetu inakadiriwa kuwa na watu 37,000,000 kati ya hao asilimia 27. wanaishi mijini. Inakadiriwa kuwa ifikapo mwaka 2025, nusu ya Watanzania watakuwa wanaishi mijini. Kutokana na ongezeko kubwa la watu mijini, mahitaji ya makazi yaliyopangwa nayo yanaongezeka lakini uwezo wa Serikali kukidhi mahitaji hayo ni mdogo kutokana na kutokuwepo na rasilimali za kutosha.

Hali hii imesabibisha wastani wa asilimia 75 ya wakazi wa mijini kuishi katika maeneo ambayo hayajapangwa na ambayo hayana huduma muhimu za makazi. Napenda kutoa wito kwa Mamlaka mbalimbali za utawala zikiwemo Halmashauri kutowafukuza wananchi hawa katika maeneo haya kwani Sheria ya Ardhi Na.4 na Na.5 za Mwaka 1999 zinawatambua, ni jukumu la Halmashauri husika kuwaelimisha katika matumizi bora ya ardhi ikiwa ni pamoja na kuyatambua maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya nyumba hapa nchini siyo kuridhisha kwani katika maeneo mengi ya mijini kuna uhaba wa nyumba za kuishi na nyingi ni duni. Watu wengi huishi katika hali ya msongamano na mazingira yasiyoridhisha. Inakadiriwa katika maeneo ya mijini peke yake kuna upungufu wa nyumba milioni 3.

Katika maeneo ya vijijini nyumba nyingi ni duni na hudumu kwa wastani wa miaka 7 tu, hali ambayo hufanya watu wa vijijini kutumia muda wao mwingi katika kukarabati nyumba badala ya kufanya shughuli nyingine za uzalishaji. Ili kuwa na makazi bora Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Miji na Wilaya imekuwa ikiandaa Sera, Sheria na kutekeleza mipango mbalimbali ya makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maendeleo ya Mijo, kama nilivyoeleza mwaka jana Wizara yangu inaandaa mipango ya aina mbili ya kuongoza uendelezaji wa miji. Mipango ya muda mrefu ambayo utekelezaji wake huchukua miaka ishirini (*Master Plans*) na mipango ya matumizi ya ardhi ya muda mfupi ambayo huchukua miaka mitano hadi kumi (*Interim Land Use Plans*).

Katika mwaka wa fedha uliopita Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri husika ilikamilisha mipango ya matumizi ya ardhi ya muda mfupi ya miji ya Tandahimba, Tunduru, Namtumbo, Masasi, Babati, Mererani, Ushirombo na Misungwi. Pia katika

kipindi hicho Wizara ilianza maandalizi ya mipango ya namna hiyo kwa miji ya Mvomero, Kibaigwa, Bunda na Chato. Katika mwaka wa fedha 2007/08 Wizara yangu itakamilisha mipango hiyo na kuandaa mipango kwa ajili ya miji ya Kasulu, Kibondo, Maswa na Kyela.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri husika ilianza maandalizi ya Mipango ya Muda Mrefu *(Master Plans)* kwa jiji la Mwanza na mji wa Mtwara/Mikindani. Katika mwaka wa fedha 2007/2008 Wizara yangu itakamilisha mipango hiyo na kuandaa mpango wa namna hiyo kwa Jiji la Dar es Salaam na Mji wa Kigoma.

Napenda kuhimiza Halmashauri ambazo zina mipango ya muda mrefu au mfupi kuandaa Mipango ya Kina (*Detailed Layouts)*, ili kuweza kupata viwanja vya kupima na kuendeleza.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri husika imekuwa ikiandaa mipango ya kuendeleza upya maeneo ya kati ya miji (*Redevelopment Schemes*). Mipango hii inaandaliwa ili kuwezesha uwekezaji mpya na kuyafanya maeneo hayo yenye thamani kubwa ya ardhi yaweze kuchangia ipasavyo katika uchumi wa miji hiyo na Taifa kwa ujumla. Katika mwaka wa fedha 2006/07, Wizara ilikamilisha mipango ya namna hiyo kwa Jiji la Tanga, mji wa Singida na eneo la Upanga Jijini Dar es Salaam.

Ili kutekeleza Sera ya Makazi ya Mwaka 2000 na kuongeza thamani ya ardhi, napenda nitoe wito kwa wananchi kujenga nyumba za maghorofa katika maeneo yaliyokamilika kupangwa upya. Katika mwaka 2007/08 mipango ya namna hiyo itaandaliwa kwa eneo la kati la mji wa Lindi na kwa maeneo ya Magomeni, *Oysterbay* na Msasani *Peninsular*/Masaki katika Jiji la Dar es Salaam. Aidha, Wizara imepanga kupima eneo la Kigamboni kwa nia ya kuanzisha mji wa kisasa ndani ya Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imekuwa ikitekeleza Mradi wa Kuendeleza Upya Eneo la Kurasini tangu mwaka 2006/07 ili liweze kutumika kwa shughuli zinazohusiana na Bandari na kuwa kitega uchumi kikubwa kwa Taifa. Wizara inaendelea kulipa fidia kwa wakazi wanaohamishwa hatua kwa hatua kulingana na upatikanaji wa fedha ili kuweza kupatikana kwa maeneo huru ya kupima viwanja vikubwa na kumilikisha viwanja hivyo kwa njia ya zabuni.

Katika Mwaka wa fedha 2006/07 jumla ya viwanja vitatu vilipimwa na jumla ya shilingi bilioni 1.77 zilitumika kulipa fidia kwa nyumba zipatazo 134. Wizara imekamilisha kufanya uthamini na kupima viwanja vingine sita ambavyo tayari vimetangazwa kuuzwa kwa njia ya zabuni. Katika mwaka wa fedha 2007/08 Wizara itaendelea na utekelezaji wa Mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yangu ya mwaka jana nililieleza Bunge lako Tukufu kuwa Wizara ilikuwa inahuisha Sheria ya Mipango Miji na Vijiji (Sura 378) ya mwaka 1956 pamoja na Sheria ya Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Na.3 ya mwaka 1984 na kuandaa Sheria ya kusimamia taaluma ya Mipango Miji. Napenda kuchukua nafasi hii kulishukuru Bunge lako Tukufu kwa kutunga Sheria Mpya ambazo ni Sheria ya Mipango Miji, Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi na Sheria ya Kusajili Wataalamu wa Mipango Miji. Katika mwaka 2007/08 Wizara itaandaa Kanuni na Miongozo ya kutekeleza Sheria hizi. Utekelezaji wa Sheria hizo utaboresha hali ya makazi hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2006/07, Wizara ilishiriki katika Mkutano wa 21 wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Makazi (*UN-Habitat*) na Mkutano wa Shirika la Afrika linalotoa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba kwa nchi za Afrika (*Shelter Afrique*).

Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Makazi (*UN-Habitat*) limewezesha vikundi vya akina mama visivyokuwa vya Kiserikali kupata eneo katika Manispaa ya Kinondoni kwa ajili ya kujenga jengo la ghorofa zaidi ya tano kwa njia ya ubia. Katika mwaka wa fedha 2007/08 Wizara itaendelea kushirikiana na Mashirika ya Kimataifa kama *UN-Habitat, United Nations Environment Programme (UNEP), Shelter Afrique* pamoja na Sekta binafsi kubuni njia mbalimbali za kuboresha makazi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mradi wa kutambua miliki katika maeneo yaliyojengwa kiholela, Wizara yangu inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Kutambua miliki katika Jiji la Dar es Salaam kwa kushirikiana na Halmashauri zote. Katika mwaka 2006/07, Wizara ilianza kutekeleza awamu ya pili ya Mradi ambayo inahusu kutambua miliki na kuendeleza maeneo ya pembezoni mwa Jiji la Dar es Salaam.

Katika utekelezaji huo miliki 10,842 zilitambuliwa katika maeneo ya Kimara na Mbezi Luguruni pamoja na kuandaa Mpango wa Kina wa eneo la Mbezi Luguruni kuwa kitovu cha huduma *(Satelite urban centre)*. Ili kuhakikisha maeneo hayo yanaendelezwa kwa mpangilio, katika mwaka 2007/08 Wizara itaendelea kushirikiana na Halmashauri kutambua na kuandaa mipango shirikishi ya kuendeleza maeneo hayo ili kuzuia uendelezaji holela, kuwezesha upimaji wa maeneo hayo na kuweka huduma muhimu za kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maendeleo ya nyumba, kama inavyoeleweka nyumba ni moja ya mahitaji matatu muhimu ya mwanadamu ikiwa ni pamoja na chakula na mavazi. Nyumba bora huchangia katika kuwa na afya nzuri na hivyo kumwezesha mwananchi kujiendeleza kiuchumi. Vilevile shughuli za uendelezaji nyumba huleta ajira na hivyo huchangia katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuimarisha sekta ya nyumba, Wizara ilianza kuandaa Sera Mpya ya Maendeleo ya Nyumba katika mwaka 2006/07. Kazi hii itaendelea katika mwaka wa fedha 2007/08. Sera hii itakuwa ndiyo dira ya kuendeleza nyumba hapa nchini na itaandaliwa Sheria husika '*Housing Act'* ambayo itarahisisha utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeendelea na jukumu la kusimamia Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali. Lengo ni kuwakopesha watumishi ili waweze kukarabati, kujenga au kununua nyumba za kuishi na hivyo kujipatia makazi ya uhakika. Mfuko huu ni wa mzunguko (*Revolving Fund)* na marejesho yake huzingatia kipindi cha mtumishi kuwa katika ajira.

Katika mwaka wa fedha 2006/07 waombaji wapya 390 waliidhinishiwa mikopo yenye thamani ya Shilingi 1,646,277,979 na kufanya idadi ya watumishi walioidhinishiwa mikopo tangu mfuko huu uanzishwe kufikia 1,169 yenye thamani ya shilingi 4,484,457,515.85. Hadi kufikia mwezi Juni, 2007 marejesho halisi yalifikia shilingi 761,008,608.50. Katika mwaka wa fedha 2007/08, Wizara yangu itaendelea kuboresha kumbukumbu za wakopaji na kutumia mfuko huo kukopesha wafanyakazi ili waweze kupata makazi bora (Jedwali Na. 8).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi ni nyenzo mahususi katika kuhifadhi mazingira, kuwezesha uzalishaji endelevu katika ardhi na rasilimali zake, kuondoa migogoro ya ardhi, kunusuru wananchi katika majanga mbalimbali na kugawanya ardhi kisayansi kwa watumiaji mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2006/07, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi imeendelea kusimamia na kuratibu uandaaji na utekelezaji wa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi katika ngazi ya Vijiji, Wilaya na Taifa. Kufuatia kutangazwa kwa Mkakati wa Taifa wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji, Tume iliweza kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika Wilaya 13 na Vijiji 172.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/08 Tume kwa kushirikiana na Halmashauri na Wizara ya Maliasili na Utalii itaendelea kuandaa na kutekeleza mipango ya matumizi bora ya ardhi katika wilaya 6 za mpakani, wilaya 4 zenye hifadhi za wanyamapori na mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji 40. Aidha, Tume itaratibu mipango yote inayoandaliwa na wadau wengine na kuhakikisha inatekelezwa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wakala wa Taifa wa utafiti wa nyumba bora na vifaa vya ujenzi (*NHBRA*), Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi unalo jukumu la kutafiti, kukuza, kushauri, kuhamasisha na kusambaza matokeo ya utafiti na utaalamu wa ujenzi wa nyumba bora za gharama nafuu. Vilevile Wakala huelimisha na kuhamasisha wananchi kuanzisha vikundi vya ushirika vya uzalishaji na vya ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu kwa kutumia vifaa vilivyotafitiwa na Wakala katika ngazi zote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2006/07, Wakala uliendesha semina za uhamasishaji kwa viongozi, maafisa maendeleo ya jamii, madiwani, wahandisi na wananchi, katika wilaya za Tabora Vijijini na Mjini, Morogoro Vijijini na Mkoa wa Pwani, jumla ya washiriki 800 walihudhuria. Mafunzo kwa vitendo yamefanyika katika

Wilaya za Namtumbo, Kinondoni, Ilala, Temeke, Tabora Vijijini na Mjini, na Iringa Vijijini ambako vikundi vya ujenzi vilifundishwa mbinu za kufyatua matofali ya udongo saruji au ya mfinyanzi ya kuchoma pamoja na ujenzi kwa kutumia matofali yanayofungamana.

Shirika la Taifa la Nyumba kwa kushirikiana na Wakala linatumia teknolojia hiyo katika ujenzi wa maduka 76 huko Ipogolo – Iringa, pia Wakala wa Majengo ya Serikali wanatumia teknolojia hiyo kujenga nyumba za serikali katika baadhi ya mikoa nchini. Wananchi wameanza kuvutiwa na teknolojia hii, hivyo kuitumia katika ujenzi wa nyumba zao. Pia utafiti wa mashine za kufyatulia matofali yanayofungamana unaendelea kuboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili matokeo ya tafiti yaweze kuwafikia watumiaji, Wakala hutumia fursa mbalimbali kujitangaza. Katika mwaka 2006/07, Wakala ulijitangaza kwa kushiriki katika maonyesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma, Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam na Mkutano wa Kimataifa wa Hakimiliki uliofanyika nchini. Pia Wakala ulijitangaza kupitia vyombo mbalimbali vya habari, magazeti na vipeperushi. Katika mwaka wa fedha 2007/08, Wakala utaendelea kujitangaza kwa kutumia fursa mbalimbali zitakazojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2007/08, Wakala utaendelea na utafiti na utaimarisha maabara yake ya utafiti kwa kununua vifaa vipya ili kuingia katika ushindani na kwenda pamoja na kasi ya mabadiliko ya sayansi na teknolojia. Pia utaelimisha na kuhamasisha wananchi kuanzisha vikundi vya ushirika vya ujenzi wa nyumba bora za gharama nafuu na vya uzalishaji wa vifaa vya ujenzi vilivyotafitiwa. Yote hayo yatafanyika kwa njia za semina na mafunzo kwa vitendo. Aidha, Wakala utashiriki katika maonyesho mbalimbali ya Kitaifa na kimataifa. Napenda kurudia tena wito nilioutoa mwaka uliopita kwa Halmashauri zote nchini na Wananchi kuwasiliana na Wakala na kutumia teknolojia zake ili kuboresha makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Shirika la Nyumba la Taifa, Sheria ya Bunge Na. 2 ya mwaka 1990 iliyorekebishwa mnamo Juni, 2005, inalitaka Shirika la Nyumba la Taifa liendeshe majukumu yake kibiashara. Majukumu haya ni pamoja na kujenga nyumba kwa madhumuni ya kupangisha na kuuza, kusimamia miliki, kusimamia majengo kama wakala, kuendesha miradi ya ujenzi itakayoidhinishwa na Serikali na kufanya shughuli za ukandarasi wa majengo. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba za kupanga ndiyo rasilimali kubwa ya Shirika, kwani zaidi ya asilimia 88 ya mapato yake hutokana na kodi ya pango ya nyumba zake 16,021. Nyumba hizi zipo kwenye miji mbali mbali ya mikoa ya Tanzania Bara. Kiasi kingine cha mapato ya Shirika hutokana na ujenzi wa nyumba za kuuza na shughuli za ukandarasi. Aidha, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kutokana na marekebisho ya Sheria Na. 2 ya Shirika la Nyumba la Taifa yaliyofanywa na Bunge hili mwezi Juni 2005, yamewafanya wapangaji wengi kulipa kodi zao za pango kwa wakati kulingana na mikataba yao ya pango.

Katika kipindi cha mwaka 2005/06, Shirika liliweza kukusanya kiasi cha shilingi 19,227,302,242 ambacho ni makusanyo makubwa katika historia ya Shirika. Ongezeko hilo lilitokana na wapangaji wengi kulipa malimbikizo ya nyuma. Pia kiasi cha shilingi 17,065,716,170 kilikusanywa katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2006 hadi mwezi Mei, 2007.

Katika juhudi za kuimarisha ukusanyaji wa mapato, Shirika lilirekebisha kodi za pango kwa nyumba zake nchini kote kuanzia mwezi Machi, 2007. Kodi hiyo mpya itaongeza mapato kutoka shilingi 15,000,000,000 hadi 22,600,000,000 kwa mwaka. Nawashukuru na kuwapongeza wapangaji wote waliotimiza wajibu wao wa kulipa kodi zao za pango kwa wakati na pia nachukua fursa hii tena kuwataka wapangaji wenye malimbikizo kuyalipa mara moja ili kuliwezesha Shirika kutekeleza wajibu wake ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika zoezi la kuuza nyumba ndogo ndogo na za kati, jumla ya nyumba 4,838 kati ya 4988 ambazo ni sawa na asilimia 97 ya nyumba zilizokusudiwa kuuzwa zimelipiwa kikamilifu na kulipatia Shirika jumla ya Shilingi 7,383,936,065. Ni matarajio ya Shirika kuwa wapangaji wa nyumba 150 waliobaki watakamilisha kulipa madeni yao kulingana na mikataba ya mauziano.

Sanjari na hilo, Shirika liliendelea kupokea malipo kutoka kwa wanunuzi wa nyumba mpya 314 zilizojengwa kwa ajili ya kuuzwa. Hadi kufikia Juni 2007, kiasi cha shilingi 5,621,569,868 kilikusanywa ikilinganishwa na matarajio ya shilingi 8,818,961,114. Hata hivyo, kasi ya kulipia nyumba hizi bado ni ndogo. Natoa wito kwa wanunuzi wote waliopewa fursa hii kukamilisha malipo yao ifikapo mwezi Desemba, 2007. Baada ya muda huo kupita nyumba hizo zitauzwa kwa wananchi wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapato hayo yameliwezesha Shirika kushughulikia majukumu yake mbalimbali kama vile ujenzi wa nyumba za makazi, majengo makubwa ya biashara, gharama za uendeshaji, matengenezo ya nyumba na malipo ya kodi mbalimbali kwa mujibu wa Sheria. Katika mwaka wa fedha 2006/07, Shirika limekwishalipa Serikalini jumla ya shilingi 2,176,411,126 zikiwa kodi za mapato, ongezeko la thamani, majengo na viwanja. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita Shirika liliweza kulipa shilingi 8,180,399,028 kama kodi mbalimbali ambazo zimechangia katika kuwaletea wananchi maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufanikisha jukumu la usimamizi wa nyumba zilizopo, Shirika linatenga asilimia 25 ya mapato yatokanayo na kodi ya pango kila mwaka kwa ajili ya kugharamia matengenezo. Hatua hii imeliwezesha Shirika kuzifanyia matengenezo makubwa baadhi ya nyumba zilizokuwa katika hali mbaya na kupunguza kero kwa wapangaji. Katika mwaka wa fedha 2006/07 jumla ya nyumba 2,124 zilitengenezwa pamoja na majengo 412 kwa gharama ya Shilingi 4,664,968,030 (Jedwali Na. 9).

Aidha, ili kuwa na mpango wa matengenezo endelevu na wenye ufanisi, Shirika limeandaa programu ya miaka mitano (5) ya matengenezo kama sehemu ya Mpango

Mkakati wa Shirika (*Corporate Plan*). Katika mpango huo, Shirika limepanga kuyafanyia matengenezo makubwa majengo yapatayo 478 kila mwaka ili ndani ya kipindi cha miaka mitano ijayo majengo yote yawe yamefanyiwa matengenezo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika limeendelea kujenga majengo makubwa ya vitega uchumi kwa kutumia mtaji wake na kwa kushirikiana na sekta binafsi. Katika mwaka 2006/07 Shirika lilikamilisha jengo 1 la ghorofa Kigoma, majengo 2 yenye maduka 15 Arusha na maghorofa 2 ya makazi yenye nyumba 24 Dodoma kwa kutumia mtaji wake.

Shirika limekamilisha majengo 3 makubwa na linaendelea na ujenzi wa majengo mengine 16 kwa njia ya ubia. Katika mwaka 2007/08 Shirika linatarajia kujenga majengo makubwa 29 ya makazi na biashara na maduka 87 katika Jiji la Dar es Salaam na Arusha na miji ya Kigoma, Iringa, Shinyanga na Tabora kwa kutumia mtaji wake na kwa kushirikiana na wabia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2006/07, Shirika lilikamilisha ujenzi wa nyumba 64 za kuuza na kupangisha zilizojengwa katika Mikoa ya Dar es Salaam maeneo ya Boko, Mbezi *Beach* na Mbweni JKT na Arusha maeneo ya Kijenge na Mwandamo.

Katika mwaka wa fedha 2007/08, Shirika linatarajia kujenga nyumba 222 kwa ajili ya kuuza na kupangisha katika Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Pwani, Lindi na Kagera. Pamoja na hili, Shirika litafanya upembuzi yakinifu wa kujenga nyumba katika miji midogo ya Mikoa na Wilaya. Nia na madhumuni ya kufanya upembuzi huu, ni kutaka kubaini mahitaji na aina ya nyumba zinazohitajika katika miji hiyo. Utekelezaji wa jukumu hili unalenga kulipatia Shirika sura ya kitaifa. Shughuli hizi zinalenga katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Ibara 68(g).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Shirika linakabiliwa na matatizo mbalimbali yakiwa ni pamoja na:- mtaji mdogo kwa ajili ya ujenzi, ukosefu wa soko la uhakika la nyumba zinazojengwa kutokana na kukosekana kwa mfumo rasmi wa kutoa mikopo ya ujenzi na ununuzi wa nyumba na kesi zilizoko mahakamani zinazohusu wapangaji wanaopinga uendelezaji wa viwanja vyenye majengo chakavu au yaliyopitwa na wakati katikati ya miji zinazochukua muda mrefu bila kumalizika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika limejiwekea mikakati ya kutatua matatizo hayo, ili kuongeza ufanisi kama ifuatavyo: kuendelea na usimamizi wa rasilimali za nyumba zilizopo ambapo msukumo zaidi utawekwa katika matengenezo makubwa na ya kina ya nyumba na majengo; kupanua wigo wa ujenzi wa nyumba za makazi kwa ajili ya kuuza na kupangisha; kuendelea na mkakati wa uendelezaji upya wa viwanja vilivyoko katikati ya miji kupitia Sera ya ubia iliyobuniwa na Shirika; kuendelea kuiomba mahakama ione umuhimu wa uendelezaji wa viwanja vyenye majengo chakavu au yaliyokusudiwa kuendelezwa ili itoe maamuzi ya kesi mapema; kuendelea kuhimiza ushirikiano baina ya Serikali, shirika na vyombo vya fedha kwa ajili ya uanzishaji wa

mfumo rasmi wa kutoa mikopo ya ununuzi na ujenzi wa nyumba kwa raia na taasisi mbalimbali. Natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kutoa msukumo katika uanzishaji wa mfumo wa kutoa mikopo kwenye sekta ya nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huduma za utawala na rasilimali watu, Wizara yangu imeendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa ufanisi wa hali ya juu. Dhamira hii inathibitishwa na jitihada mbalimbali zilizofanywa na zinazoendelea za kuboresha mifumo ya utendaji kazi na usimamizi wa Rasilimali watu. Wizara yangu imeendelea kutoa mafunzo, kuboresha mazingira ya ofisi, kutoa stahili kwa watumishi zinazoendana na ajira zao pamoja na kudumisha Utawala Bora.

Aidha, msisitizo umelenga katika kutumia dhana shirikishi ya kupanga, kujenga uwezo, kutekeleza, kusimamia na kutathmini utekelezaji ili kuboresha utendaji kazi na kudhibiti nidhamu. Pia Wizara yangu imeendelea kupiga vita rushwa, kutoa huduma kwa waathirika waliopo na kuongeza kasi ya mapambano dhidi ya maambukizi ya UKIMWI mahali pa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2006/07, Wizara yangu imeboresha utendaji kazi kwa kununua vitendea kazi, ikiwa ni pamoja na kompyuta, samani za ofisi na magari kwa ajili ya kutoa huduma kwa ufanisi. Wizara imeajiri watumishi wapya 93, kati yao 69 ni ajira mpya na 24 ni ajira mbadala, watumishi 109 wamepandishwa vyeo na watumishi 8 wamechukuliwa hatua za kinidhamu (Jedwali Na. 10). Katika mwaka wa fedha 2007/08, Wizara yangu itaendelea kuboresha mazingira ya kazi, kutoa stahili mbalimbali za watumishi pamoja na kuajiri watumishi wengine 246 wa fani tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2006/07, Wizara yangu ilikamilisha hatua ya pili ya ukarabati wa jengo la Ardhi. Licha ya ukarabati huu kuleta mandhari nzuri ya jengo, utaboresha mpangilio wa ukaaji wa wazi unaosaidia kuleta ufanisi zaidi katika utendaji pamoja na kusaidia kuzuia mianya ya rushwa. Ukarabati wa jengo la Menejimenti ya Mifumo ya Habari (*Management Information System*) umekamilika. Aidha, michoro ya ubunifu na usanifu wa jengo la Upimaji na Ramani imekamililka katika mwaka wa fedha 2006/07. Wizara itakamilisha maandalizi kwa kuandaa makadirio ya gharama za ujenzi, nyaraka za zabuni na mikataba ya ujenzi katika mwaka wa fedha 2007/08.

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi wa Sekta ya Ardhi wameendelea kupelekwa kwenye mafunzo ya aina mbalimbali. Katika mwaka 2006/07 jumla ya Watumishi 272 wa Wizara na Halmashauri walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi. Kati ya hao watumishi 57 walikuwa wanawake (Jedwali Na. 11 (a) na 11 (b)). Katika mwaka wa fedha 2007/08, Wizara yangu inatarajia kuwapatia mafunzo jumla ya watumishi 50 kati yao 5 ni kutoka katika Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha na kudumisha utendaji kazi, Wizara yangu imeendelea kutoa mafunzo juu ya utoaji wa huduma bora kwa mteja (*customer care service*) kwa waajiriwa wapya na watumishi wa vituo vya nje. Mafunzo haya

yamesaidia kuwafanya watumishi kuelewa wajibu wao na matarajio ya wateja ya kupatiwa huduma bora. Aidha, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Wizara yangu imeboresha utaratibu uliokuwepo wa kushughulikia malalamiko ya wananchi. Katika mwaka 2007/08, Wizara yangu itaendelea kutoa mafunzo ya utoaji wa huduma bora kwa mteja kwa waajiriwa wapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, maadhimisho ya wiki ya Utumishi wa Umma huadhimishwa kila mwaka katika wiki ya tatu ya mwezi Juni, ambapo mwaka huu iliadhimishwa tarehe 17/6/2007 hadi 23/6/2007. Katika maadhimisho hayo Wizara na Taasisi za Serikali hushiriki maonyesho kwa lengo la kuuelimisha umma juu ya huduma zitolewazo na Wizara/Taasisi hizo.

Mwaka huu jumla ya Wizara na Taasisi 77 zimeshiriki maonyesho hayo na kauli mbiu ilikuwa ni zingatia Maadili, Pambana na Rushwa ili kuimarisha Utawala Bora. Nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa kati ya Washiriki hao 77, Wizara yangu imepata ushindi wa pili, ambapo kwa upande wa Wizara zote zilizoshiriki imekuwa mshindi wa kwanza. Ushindi huu wa Wizara yetu ni changamoto kubwa kwetu na umetokana na michango na ushauri mkubwa tunaoupata kutoka kwa Waheshimiwa wabunge na wananchi kwa ujumla. Ninawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupambana na janga la UKIMWI katika sehemu ya kazi, Wizara yangu imeendelea kuhamasisha watumishi ili waweze kupima afya zao kwa kuwaleta wataalamu wa Huduma ya Ushauri Nasaha na Kupima kwa Hiari mahali pa kazi kila baada ya miezi mitatu.

Vilevile, katika uhamasishaji huo watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI walisaidia kuhamasisha kwa kutoa uzoefu wa kuishi kwa matumaini. Kutokana na hamasa hiyo, jumla ya watumishi 219 wamepima kwa hiari. Zoezi hili limeongeza hamasa ya watumishi kupima afya zao. Wizara imekuwa ikiwapatia watumishi walioathirika huduma za dawa na lishe. Katika mwaka wa fedha 2007/08 Wizara yangu itaendelea kuhamasisha upimaji wa afya na kutoa huduma kwa waathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeanzisha Kitengo cha Elimu, Habari na Mawasiliano ambacho kina jukumu la kutoa taarifa zinazoihusu Wizara kwa wananchi. Katika mwaka wa fedha 2006/07, Kitengo hiki kiliratibu vipindi vya Elimu, Habari na Mawasiliano ndani na nje ya Wizara. Utaratibu huu umesaidia kuelimisha umma juu ya huduma mbalimbali zinazotolewa. Katika mwaka wa fedha 2007/08, Wizara yangu itaendelea kuboresha mawasiliano, kutoa elimu na habari kwa wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ina vyuo viwili vya Ardhi vya Tabora na Morogoro ambavyo vinatoa mafunzo ya Astashahada *(Ordinary Diploma)* katika fani za Urasimu Ramani na Upimaji Ardhi, na Cheti katika fani za Umiliki Ardhi na Uthamini na Uchapaji Ramani. Fani hizi ni muhimu kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya soko la wataalamu wa ardhi nchini. Katika mwaka wa fedha 2006/07 idadi ya wahitimu ilikuwa

124 kati yao 44 walitoka Chuo cha Ardhi Morogoro na 80 walitoka Chuo cha Ardhi Tabora (Jedwali Na. 12).

Katika Mwaka wa Fedha 2007/08, vyuo hivyo vitaandaa programu ya mafunzo ya muda mfupi ili wataalamu wa Sekta ya ardhi waliopo katika Halmashauri waweze kupatiwa mafunzo. Mafunzo hayo yatatolewa kwa maombi maalumu. Natoa wito kwa Halmashauri kutumia fursa hii kuwapeleka wataalamu wao kujifunza ili waende sanjari na mabadiliko ya teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rita Louise Mlaki, Mbunge, Naibu Waziri, Bibi Salome T. Sijaona, Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara na Taasisi na Wafanyakazi wote wa Wizara yangu kwa juhudi na mshikamano wao katika kufanikisha malengo ya Wizara na Taifa kwa ujumla. Itakuwa ni ukosefu wa fadhila kama sitaishukuru Kamati ya Kilimo na Ardhi kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kushauri na kutoa maoni ya kuboresha Sekta ya Ardhi.

Pia natoa shukrani kwa Benki ya Dunia, Kamisheni ya Umoja wa Ulaya, *Denmark,* Uingereza, *Sweden* na Uholanzi kupitia Mradi wa *"Business Environment Strengthening for Tanzania*" (*BEST*) na Mkakati wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA), ambazo zimeisaidia Wizara katika kutekeleza Mkakati wa Utekelezaji wa Sheria za Ardhi, natoa shukurani kwa *UN-Habitat* kwa kuendelea kushirikiana na Sekta ya Ardhi na Makazi katika kuboresha makazi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nazishukuru Asasi zisizo za Kiserikali zilizoshirikiana na Wizara katika kutoa elimu ya Sheria za Ardhi na Mipango Shirikishi ya Matumizi ya Ardhi Vijijini. Msaada wao tunauheshimu na kuuenzi na nawaomba wadau wengine zaidi kujitokeza kusaidia jitihada za Serikali kuboresha huduma za ardhi na makazi kwa wananchi. Mwisho kabisa napenda kuwashukuru wapiga kura wangu wa jimbo la Biharamuro Mashariki katika Wilaya mpya ya Chato kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kuutoa kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuhitimisha, Sera na Sheria zilizopo zinawalinda kikamilifu wananchi wetu, lakini tatizo kubwa lililopo kwa sasa ni baadhi ya Wananchi, Mamlaka na Taasisi mbalimbali kutozingatia matakwa ya Sheria katika suala zima la utwaaji ardhi pindi ardhi hiyo inapohitajika kwa shughuli za maendeleo.

Sera ya Ardhi ya Mwaka 1995 inatamka wazi kuwa kila kipande cha ardhi kina thamani na kwamba kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya Mwaka 1999 kifungu cha 3 (g), Sheria ya Ardhi Na.4 ya Mwaka 1999, kifungu cha 3 (g) na Sheria ya Utwaaji ardhi Na. 47 ya Mwaka 1967 zinatambua kwamba ardhi yote inayotwaliwa kwa mtu yeyote kwa ajili ya matumizi yoyote ni lazima mhusika wa ardhi hiyo alipwe fidia. Kutofuatwa kwa Sheria hizi kunawaletea usumbufu mkubwa wananchi katika kudai haki zao. Ni vizuri Mamlaka zote zinazohusika na usimamizi wa ardhi nchini kuwa mstari wa mbele kuwaelimisha wananchi juu ya haki ya ardhi wanayoimiliki. Natoa rai kwa Mamlaka na Taasisi mbalimbali zinazotwaa ardhi za wananchi hao kuheshimu Sheria,

Kanuni na Taratibu za utwaaji ardhi ili wananchi walipwe fidia kwa mujibu wa Sheria hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua kuwa ardhi ni mali, ni ukweli usiofichika kwamba Watanzania hatuwezi kushinda vita dhidi ya umaskini kwa silaha ambayo hatuna. Silaha ya uhakika aliyonayo kila Mtanzania ni ardhi. Kwa kutumia ardhi kama ardhi, na ardhi kama mtaji, tunaweza kuushinda umaskini tulionao.

Hivyo basi, njia pekee ya kuhakikisha ardhi inamwondolea mwananchi umaskini. Ni kwa Serikali kupima kila kipande cha ardhi yetu na kummilikisha mwananchi kwa kumpa hatimiliki iwe ya kimila au ya Serikali ili aweze kuitumia kama dhamana ya kupata mikopo kutoka kwenye Taasisi za fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bajeti ya mwaka wa fedha 2007/2008, katika mwaka wa fedha 2006/07 Wizara yangu ilitengewa shilingi 18,274,683,000 na katika mwaka wa fedha 2007/08 Wizara inaomba Bunge lako tukufu likubali kupitisha makadirio ya matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ya jumla ya Shilingi 14,691,991,000 kama ifuatavyo:- (i) Shilingi 11,091,832,000 kama Makusanyo ya Mapato ya Serikali; (ii) Shilingi 3,909,653,000 kwa ajili ya mishahara ya Watumishi; (iii)Shilingi 8,806,338,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo; na (iv) Shilingi 1,976,000,000 kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo jumla ya fedha yote ninayoomba ambayo inajumuisha Mishahara, Matumizi Mengineyo na Matumizi ya Miradi ya Maendeleo ni Shilingi bilioni 14,691,991,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana wewe, na pia waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI)**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilito na Ardhi, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo na Ardhi kuhusu utekelezaji wa malengo ya bajeti kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2006/2007, pamoja na ushauri wa Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 81(1), Toleo la 2004 na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kuhusu utekelezaji wa malengo ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka uliopita 2006/2007 pamoja na maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kufika hapa salama na kwamba tuko wazima. Napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo, Mbunge, Mwenyekiti wa Kamati, kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwa niaba yake na Wajumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikumshukuru mke wangu kwa kuniunga mkono na kunivumilia wakati wote. Vilevile napenda kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Matemwe na ninawaambia *Aluta continua! (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia natumia fursa hii kwa niaba ya Kamati kutoa pole kwa wazazi, ndugu na jamaa wote wa aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalumu, Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia. Aidha, Kamati inatoa pole kwa Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Mbunge, kwa kufiwa na mama yake. Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, Amin!

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupitia utekelezaji wa Bajeti ya mwaka uliopita, Kamati iliridhika na hatua zilizochukuliwa na Serikali katika utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati ilioutoa wakati ilipochambua Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2006/2007. Aidha, Kamati ilitoa ushauri ili kuboresha na kuongeza kasi katika utoaji wa huduma za Ardhi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafanikio, Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi ilikutana Dar es Salaam tarehe 29 Mei, 2007 ili kupitia utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2006/2007. Katika utekelezaji wa Bajeti hiyo, yamekuwepo mafanikio mbalimbali. Baadhi ya mafanikio hayo ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Kutayarisha miswada ya Sheria tatu za matumizi ya Ardhi, mipangomiji na usajili wa wataalamu wa mipangomiji. Miswada hiyo ilipitishwa na Bunge hili tukufu mwezi Aprili , 2007, na sasa ni Sheria kamili.

(ii) Kupima mipaka ya vijiji 2,668 katika mikoa ya Kigoma, Kagera, Iringa, Lindi, Mbeya, Pwani, Rukwa, Shinyanga na Tanga.

(iii) Kusimamia na kuratibu upimaji wa viwanja katika miji ya Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya na Morogoro. Zaidi ya viwanja 49,000 vimekwishapimwa katika miji hiyo.

(iv) Kuendelea na utekelezaji wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka 1999 kwa kutoa vyeti vya vijiji 211 na Hatimiliki za kimila 3,940 kwa wanavijiji.

(v) Kutambua miliki kwenye maeneo yaliyojengwa kiholela na kutoa leseni za makazi. Jumla ya miliki 230,000 zimetambuliwa na leseni za makazi 75,000 zimetolewa.

(vi) Kutayarisha mipango ya matumizi ya Ardhi katika ngazi ya Taifa, Wilaya na Vijiji. Jumla ya Wilaya 13 na Vijiji 172 vimehusishwa.

(vii) Kushughulikia mashauri ya Ardhi na Nyumba na kuyafanyia uamuzi katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Iringa, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Mbeya, Lindi, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Pwani, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga, Singida, Tabora na Tanga.

(viii) Kuboresha na kuongeza juhudi za kukusanya kodi ya pango la nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa na kufikia kiwango cha shilingi bilioni 19.8.
(ix) Kuendelea na ujenzi wa nyumba za kuuza au kupangisha katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Dodoma na Kigoma.

(x) Kukamilisha ujenzi wa tovuti ya Wizara na mtandao wa mawasiliano ya Wizara kwa kuunganisha makao makuu ya Wizara na Ofisi za kanda za usajili wa Hati katika miji ya Mwanza, Mbeya, Dodoma, Moshi pamoja na Ofisi za Ardhi katika manispaa za Kinondoni, Ilala na Temeke.

(xi) Kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu sera na Sheria za Ardhi zilizopo kwa njia ya mafunzo, vipindi vya Redio na Televisheni, magazeti, na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio hayo yamekuwepo matatizo na changamoto kadhaa katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2006/2007. Baadhi ya changamoto hizo ni kama zifuatazo:-

(i) Ukosefu wa vitendea kazi kama kompyuta, magari na vifaa vya upimaji katika Halmashauri za Wilaya na Miji. Aidha, kuna ukosefu wa fedha za kutosha kugharamia majukumu yote ya Wizara katika kutenda kazi zake kwa ufanisi.

(ii) Migogoro baina ya vijiji huchelewesha upimaji wa mipaka vijijini na kuathiri zoezi la kuwamilikisha wananchi ardhi vijijini.

(iii) Uhaba wa fedha kwa ajili ya uendeshaji wa mabaraza unaosababisha mlundikano wa kesi kwa kukosa fedha za kulipia posho za Wajumbe na mahitaji ya kiofisi.

(iv) Ukosefu wa takwimu za miliki za viwanja na ukosefu wa wataalamu wa kutosha katika sekta ya Ardhi unapunguza kasi ya utekelezaji kuwafikia walengwa na unakwamisha upatikanaji wa mapato ya kutosha.

(v) Ukosefu wa ndege ya kupigia picha za anga na kung'olewa kwa alama za mipaka ni matatizo ya muda mrefu yanayokwamisha taratibu za kudhibiti mipaka ya Kimataifa na upimaji wa viwanja katika maeneo mbalimbali.

(vi) Ujenzi wa makazi kiholela katika maeneo ya mabondeni ambao unahatarisha maisha na mali za watu waishio maeneo hayo ni kikwazo katika mpango wa kurasimisha rasilimali (ardhi na nyumba) mijini.

(vii) Kuwepo kwa mawingu angani kwa kipindi kirefu kumezuia upatikanaji wa *satellite image* kwa eneo la Bagamoyo na Rufiji. Maeneo haya ndiyo yaliyolengwa kufanyia kazi kwa mwaka huu wa fedha uliopita, kazi hiyo haikufanyika.

(viii) Ukosefu wa mfumo rasmi wa kutoa mikopo ya ujenzi na ununuzi wa nyumba hupunguza kasi ya kuendeleza sekta ya Nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Wizara imepanga kufanya kazi mbalimbali zenye lengo la kuhakikisha kwamba rasilimali za ardhi zinaendelezwa, zinahakikiwa na kutumika ipasavyo kwa matumizi endelevu kwa wadau wote. Baadhi ya kazi hizo ni kama zifuatazo:-

(i) Kukusanya mapato ya jumla ya Shilingi 11,091,832,000/= kutokana na ada/kodi mbalimbali zitokanazo na huduma za ardhi. Aidha, Wizara itaendeleza juhudi za ukusanyaji wa madeni ya kodi za viwanja ili kuongeza mapato na kutumika katika maeneo mengine ya Wizara katika kufanikisha shughuli zake.

(ii) Kuendelea na upimaji wa mipaka ya ardhi katika maeneo yenye migogoro ndani ya nchi na ile ya mipaka kati ya nchi yetu ya Tanzania na nchi jirani. Pia Wizara itaendelea na zoezi la upimaji wa mipaka ya Vijiji, katika mikoa mbalimbali.

(iii) Kuendelea kushirikiana na mamlaka za Halmashauri za Wilaya kugawa ardhi kati ya wakulima na wafugaji ili kuepusha migogoro ya mara kwa mara inayozuka baina yao.

(iv) Kuendelea na zoezi la kupima viwanja katika miji mbalimbali kwa kushirikiana na Halmashauri husika.

(v) Kuendelea na zoezi la kuhuisha ramani, kutayarisha ramani na kupiga picha za anga za Miji na Wilaya kadhaa.

(vi) Kuendelea na mipango ya kudhibiti alama za mipaka ya Kimataifa, na kudhibiti Mto Songwe ambao ni mpaka kati ya Tanzania na Malawi.

(vii) Kuendelea na kuanzisha na kuimarisha Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya katika Mikoa mbalimbali.

(viii) Kuendelea na ujenzi wa nyumba za kuuza na kupangisha katika miji yenye soko la uhakika.

(ix) Kuendelea na mipango ya elimu kwa umma kuhusu Sera na Sheria za Ardhi zilizopo.

(x) Kuendelea kuandaa na kukamilisha kanuni na kuanza utekelezaji wa Sheria mpya za matumizi ya Ardhi na mipangomiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza kwa ufupi utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka uliopita (2006/2007), naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2007/2008 kama ifuatavyo:-

(i) Kutokana na majukumu ya kudhibiti mipaka ya Kimataifa, Mikoa, Wilaya na Vijiji, upo umuhimu wa kuiwezesha Wizara hii kupitia Bajeti ili iweze kutekeleza majukumu yake na kuepusha migogoro itakayohatarisha amani na utulivu nchini.

(ii) Kutokana na ufinyu wa Bajeti, Wizara iendelee kubuni mbinu mbalimbali za kuongeza mapato inayoyasimamia, ikiwa ni pamoja na kuwatambua na kuwafikia wote waliomilikishwa viwanja na mashamba kwa mujibu wa Sheria ili walipe kodi na ada zinazowahusu.

(iii) Wizara kwa kushirikiana na mamlaka za Serikali za Mitaa, iendelee na zoezi la kupima mipaka ya vijiji na hatimaye kupima maeneo ndani ya vijiji ili wananchi waweze kumilikishwa maeneo yao na kupata hatimiliki za kimila.

Hii ni njia mojawapo ya kuwawezesha wananchi maana hatimiliki za kimila zitatumika kama dhamana ya kupata mitaji kwenye vyombo vya fedha. Serikali ivihimize vyombo vya fedha kushiriki kwa ukamilifu katika zoezi hili kuwaondolea wananchi umaskini.

(iv) Kuendelea na zoezi la kupima viwanja katika miji mbalimbali kwa kutumia mfuko wa kupima viwanja, kwa kushirikiana na mamlaka za Serikali za mitaa. Kamati inaishauri Serikali kutathimini na kuhuisha viwango vya kodi na ada ili kuweka uwiano mzuri na kuwawezesha wananchi kumudu kulipa kodi na ada mbalimbali zinazowekwa.

(v) Kuendelea kushughulikia tatizo la upungufu wa wataalamu katika sekta ya Ardhi. Wizara ishirikiane na mamlaka za Serikali za mitaa kuwafundisha na kuwasambaza wataalamu hususan katika ngazi za Halmashauri. Upatikanaji wa wataalamu uendane pamoja na vitendea kazi katika ngazi zote.

(vi) Ili Mabaraza ya Ardhi na Nyumba yaweze kufanya kazi zake vizuri, ni muhimu kwa Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na yale ya Kata kuwepo na kuimarishwa. Kwa hiyo, wakati Wizara inaimarisha Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, isimamie kwa kasi zaidi uanzishwaji na uimarishwaji wa Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Kata katika Mikoa yote.

(vii) Kuendelea na zoezi la kuelimisha Umma kuhusu Sera na Sheria katika sekta ya Ardhi. Aidha, Wizara iendelee kwa kasi zaidi kukamilisha kanuni kwa sheria mpya zilizopitishwa mwaka huu na kuanza zoezi la kuzitafsiri sheria hizo katika lugha ya Kiswahili ili ziweze kueleweka kwa wananchi walio wengi.

(viii) Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuboresha ushirikiano kati ya Wizara ya Ardhi na Ofisi ya Waziri Mkuu ,Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ili kuwa na

mfumo mzuri wa kutekeleza majukumu katika Sekta ya Ardhi ya upangaji wa miji nchini. Kamati inashauri pia Serikali iongeze juhudi zaidi kuratibu zoezi zima la ugawaji wa viwanja ili kuondoa migogoro inayojitokeza baina ya Halmashauri za Wilaya na Wizara.

(ix) Kutokana na ujenzi holela wa nyumba katika sehemu za mabondeni na sehemu zilizotengwa kwa ajili ya kuendelezwa siku za usoni hasa katika jiji la Dar es Salaam, Kamati inaishauri Serikali kutilia mkazo swala la kuwahamisha Wananchi hao kuepuka kuhatarisha maisha yao. Aidha, tunaipongeza Serikali kwa utaratibu wake wa utambuzi wa makazi yaliyojengwa kiholela ambapo itasaidia kurasimisha mali kwa wahusika na kukuza pato la Taifa kwa kukusanya kodi ya ardhi katika maeneo hayo.

(x) Serikali iharakishe uanzishaji wa mfumo rasmi wa kutoa mikopo ya ujenzi na ununuzi wa nyumba (*mortgage facility*). Mfumo huu utaliwezesha Shirika la Nyumba la Taifa na wananchi kwa jumla kupata mtaji kuendeleza shughuli za ujenzi au ununuzi wa nyumba nchini.

(xi) Kamati inaishauri Wizara kufuta hatimiliki viwanja vya watu ambao hawaviendelezi na pia kuongeza kasi katika utekelezaji wa shughuli nzima bila kuathiri mchakato wa Wananchi kujiletea maendeleo yao.

(xii) Kutokana na unyeti wa tatizo la kuhamahama kwa Mto Songwe ambao ni mpaka wa Kimataifa kati ya Tanzania na Malawi, Serikali iongeze juhudi za kutafuta fedha ili kutekeleza mradi wa kudhibiti Mto Songwe mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kuzungumzia Maombi ya Fedha ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 kama ifuatavyo: Kiasi cha fedha kinachoombwa katika fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ni Shilingi 14,691,991,000/=. Kati ya fedha hizo, shilingi 12,715,991,000/= ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi 1,976,000,000/= ni fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika,kiasi cha fedha zilizotengwa ni kidogo sana ukilinganisha na majukumu ya Wizara. Hivyo Kamati iniashauri tena Serikali kuitengea sekta hii fedha za kutosha za maendeleo na za ndani katika mwaka ujao wa fedha ili iweze kutekeleza majukumu mazito iliyonayo katika kusimamia matumizi ya rasilimali ardhi.

Pamoja na angalizo hilo, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano wao wakati walipochambua na kupitia Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:-Mheshimiwa Gideon A. Cheyo, Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Idd M. Azzan, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Castor R. Ligalama.

Mheshimiwa Joyce N. Machimu, Mheshimiwa Fred T. Mpendazoe, Mheshimiwa Dkt Samson Mpanda, Mheshimiwa Manju S. Msambya, Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Shally J. Raymond, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa Martha J. Umbulla, Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe na Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir.

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa JohnP. Magufuli na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Ritta Mlaki, kwa ushirikiano mkubwa walioipatia Kamati.

Aidha, nampongeza Katibu Mkuu wa Wizara hii, Ndugu Salome Sijaona, pamoja na wataalamu wote wa Wizara hii kwa jinsi walivyofafanua hoja mbalimbali zilizotolewa na Wajumbe wa Kamati wakati wa kuchambua Bajeti hii.

Mwisho, napenda kukushukuru, kwa kunipa nafasi hii, na namshukuru Katibu wa Bunge, Bwana Damian S.L. Foka, kwa ushirikiano wake mzuri anaoutoa kwa Kamati, na Katibu wa Kamati hii, Ndugu Frank K. Mbumi, kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo napenda kutamka kwamba naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. *(Makofi).*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana mwakilishi wa Mwenyekitiwa Kamati ya Ardhi, na Maendeleo ya Nyumba. Sasa nitamwita Msemaji kutoka Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hii, Mheshimiwa Waziri Kivuli, John M. Cheyo, karibu sana.

**MHE. JOHN M. CHEYO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 45(3)(b)(c) na 81(1), Toleo la Mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwa nafasi ya kipekee kabisa naendelea kukishukuru chama cha *United Democratic Party (UDP)* na wananchi wa Jimbo la Bariadi Mashariki kwa kunikubali kuwa mtumishi wao na mwakilishi wao na kunipa nguvu kwa kuniunga mkono ninapotetea hoja zao za pamba, ardhi, michango lukuki, fidia ya mashamba na kadhalika. Nawashukuru madiwani wote wa Bariadi wanavyonisadia kuwatumikia wananchi wa Bariadi kwa wakati wote nikiwa Bungeni,

wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri Mheshimiwa Mathusela Matondo, Diwani *(UDP*).

Namshukuru sana Katibu wangu wa Mbunge Bariadi Mashariki, Mheshimiwa Diwani Njile Kingi Idebe, kwa kazi nzuri anayofanya kunisaidia kutumikia wana-Bariadi wote.

Aidha, namshukuru Mke wangu mpenzi Elizaberth, watoto wetu wote na familia, kwa kuwa msingi imara kwa kazi yangu ya Kibunge. Nawaahidi nitaendelea kuwatumikia wana-Bariadi na watanzania wote kwa umahiri, uadilifu na umakini mkubwa na Mungu awe nasi daima.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa John M. Cheyo , naomba nikuingilie kidogo samahani sana! Naomba baada ya Mheshimwia John M. Cheyo kumaliza kusoma, wafuatao wasije wakaondoka hapa, wawepo: Mheshimiwa Felix Christopher Mrema, Mheshimiwa Athumani Said Janguo, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu, Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje na Mheshimiwa Ponsiano Damiano Nyami, kwa asubuhi hii nadhani wanatosha.

Mheshimiwa John M. Cheyo, samahani sana kwa sababu niliona wengine wataondoka wakiwa hawajui, nisamehe sana!

**MHE. JOHN M. CHEYO -MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwa Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani chini ya uongozi wa Mheshimiwa Hamad Rashid na Dr.. Wilbrod Slaa, kwa ushirikiano mzuri wanaonipa ndani na nje ya Bunge.

Nachukua nafasi hii kumpongeza, Mheshimiwa John Pombe Magufuli, (Mb.), kwa hotuba yake nzuri na kwa kazi nzuri anayofanya katika Wizara yake akisadiwa na Naibu Waziri Mahiri, Mheshimiwa Rita Louise Mlaki , (Mb) na wafanyakazi wote wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu, *Mrs.* Salome T. Sijaona.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa uteuzi wa kutukuka wa Jaji Mkuu wa Tanzania, Jaji Augustino Ramadhani anayestahili kabisa kazi hiyo na namtakia mafanikio makubwa katika kulitumikia Taifa kwa nafasi hii muhimu na nyeti ya kulinda na kutoa haki.

Mwisho, lakini siyo kwa umuhimu , nampongeza Mheshimiwa Spika na wewe Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti, Katibu wa Bunge na Wafanyakazi wote kwa umahiri na kazi nzuri mnayoifanya kuongoza na kulitumikia Bunge letu.

Sisi tunaopata nafasi ya kusafiri tunajivunia kuwa Wabunge wa Bunge la Tanzania lenye utulivu, umahiri na undugu pamoja na kuwa na ushindani mkali wa kisiasa na kisera.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ninalotaka kuzungumzia ni Sera Mbadala ya Ardhi.

Naomba kuanza kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kwa kusema kwamba Mimi na Mheshimiwa Waziri kama wasukuma, tunakubaliana na dhana moja kwamba ardhi ni mali.

Sisi wasukuma tunasema " *Igembe sabo* " yaani jembe ni mali na kwa kuwa jembe ni la kulimia ardhi basi ardhi unayolima ndiyo mali yenyewe na ni silaha kabisa kama ulivyosema ya kuondoa umasikini au MKUKUTA.

Watanzania wengi tunaamini ardhi ndiyo mali tuliyopewa na Mwenyezi Mungu kama mtaji.

Kwa kuwa tunatoka vyama tofauti tunatofautiana kwa mtazamo wa kumiliki hii mali ardhi. Mtazamo wa Kambi ya upinzani ni kwamba ardhi ni mali ya mwenye ardhi.

Maana yake mtu mmoja mmoja na mtu huyu anaipata hiyo ardhi kwa kununua, kurithi au kupewa. Mtazamo wa CCM ardhi ni mali kwa matumizi ya kuiendeleza na usipoiendeleza unanyang'anywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtazamo huu una matatizo yafuatayo: (i) Dhana hii ya CCM haina misingi ya mila za makabila ya nchi hii kwani historia inayofahamika ni mji wa mtu au shamba la mtu au kabla watu hatujawa wengi kijiji kilijulikana kama Ngwaswale, Ngwalushu, Ngwamomose, Kwa Lema, Masawe, Kwa Mohamad au kwa Sheikh Rashid na kadhalika; (ii) Dhana hii inasisitiza umiliki wa kikomo, (*non-permanent ownership*) na umilki wa masharti (*conditional ownership*); (iii) Umiliki wa kikomo ( *Term Tenure*).

Kwa mfano, miaka 33 kijijini na miaka mpaka 99 mijini na masharti mfano sharti la kuendeleza katika miaka miwili ni dhana ya kigeni ( *Foreign concept* ) na inapunguza haki na uwezo wa mtu kwenye mali yake ardhi. Kwa mfano, familia vijjini zinazopewa miaka 33 hati ya kumiliki kimila hazitakuwa na ardhi baada ya miaka hiyo isipokuwa kwa hisani ya kijiji na kwa hiyo dhana hii inajenga tabaka la wananchi wasio na ardhi (*landless*).

· Aidha, watu wote waliopewa hatimiliki miaka kati ya 1961/1974 mijini sasa hivi hawana haki ya viwanja hivyo isipokuwa kwa hisani ya Waziri, na leo Waziri amesema yuko tayari kuongeza miaka 99. Viwanja hivi kama viko Magomeni, Kijitonyama, Mwananyamala, Temeke na miji mingine kama vile Mwanza, Mbeya, Tabora, Tanga, na kwingineko, Kambi ya Upinzani inawatahadharisha wananchi wote kuangalia hati zao za miaka hiyo na kufuatilia Wizarani hatima ya makazi yao. Ninawashauri wa wachangamkie ofa ya Waziri leo ili waweze wakaongezewa miaka 99. (*Makofi*)

Umiliki wa Kikomo na wenye masharti unapunguza thamani ya ardhi. Mfano, ardhi yenye madini ina thamani zaidi ya ardhi isiyo na madini. Tanzania ina bahati sana kwani kila mkoa una madini. Kahama kuna dhahabu na Kishapu Mwadui kuna almasi na Mtwara na Mkuranga kuna gesi na Arusha kuna *Tanzanite*.

Kwa kuwa umiliki wa ardhi hizi ni wa masharti kwamba chochote chini ya ardhi siyo cha mwenye ardhi, ni mali ya Serikali, wakulima wa Bulyangh'ulu, Geita, na wakulima wa sehemu zingine za madini walihamishwa bila kuthaminisha madini chini ya mashamba yao.

· Mtazamo huu ni chanzo cha migogoro mingi kati ya wakulima na wenye migodi na pia ni chanzo cha kuikosesha nchi mapato kwani ni kawaida kwa wale waliopewa leseni za kuchimba madini kuuza migodi yao kwa fedha nyingi za kigeni na bila Serikali kuhusishwa au kupata gawio. Kama wageni wanaweza kuuza maeneo yao kwa gharama kubwa kwanini wenyeji waliopewa ardhi hiyo na Mwenyeji Mungu wasiiuze kwa bei ya soko kama mgeni aliyepewa na Serikali. Kwa mfano, Bulyanghulu iliuzwa kwa *Barrick* dola za Kimarekani million 750 au karibu trilion moja, karibu theluthi moja ya mapato yote ya kodi ya Serikali mwaka wa 2006/2007.

· Dhana kwamba ardhi ni mali ya Serikali na ni kwa matumizi ya kuiendeleza, inaipa Serikali uwezo mkubwa sana wa kutawala mali hii na ni kwa msingi huu, tumeona Serikali ikifanya maamuzi juu ya ardhi hata bila ya kuwauliza wenye ardhi.

Maamuzi ya kuhamisha watu kutoka Wilaya ya Hanang kwa nguvu, vijiji vya Gawal, Gidgamod, Murjanda, na kadhalika vyenye eneo la karibu hekari 100, 000 mwaka 1972/73 na kufanya eneo la Mashamba ya *NAFCO* kwa ajili ya kilimo cha ya ngano. Mashamba hayo sasa yamebinafisishwa kwa Mgeni kutoka Kenya ambaye sasa anawakodishia wenyeji waliofukuzwa na Serikali yao. (*Makofi*)

· Baadhi ya wenyeji hawa waliofukuzwa na wale waliofukuzwa wakati wa opereshini kijiji ndiyo waliopata maskani katika bonde la Mbalali na sasa wamefukuzwa na Serikali yao. Wenyeji wengine walio mbioni kupata madhara haya ni wakazi wa milima ya mkoani Morogoro ambao wametakiwa kuhama na Serikali yao.

Mifano mingine ni wakazi wanaokutwa na miradi ya maendeleo kama vile mabwawa na shule wanaohamishwa mara nyingine bila fidia inayotosha kuanza maisha mapya. Pamoja na udhaifu kwa baadhi ya viongozi juu ya fidia, Kambi ya Upinzani inakupongeza wewe Waziri na wizara yako kwa kusisitiza haki ya fidia kwa mujibu wa Sheria, na leo umefanya pia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mtazamo mbadala ni umiliki usio na kikomo na masharti ( *freehold* ) zaidi katika maeneo ya vijiji na katika miji masharti madogo yasiyopingana na dhana ya umiliki usio na kikomo (*permanent ownership*) na maendelezo yasiyoathiri umilikaji (*ownership independent of the right to develop*) yaani kutoendeleza ardhi kusiwe sababu ya kumnyang'anya mmiliki ardhi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya Kambi ya Upinzani ni kwamba huwezi ukakubali ardhi ni mali, ardhi ina thamani, ardhi ni dhamana ya mikopo halafu ukang'a ng'ania kutwaa ardhi isipoendelezwa. Je, kama Benki ikitwaa ardhi kwa sababu mkopo haukulipwa, utailazimisha iendeleze kama sharti la kukaa na hiyo ardhi? Dhana ya MKURABITA inapingana na mtazamo wa CCM kwamba ardhi ni mali ya Serikali na mtu anapata haki ya kuendeleza tu na si kumiliki kama mali yake.

Ili ardhi imsaidie mtanzania kama mtaji inapaswa kuwa mtaji unaoaminika, unaouzika, unaobadilishika, (*land can be exchanged like any other property*). Mtazamo huu ndiyo utaleta mapinduzi na maendeleo makubwa ya kilimo na majengo kama ilivyo katika nchi zilizoendelea. Jitihada zinazofanywa za kupima vijiji na hatimaye mashamba ya watu ni hatua kuelekea kwenye mtazamo wa ardhi ni mali na ni mtaji lakini sera rasmi ni tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika,tunajua kwa sasa mtazamo wetu si mtazamo wa CCM wala si hali iliyopo katika Sheria za sasa za ardhi. Kwa kuwa tunaishi na sheria za sasa Kambi ya Upinzani, tumeainisha pia maswala muhimu ambayo tunaitaka serikali iangalie kama njia ya kuboresha umiliki wa ardhi kwa Watanzania.

Tunafanya hivi kwa kuamini kwamba mwananchi mwenye ardhi ndiyo mwenye nchi na yuko kwenye mwelekeo wa kujikomboa kutoka lindi la umasikini. Masuala muhimu ya ardhi Tanzania kwa mtazamo wa Kambi ya Upinzani ni kama yafuatayo:

Mheshimiwa Naibu Spika, Ardhi nchini Tanzania ni nguzo kuu ya uchumi wa wananchi walio wengi hasa wanaoishi vijijini. Mustakabali wa maisha ya Mtanzania yanategemea ardhi.

Licha ya kuwa kumefanyika jitihada za makusudi za kurekebisha mfumo wa miliki na matumizi ya ardhi, lakini bado mfumo uliopo sasa wa umiliki ardhi hautoi fursa kwa wananchi wa kawaida kupata haki za ardhi hususan uhakika wa miliki (*security of tenure*).

Hii inatokana na ukweli kuwa ardhi imefunganishwa zaidi na dola na maamuzi yapo mikononi mwa wachache hususan watendaji wa Serikali ambao kwa kutumia mamlaka waliyo nayo hufanya maamuzi yanayowakosesha haki wamiliki na watumiaji wadogo.

Kwa mfano, Rais ana madaraka makubwa juu ya ardhi yanayotokana na kuwa ndiye mwenye miliki ya hatima, hivyo anaweza kuamua kubatilisha umiliki, kubadili matumizi na hata kutwaa ardhi ya aina yoyote wakati wowote kwa kile kinachoitwa maslahi ya taifa. Mfumo huu umeleta matatizo makubwa kwa watumiaji wadogo wa ardhi hasa pale ardhi yao inapochukuliwa ili kufanyika matumizi mengine hasa uwekezaji bila kuzingatia maslahi yao au kuwapa fidia kidogo isiyoendana na viwango halisi. Malalamiko ya wananchi wa Tuangoma, Buyuni na Kibada jijini Dar es salaam kuhusiana na mradi wa viwanja elfu ishirini ni sehemu tu ya ushahidi wa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni Ardhi na Katiba. Suala la ardhi kuwa sehemu ya Katiba ni jambo la msingi na muhimu. Japo kuwa Sera ya Ardhi ya 1995 inatamka kuwa ardhi itafanywa kuwa sehemu ya Katiba lakini hadi sasa ardhi nchini Tanzania si sehemu katika Katiba ya nchi bali inasimamiwa na sheria za kawaida na si sheria mama. Hivyo basi mabadiliko ya sheria za ardhi yanafanyika pasipo kuwashirikisha wananchi wengi zaidi kwa vile mabadiliko ya sheria hayatoi mjadala mpana kama ambavyo mabadiliko ya katiba yanavyofanyika. Hii inasababisha mabadiliko ya mara kwa mara ambayo yanasukumwa na nguvu ya soko bila kujali maslahi ya wananchi wa kawaida na hivyo kuathiri upatikanaji wa haki zao. Pendekezo ni kuifanya ardhi kuwa sehemu ya katiba ya nchi ili kulinda umiliki wa watumiaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inafahamu kuwa kuna juhudi kubwa zinazofanywa na taasisi za fedha kama vile mabenki nchini kubadilisha sheria za ardhi ili zisaidie zaidi benki kutwaa ardhi zilizowekwa dhamana. Huu ni mfano unaoonesha ni jinsi gani suala la ardhi lilivyo muhimu kuwekwa katika katiba ya nchi. Tunatoa mwito kwa Serikali kuliangalia jambo hili kwa kuweka kipaumbele maslahi ya wanyonge wamiliki wa ardhi wadogo wadogo kuliko maslahi ya kifedha na kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na migogoro mingi ya ardhi karibu nchi nzima. Migogoro hii ni baina ya mtu na mtu, mtu na Serikali, vijiji kwa vijiji, au vijiji na wawekezaji. Chanzo kikubwa cha migogoro hii ni kushindwa au kuwepo kwa mfumo mbovu wa umiliki na usimamizi wa ardhi. Mfumo huu kama ulivyosemwa awali

umelimbikiza madaraka kwa watu wachache ambao hawawezi kusimamia ardhi ipasavyo. Mfano Kamishna wa Ardhi, na Makamishna Wateule Wilayani ndio wenye majukumu makubwa ya kusimamia ardhi. Lakini ikumbukwe kuwa hawa watu ni wachache kumudu kazi hiyo na mara nyingine wanakosa utaalamu unaotakiwa katika kusimamia ardhi. Matokeo yake ni ucheleweshwaji wa maamuzi au kufanya maamuzi mabovu.

Mfano, ugawaji wa eneo moja mara mbili (*double allocation*), au ucheleweshwaji wa ugawaji wa ardhi hivyo kupelekea watu kujenga kiholela (*Squatters*).Tunapendekeza kuwepo na ajira za wataalamu wa kutosha ili kusaidia usimamizi wa ardhi na kuepusha migogoro isiyo ya lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukiukwaji wa Sheria. Kumekuwa pia na ukiukwaji mkubwa wa Sheria za ardhi ama kwa makusudi au kwa kutojua. Vyombo vya habari vimekuwa vikiuarifu umma matukio ya ukiukwaji wa taratibu na sheria na katika nyakati tofauti mahakama zimekuwa zikipokea kesi zinazohusiana na ukiukwaji huo. Kumekuwa na ugawaji wa maeneo kiholela, uvamizi wa fukwe za bahari ambazo wamiliki binafsi wanawanyima raia haki kwa kuzifunga kinyume cha sheria.

Sheria inataka fukwe hizo kuwa wazi kwa ajili ya matumizi ya jamii. Maeneo ya fukwe za Bahari ya Hindi huko Bagamoyo, Kigamboni na hata Dar es salaam ni ushahidi tosha wa hili. Ikumbukwe pia ujenzi usiofuata taratibu na kanuni za kisheria umepelekea kuwepo kwa majengo yasiyo na ubora. Serikali haijafanya lolote kuhakikisha kuwa watu wetu wanaishi katika makazi yenye usalama. Mfano suala la *Empire Properties* limieshia wapi? Hilo tunataka kujua. Tunaitaka Serikali kuwachukulia hatua Watendaji wanaokiuka sheria ili kudhibiti hali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uwepo wa Mipango isiyo endelevu: Serikali imejiingiza katika mpango wa kurasimisha rasilimali za wanyonye, MKURABITA. Mpango huu ni hatari kwa miliki ya ardhi hususan watumiaji wadogo wa ardhi. Hii inaweka shaka katika uhakika wa miliki na pia una madhara makubwa kwa watumiaji wa pamoja wa ardhi kama vile koo, na jamii mbalimbali hususani wafugaji ambao mfumo wa umiliki wa ardhi ni wa pamoja.

Pili, mpango huu ambao Serikali imejiingiza hauna faida zaidi ya kuipa serikali mzigo mzito kwa sababu tayari kuna mpango wa kusimamia au kutekeleza sheria za ardhi za mwaka 1999 ujulikanao kama *SPILL (Strategic Plan for Implementation of land Laws).* Mifumo hii miwili ina lengo moja, kwa nini basi isifanywe kuwa mmoja badala ya kuwa na mifumo miwili?

Mheshimiwa Naibu Spika, MKURABITA unatoa fursa kwa wananchi kutumia ardhi kama dhamana. Tunautahadharisha umma ujihadhari na kampeni ya kukopa na kuweka ardhi kama dhamana na bila ya kuwa na mradi uliosanifiwa vizuri kibiashara, kwani kufanya hivyo ni hatari ya kupoteza mashamba ya kulisha familia zao.Tunaishauri Serikali itumie vipindi vya redio na televisheni kuwaelimisha na kuwahamasisha watu

kubuni miradi yenye tija na faida kuliko kukopa bila miradi yenye faida, watapoteza ardhi ya familia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mustakabali wa Wafugaji nchini: Tanzania inasifika kwa kuwa nchi yenye mifugo mingi barani Afrika. Mingi ya mifugo hii inafugwa katika mfumo wa kuhamahama – yaani "*pastoralism*". Huu ni mfumo ambao katika MKUKUTA umekubaliwa kama sehemu ya maisha yaani "*Livelihood system*".

Pamoja na kuingizia serikali mapato na kutoa ajira bado serikali imeendelea kuupuuza mfumo huu. Hili linatokana na ukweli kwamba Serikali imekuwa ikiwanyanyasa wafugaji kwa kuwanyang'hanya maeneo yao kwa visingizio vya kutunza mazingira au kupisha wawekezaji. Hivi karibuni serikali iliunda tume kuchunguza mpango wa kuwahamisha wafugaji toka bonde la Ihefu Mkoani Mbeya na kuwapelekea Wilaya za Kisarawe, Kilwa na Lindi.

Zoezi hili liligubikwa na utata mwingi ambapo mifugo mingi iliripotiwa kufa na wafugaji kulipishwa faini na gharama kubwa za kusafirisha mifugo. Lakini mpaka sasa taarifa ya tume hiyo haijawekwa hadharani pamoja na ukweli kuwa tume hiyo imekamilisha kazi na kukabidhi ripoti yake. Je, Serikali inasema nini juu ya hilo? Tunaitaka serikali iwasilishe taarifa hii katika Bunge lako Tukufu ili ijadiliwe na Bunge zima na kutolewa uamuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia kituo cha Uwekezaji nchini (*Tanzania Investment Centre*) imeanzisha Benki ya Ardhi. Benki hii si asasi ya kifedha bali ni asasi inayotumia nyaraka zinazoonyesha ardhi ambayo inafaa kwa mwekezaji husussan wageni toka nje. Kwa mujibu wa taarifa za Mkurugenzi wa Kituo hicho hekta zipatazo milioni mbili na nusu zipo tayari kwa uwekezaji. Suala linalojitokeza hapa ni usiri wa namna ardhi hiyo ilivyopatikana na mahali ilipo. *TIC* hawajaweka wazi ardhi hiyo ipo wapi na waliipata vipi. Kinachoonekana ni taarifa za juu juu tu kuwa ardhi hiyo ipo. Kambi ya Upinzani tunachotaka ni kuelewa waziwazi ili wananchi wasije wakapoteza ardhi yao. Kumekuwa na wimbi kubwa la uwekezaji katika ardhi za vijiji. Miaka ya hivi karibuni kumekuwa na msukumo wa watu katika kutafuta maeneo ya uwekezaji hasa ardhi huko vijijini.Vijiji vingi vimejikuta vikipokea maombi ya ardhi kutoka makampuni mbalimbali.

Utafiti unaonyesha kuwa taratibu za ugawaji ardhi hazifuatwi ikiwa ni pamoja na kutoshirikisha wanavijiji katika mikutano mikuu ya vijiji.Maamuzi juu ya uwekezaji huo yanakuwa yamekwisha fanywa na Wizara au katika ngazi za Wilaya na wanavijiji wanabaki kuwa wapokeaji tu wa maamuzi. Hii imesababisha migogoro kati ya wanavijiji na wawekezaji. Maeneo yenye migogoro ni yale yanayohusisha maeneo ya hifadhi za wanyamapori mikoa ya Manyara, Arusha, Morogoro, Bonde la Mto Ruaha na Pwani. Uhamishwaji wa watu katika maeneo ya madini kama vile Buzwagi, Bulyanhulu na kwingine ni ushahidi tosha kuwa Sheria na taratibu zimekuwa hazifuatwi na kusababisha ukosefu wa uhakika wa miliki kwa mwananchi wa kawaida hasa watumiaji wadogo wa ardhi.

Miji imeendelea kupanuka kwa kasi na kumeza vijiji vilivyo pembezoni. Wananchi wamejikuta wakipoteza haki zao za ardhi na hata wanapojaribu kuzidai basi huishia kuzungushwa kulipwa fidia huku wakiendelea kuwa maskini. Ni heri miji ipanuke wima badala ya kwenda pembezoni bila ukomo kwani kwa kufanya hivyo maeneo ya vijiji vya pembezoni mwa miji yanazidi kumezwa na miji. Miji mingi imepanuka kwa njia hii. "Mradi wa Viwanja Elfu Ishirini" ni mfano wa vijiji vingi kupoteza umiliki wa ardhi na wananchi wake kupoteza mali na haki zao katika ardhi waliyokuwa wakitumia kupata riziki zao na kujikimu kimaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mabaraza ya utatuzi wa migogoro ya Ardhi yanaundwa kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya 1999, Sheria ya Ardhi Namba 4 ya 1999 na Sheria ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Namba 2 ya 2002. Hata hivyo, tangu sheria hizi zianze kufanya kazi ni vijiji vichache sana ambako mabaraza yamekwishaundwa. Aidha, yaliyoundwa kwa sehemu kubwa ni kwa msaada wa mashirika ya kiraia kama Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, Haki Ardhi, Kituo cha Msaada wa Sheria kwa Wanawake na mengineyo. Pamoja na Wizara kujitahidi na kufanya kazi nzuri kwa mwaka 2006/07 kwa kupima vijji 2668 kati ya vijiji 7000 vilivyobaki mwaka 2005/2006, na kutoa vyeti na hati za kimila, sehemu nyingine bado vijiji havijapimwa wala kupewa vyeti vya ardhi na hivyo hata mabaraza nayo hayajaundwa.

Hali hii inaendelea kusababisha migogoro ya ardhi vijijini. Rai yetu kwa serikali ni kuwa vijiji vipimwe, mabaraza yaundwe na yawezeshwe kufanya kazi kwani hata kule yalikoundwa hayawezi kujiendesha bila mafunzo wala miongozo sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama za Ardhi bado ni tatizo. Wilaya nyingi hazina Mahakama za Ardhi na wilaya chache zenye Mahakama ya Ardhi bado kumekuwa na tatizo la mahakama hizi kuwa mbali na makazi ya watu. Watendaji wa mahakama hizo pia ni wachache na hivyo kusababisha msongamano mkubwa wa kesi. Kambi ya Upinzani tunaishauri Serikali kuondoa mapungufu haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maendeleo ya Makazi: Kutokana na ukuaji wa kasi wa miji pamekuwepo na mahitaji makubwa ya nyumba za kuishi ili kukabiliana na ongezeko la watu mijini. Inakadiriwa kuwa mahitaji ya nyumba mijini ni nyumba 2, 000, 000 lakini nyumba zilizopo ni 1,448, 000 tu (rejea Hotuba ya Waziri wa Ardhi 2006/07).

Kwa mtazamo wa Kambi ya Upinzani, tunapozungumzia nyumba tunazungumzia nyumba bora angalau iwe imejengwa kwa tofali la kuchoma au saruji na kuezekwa kwa bati. Kwa upande wa vijijini upungufu wa nyumba bora ni mkubwa mno. Asilimia 52% ya nyumba zimejengwa kwa miti na tope. Uhalisi wa jambo hili ni kwamba Tanzania ya leo na kesho inahitaji makazi bora na hili halina ubishi au itikadi kwani hakuna chama kinachotaka makazi duni.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi za serikali katika kutatua suala la nyumba zimekuwa ni kuwawezesha wafanyakazi wa serikalini tu kuwa na nyumba bora kwa kuwapatia mikopo ya nyumba kutoka kwenye Mfuko wa Mikopo ya Nyumba. Umefika wakati sasa serikali ianze kuhakikisha kuwa wananchi wote hata wale ambao sio watumishi wa serikali wanawezeshwa kupata nyumba bora. “Maisha bora kwa kila mtanzania yanahitaji pia nyumba bora za kuishi”.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufikia azma hii ya kuwawezesha wananchi kuwa na nyumba bora, Kambi ya Upinzani tunasisitiza haja ya kuanzisha chombo cha kutoa mikopo kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba. Tukiwa na chombo hiki tutaweza kuwapatia wananchi wetu makazi bora, tutapanua shughuli za sekta ya ujenzi na hivyo kuongeza ajira na kupunguza umaskini wa wananchi wetu. Pia kwa kufanya hivyo mazingira ya miji yetu yataboreka. Njia nyingine ya Serikali kutatua tatizo la nyumba kwa wananchi ni kuliimarisha zaidi Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)* kama tulivyoshauri mwaka jana. Shirika liwezeshwe kwa kudhaminiwa na vyombo vya serikali (*BoT long term security bonds*), mikopo ya muda mrefu kujenga nyumba na kuziuza kwa serikali au kwa watu binafsi wenye uwezo wa kuzinunua. Zoezi hili liendeshwe kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeloe ya Makazi, ni vyema ikakumbukwa kuwa kazi zote zilizopangwa kufanywa na wizara hii katika mwaka wa fedha wa 2006/07 zilikuwa na malengo makuu matatu:

(i)· Kuongeza wigo wa ukusanyaji mapato ya serikali katika sekta ya Ardhi na Makazi ili kuwa na uwezo kifedha;

(ii) Kuwezesha wananchi kutumia raslimali ardhi kuwa nyenzo muhimu ya kuwaletea maendeleo na kuondoa umaskini;

(iii) Kuimarisha utawala bora katika sekta ya Ardhi na Makazi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo ili kudumisha haki na amani miongoni mwa watumiaji ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika lengo la kuongeza wigo wa mapato ya serikali katika sekta hii ya Ardhi na Makazi, Wizara imekusanya jumla ya shilingi 8, 632, 957, 841 hadi kufikia Mei, 2007. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 80.3% ya lengo la makusanyo ya shilingi 10, 747, 833, 000. Katika makusanyo haya kiasi cha shilingi 7, 311, 551, 487 ni ada ya pango (*land rent)* itokanayo na mashamba na viwanja. Kiasi hiki ni sawa na 85% ya makusanyo yaliyokwishapatikana.

Wizara ilikuwa na matarajio ya kukusanya kiasi kilichobaki cha shilingi 2, 114, 875, 159 hadi kufikia tarehe 30, Juni, 2007. Kambi ya Upinzani tunaipongeza Wizara hii kwa kuelekea kutimiza lengo lake la ukusanyaji mapato.

Hata hivyo, utekelezaji huu umetuonyesha kwamba Wizara hii ina uwezo zaidi wa kukusanya mapato ya serikali (*potential to collect more revenue*) ambao kama Wizara ikiongeza ubunifu inaweza kuongeza mapato.

Kambi ya Upinzani inaamini kuwa Wizara ingeweza kabisa kukusanya kiasi kikubwa zaidi cha mapato kuzidi lengo ililojiwekea kama ingefanya yafuatayo: Ingeongeza idadi ya kuridhisha ya mashamba na viwanja vilivyopimwa; ingetambua miliki nyingi za ardhi katika maeneo yaliyojengwa kiholela mijini; ingejenga uwezo na kuboresha vituo vya makusanyo ya kodi kwa kuvipatia vifaa mbalimbali vikiwemo kompyuta na programu ya kukadiria kodi; na ingetunza kumbukumbu pamoja na kuhamasisha ukusanyaji zaidi wa kodi ya pango la ardhi katika Halmashuri za Miji na Wilaya nchini kote. Aidha, Wizara ina mapungufu ya kihasibu yanayopunguza mapato halisi kama taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ilivyoonyesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2006, inaonyesha kuwa Wizara hii ilipata Hati yenye Shaka. Mapungufu ya Wizara hii yameripotiwa kuwa na:-

(i) kutoonyeshwa kwa malimbikizo ya maduhuli ya sh. 642,709, 624; kutoelezwa kwa kodi ya ardhi ya sh. 96, 727, 866;

(ii) malipo yenye shaka ya gharama za upigaji picha kutoka angani ya sh. 147,139, 665;

(iii) matumizi yenye nyaraka pungufu sh. 356, 096, 634; kulikuwa na mikopo iliyofikia muda wa kulipwa lakini haijarejeshwa ya sh. 63,288,576;

(iv) ununuzi wa bidhaa na huduma vyenye thamani ya sh.253, 323,394 ambao haukufuata sheria;

(v) kuchelewa kutoa gharama za fidia kwenye shamba kulikoisababishia serikali hasara ya sh. 62, 314, 079;

(vi) kasoro zote hizi zilifanya jumla ya fedha ambazo hazikukusanywa na kusimamiwa vizuri katika wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuwa ni sh. 1, 621,599,838.

Hii inadhihirisha kuwepo kwa mwenendo usioridhisha wa Wizara hii katika usimamizi wa fedha suala ambalo kama lingefanyiwa kazi kikamilifu basi Wizara ingeweza kuongeza kiasi cha shilingi bilioni 1.6 katika mapato yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya kazi muhimu zilizoahidiwa kufanywa na wizara hii kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Ardhi ni kukamilishwa kwa Mpango wa Taifa wa Matumizi Bora ya Ardhi mpango ambao mchakato wake ulianza katika msimu wa fedha wa 2005/06. Wizara katika hotuba yake ya bajeti mwaka jana iliarifu kuwa mapendekezo ya awali juu ya Mpango huo yalikuwa yamekwishawasilishwa na kujadiliwa na wadau mbalimbali na ikaahidi kuwa mpango huo ungekamilika katika mwaka wa fedha wa 2006/07. Kambi ya Upinzani tunataka kujua sababu zilizofanya kushindwa kuwa kukamilisha mpango huo .

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha uliopita baadhi ahadi za Wizara kuhusu maendeleo ya makazi hazikutimia. Wizara iliahidi kuanza kuandaa Mipango Kabambe (*Master Plans*) kwa jiji la Dar es Salaam, Mwanza, na Miji ya Mtwara na Bukoba. Kambi ya Upinzani inaomba kupata taarifa juu ya utekelezwaji wa shughuli hii. Akizungumzia kuhusu Mipango ya Kimkakati ya Kusimamia Ukuaji na Uendelezaji Miji, Mheshimiwa Waziri John Pombe Magufuli katika uk. 34 na 35 wa hotuba yake ya mwaka jana alisema maneno yafuatayo ninamnukuu: ‘‘Mipango hiyo huchukua muda mrefu na gharama kubwa katika utayarishaji wake ukilinganisha na uwezo wa Serikali na hivyo kushindwa kutoa mpango unaotarajiwa kwa wakati. Kwa mfano, maandalizi ya mpango wa kimkakati wa jiji la Dar es Salaam umechukua muda wa zaidi ya miaka 10 na bado haujakamilika”. Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika,nukuu hii inaeleza wazi kuwa kwa zaidi ya miaka 10 Wizara imekuwa ikiandaa Mpango wa Kimkakati wa Uendelezaji Jiji la Dar es salaam tena kwa gharama kubwa lakini hadi Agosti mwaka jana Waziri akihutubia hapa Bungeni mpango huo ulikuwa bado haujakamilika. Jiji la Dar es Salaam linabadilika kila kukicha, kipindi cha miaka zaidi ya kumi sasa tangu Serikali kuanza kuandaa mpango wa kimkakati wa jiji hili, tayari jiji lenyewe limeshabadilika sana kiasi ambacho kinaweza kufanya mpango wa kimkakati wenyewe kupoteza uhalisia *(relevance)* kwa jiji hili.

Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali ilieleze Bunge hili haya yafuatayo: (i) Sababu za msingi zilizofanya mpango huo kutokamilika kwa zaidi ya miaka kumi; (ii) Gharama zilizotumika katika uandaaji wa mpango huo kwa kipindi chote cha zaidi ya miaka kumi; na (iii) Wizara itueleze sasa iwapo Mpango wa Kimkakati huo wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam utakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kuwa Wizara hii ni kubwa na majukumu yake ni mengi na mazito. Kwa kuangalia kiasi cha fedha kilichotengwa kwa Wizara kwa mwaka wa Fedha wa 2007/2008 kwa mpango wake wa kazi kwa kipindi cha 2007/08 ni shilingi 12,715,991,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 1,976,000,000/= kwa ajili ya miradi ya Maendeleo.

Hizi zinahusisha fedha za wafadhili. Kwa mwaka wa fedha 2006/07 zilitengwa shilingi 16,208,689,000/= kwa matumizi ya kawaida na shilingi 2,065, 994,000/= kwa miradi ya maendeleo. Kwa kufanya ulinganisho wa takwimu hizo ni dhahiri kiasi kilichotengwa kimepunguzwa katika bajeti hii kwa kulingana na kile kilichotengwa mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inajiuliza ni kwa jinsi gani Wizara hii itatimiza majukumu yake wakati fedha zinazidi kupungua? Hivi ni kweli tunapanga kulingana na tulichonacho au tunafanya mazoea ya kupitisha mipango wakati fedha za kutimiza mipango hiyo hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishauri Wizara iongeze juhudi za kukusanya maduhuli na kama watavuka malengo basi Wizara ya fedha iiongezee Wizara hii fedha za

ziada ili iweze kukabili mapungufu tuliyoyataja hapo juu na kweli Wizara hii ihudumie rasilimali ardhi ambayo wote tunaitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, msiwe na wasiwasi mnapowasilisha zile nyaraka mezani maana yake zinaenda hivyo hivyo kwenye *Hansard.* Ilivyopelekwa ndivyo ulivyoiwasilisha na ndiyo *official document.*

Kwanza, nimeambiwa kuna Kikao kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa kati ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko na wajumbe wote wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge, baada ya kuahirisha Kikao hiki. Kwa hiyo, namwita Mheshimiwa Felix Mrema atafuatiwa na Mheshimiwa Athumani Janguo na Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah.

**MHE. FELIX C. MREMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie wa kwanza katika hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kwa niaba yangu mimi binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Arusha Mjini , tunatoa pole zetu na salamu za rambirambi zetu kwa kifo cha mwenzetu Mheshimiwa Marehemu Amina Chifupa. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin!*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na viongozi waliopo chini ya Wizara yao pamoja na viongozi wa Taasisi zilizopo kwenye Wizara hii kwa hotuba nzuri iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri asubuhi hii ya leo. Nimtoe hofu Mheshimiwa Waziri, mimi nainaunga mkono hoja yake moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri, nianze kwanza kwa kumpongeza na kumshukuru tena sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete. Namshukuru kwa nini? Wakati Mheshimiwa Rais alipotembelea Jimbo langu hivi karibuni tulimpeleka kwenye Kata moja, inaitwa Kata ya Revolosi sehemu inayoitwa Kolokoni. Pale mahali tuliwaweka wajasiriamali wadogo wasiopungua 800 hususan wauza mitumba ili waendelee na biashara zao za kuuza mitumba. Tulipowaweka pale hao wajasiriamali baada ya kupewa eneo hilo kwa jasho lao na kwa nguvu zao wameligeuza lile eneo kiasi kwamba sasa ni kivutio kikubwa kwenye Jiji letu la Arusha siyo tu kwa wateja wa mitumba bali hata wale wengi wetu ambao tunanunua vitu vyetu kwenye maduka ya kisasa kama ya *woolworth.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hao wajasiriamali wadogo wameigeuza ile sehemu sasa hivi wameitengeneza ndiyo inafanana na *woolworth* ya wanyonge pale kwenye Jiji la Arusha. Ukifika pale unashangaa maajabu ambao wajasiriamali wanaweza wakayafanya kama wakipangwa vizuri.

Mheshimiwa Rais alipofika pale naye pia alishangaa na alifurahishwa mno na mpaka akatoa agizo, akaagiza kwamba wale wajasiriamali mia nane na kitu wamilikishwe lile eneo na hilo lilikuwa ni tendo la kihistoria, halijapata kutokea kwa wajisiriamali wadogo kumilikishwa eneo na kwa agizo la Mheshimiwa Rais. Baada ya kuvutiwa na kazi kubwa na nzuri waliyofanya ya kujipanga vizuri wananchi wangu, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tujiunge wote kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa heshima hiyo aliyotupa ya kuenzi wajasiriamali kwa nguvu kubwa na kwa kazi kubwa waliyofanya pale kwenye Jiji la Arusha. *(Makofi*)

Lakini Rais akaendelea zaidi akatoa agizo akasema hao wajasiriamali wapewe hatimiliki yao ndani ya kipindi cha mwezi mmoja. Napenda kutoa taarifa kwamba hilo lilifanyika, wajasiriamali hao wamepewa hatimiliki katika eneo lile ndani ya mwezi mmoja. Namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maendeleo ya Makazi na wataalamu wote kwenye Wizara yake kwa kuitikia wito wa agizo la Rais kwa kutoa hatimiliki kwa kipindi kifupi kabisa ndani ya mwezi mmoja. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii ikanisukuma, pale Arusha sisi tumehamasika sana na kitendo hicho kiasi kwamba sasa tunawatafutia wajasiriamali wengine zaidi ya elfu moja mia mbili eneo lingine kule Mbauda kwenye Kata ya Sombetini ili nao kama watajipanga kama hao wengine walivyojipanga ni imani yetu kwamba Serikali itawamilikisha hao wengine 1200 kama jinsi hao wajasiriamali 800 walivyomilikishwa eneo lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, inatufundisha nini hili. Kwanza, kwamba hatimiliki zinaweza kutolewa ndani ya mwezi mmoja. Kama hatimiliki zinaweza kutolewa ndani ya mwezi mmoja kwa kutokana na agizo la Rais. Mimi ninapenda kuamini kwamba kule ndani ya Wizara wakijipanga vizuri watakuwa na tabia ya kutoa hatimiliki ndani ya mwezi moja kwa mtu yeyote yule anayehitaji hatimiliki bila kungoja agizo la Mheshimiwa Rais. Hilo ni moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, tunalojifunza hapa ni umuhimu wa Wizara hii. Hii ni Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ni sehemu muhimu sana katika uchumi wowote ule pale Duniani na sisi Tanzania siyo tofauti. Ukitaka kuchochea ongezeko la ajira ya aina yoyote matumizi ya ardhi na ujenzi wa nyumba ni sehemu muhimu sana katika kuchochea ajira.

Maisha bora kwa kila Mtanzania ni lazima uangalie sekta yako na mfumo wako ambao unawasaidia watu kuweza kujenga nyumba bora. Kichocheo cha uhakika na cha haraka cha kuharakisha ukuaji wa uchumi ili tuweze kufikia kile kiwango cha asilimia 10 kila mwaka cha *GDP* yetu, huwezi kufanya hivyo bila kuwa na matumizi mazuri ya ardhi na ujenzi wa nyumba za kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifupi utekelezaji wa Ilani yetu ya Uchaguzi ya CCM unategemea kwa kiwango kikubwa sana Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Sasa Mheshimiwa Waziri John Magufuli anaheshimika sana kwa

uwezo wake wa kipekee wa kusukuma mambo. Hii haina ubishi na amesukuma mambo mengi sana na mazuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi wakati mwingine ninakuwa na wasiwasi anapoamua kusukuma mambo ambayo mimi yananisumbua sumbua kidogo. Nitoe mfano, ametishia wale wote ambao wameshindwa kuendeleza maeneo waliyomilikishwa kuwanyang'anya hatimiliki zao. Kweli kabisa sheria inamruhusu lakini hao tunawaonea jamani. Wanaoshindwa kuendeleza maeneo hayo hawakushindwa kwa sababu hawataki kuyaendeleza yale maeneo, wameshindwa kwa sababu hatuna mfumo wa kuwawezesha kuviendeleza vile viwanja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaangalia madaktari wangu pale Arusha; nawaangalia wauguzi wangu pale *Mount Meru* Hospitali; walimu wangu pale Arusha, polisi, mahakimu, wafanayakazi Serikalini, watapata wapi fedha za kuweza kuendeleza viwanja vyao kwa kasi hiyo inayotakiwa na Sheria? Maana yake ni ndoto ya kila binadamu kwamba anataka awe na nyumba bora katika uhai wa maisha yake. Sasa tuwatishia tunataka kuwanyang'anya viwanja, maana yake tunawambia watumie mbinu na ubunifu katika maeneo yao hayo, watafute njia za kujiwezesha wao wenyewe. Halafu tunakuja kuwageukia, tunawaambia rushwa, rushwa! Wachekwe jamani!

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi Wakristo tunayo sala yetu ya Bwana. Ndani ya sala ile kuna kipengele hiki, kinasema "usitutie majaribuni bali utuokoe kwa yule mwovu." Sasa tusiwatie wafanyakazi wetu majaribuni tuwaokoe kwa yale maovu, tutengeneze mfumo utakaowawezesha wao kuendeleza viwanja vyao kabla hatujafikiria suala la kuwanyang'anya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa sasa Mheshimiwa John Magufuli atumie nguvu yake hiyo ambayo tunajua anayo kusukuma *system* yetu ya Serikali kuweza kuharakisha kuleta mfumo wa *Mortgage Finance* katika nchi yetu. Anao uwezo mzuri sana wa kufanya hivyo. Aweke nguvu yake kwa mwenzake Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Gavana na ndani ya Serikali humo wasukumwe ili waweze kusukuma *system* yetu hiyo tuzibe hili pengo ambalo lipo katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kabisa kwamba Sheria ya Ardhi imefanyiwa marekebisho ya kutosha ya kuweza kuridhisha wale wote ambao wana nia safi ya kuja kuwekeza kwenye sekta hii. Lakini hizi jitihada za sasa za kujaribu kutwambia bado mabadiliko mengine yanahitajika. Sheria ya Ardhi, mimi naona ni ya kutubabaisha tu. Kwa sababu sisi tuko tayari kubabaishwa ndiyo sababu kazi hii inaonekana ni ngumu sana. Mheshimiwa Waziri John Magufuli afanye kazi hii iwe rahisi, waambie hao watu wasitubabaishe, kinachohitaji sasa ni sheria ndogo ya kutoa msukumo ili *mortgage finance* iletwe katika nchi yetu kama ilivyo katika nchi nyingine zote duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiunganisha na hilo ni suala la *Tanzania Housing Bank*. Tungeweza kabisa kutumia rasilimali iliyopo kwenye *National Housing Cooperation* iwe ndiyo kama msingi wa kuanzisha *Tanzania Housing Bank*. Tulifanya makosa sana kuacha ile *Tanzania Housing Bank* yetu ya zamani kufa. Katika nchi

zingine *Housing Bank* ikiwa na matatizo haiachwi ikafa, inasaidiwa kurekebishwa mpaka iendelee kutoa mchango wake muhimu katika Taifa. Sisi tumeachia *Housing Bank* ikafa. Sasa tutumie rasilimali tuliyonayo ya *National Housing Cooperation* tuanzishe *Bank* yetu. Maana yake tukingoja *Private Sector* ifanye kazi hiyo tutangoja mpaka kiama, hao watu wanataka kupata fedha kwa njia laini, *mortgage finance* siyo kazi laini. Kazi hii inataka Mnyamwezi na yeye Mheshimiwa John Magufuli ni Mnyamwezi mzuri sana wa kusaidia nchi yetu kuweza kupata *Housing Bank* ifanye kazi hii nzito katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia lingine wametwambia kwamba tunahitaji Sheria ya *Condominium and Sectional Property Act*. Mimi nakubaliana nao kabisa hao wanaosema hivyo. Kweli hapa kuna hiyo *gap* na tunaijua kwamba ipo. Sasa ni mategemeo yetu; na hii ilikuwa ni dhana hii ya hoja ambayo nilikuwa nataka kuiwasilisha katika Bunge hili, lakini kwa sababu nimeshawishiwa kwamba Serikali inalifanyia kazi, nitataka tu wapokee nakala ya ile hoja ambayo ninayo ili iwasaidie wao katika kukamilisha hilo. Lakini ni imani yangu kwamba katika Bunge linalokuja Wizara italeta huo Muswada wa *Condominium and Sectional Property Act*, ili pengo hili ambalo lipo katika Taifa letu lizibwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni pengo ambalo sasa hivi mtu unayekaa kwenye *apartments,* kama wale wa kwangu wa *National Housing* kule Ngarenaro, huwezi ukauza kwa sababu hakuna utaratibu wa kumuuzia ile *apartment* pale alipo. Lakini kukiwa na hii *Condominium and Sectional Property Act,* kwa wale wote wanaokaa kwenye maghorofa sasa watakuwa na hatimiliki ya kununua yale maghorofa yao na itakuwa ni hatimiliki kama nyumba ya mwingine yeyote yule ambaye yupo chini ya ardhi. Sasa namshauri Mheshimiwa Waziri hii *Condominium and Sectional Property Act*, ikamilishwe wailete hapa haraka. Maana yake hiki ndicho kitu kitakachosaidia uchumi wetu kukua kwa jinsi tunavyotaka ukue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wamesema kuna upungufu wa asilimia milioni 3 katika nchi hii na kila mwaka mahitaji mapya yanayokuja kwenye soko ni zaidi 200,000. 120,000 mijini, 80, 000 kwenye vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa changamoto yetu kubwa katika Wizara itaondoa namna gani juu ya upungufu huu mkubwa uliopo katika Sekta yetu hii? Wizara itahakikisha namna gani kwamba ina mfumo utakaohakikisha kwamba kila wakati uchumi unaweza ukumudu na kuhakikisha kwamba watu wanaendelea kujenga nyumba za kuishi au za biashara?

Hii ndiyo changamoto kubwa aliyonayo Mheshimiwa Waziri. Sasa akiweka nguvu zake katika maeneo hayo mimi ninaamini kabisa ile sifa yake nzuri ambayo inang'ara itaendelea kungara na Wizara hii itaendelea kuchangia kuhakikisha kwamba zile ajira milioni moja zinapatikana kama Ilani yetu ya Uchaguzi inavyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wa CCM wanawake mnatangaziwa kwamba mtakuwa na Kikao baada ya Kufunga Bunge saa 7.00 mchana kwenye chumba namba 122 *floor* ya kwanza. Tunaendelea na Mheshimiwa Athumani Janguo na Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah ajiandae.

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipatia nafasi na mimi nichangie kwenye hoja hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kusimama hapa ili niweze kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijafanya hivyo, ningependa kwa niaba ya wananchi wa Kisarawe nipeleke salamu zangu za rambirambi kwa watani wetu kule Usukumani kwa kumpoteza Mheshimiwa Stephen Kazi aliyepata ajali hivi karibuni. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. Amin!

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo nami nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wasaidizi wao wote kwa hotuba nzuri ambayo inaonyesha kutupa matumaini mema sana. Kilimo tumesema ni uti wa mgongo, lakini kilimo bila ya ardhi hakitokuwa kilimo, hali kadhalika viwanda na sekta yoyote ile nyingine. Hakuna sekta ambayo inaweza ikasimama yenyewe bila ardhi. Kwa hiyo, ni muhimu sana ardhi kuifanyia mipango mizuri iweze kuinufaisha Tanzania hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kuipongeza Wizara kwa jinsi ilivyoweza kusimamia zoezi la upimaji wa vijiji na matumizi bora ya ardhi. Kama hotuba inavyoonyesha, katika Wilaya yangu ya Kisarawe kati ya vijiji 76, vijiji 70 vimeishapimwa ingawa hapa inaonyesha vijiji 75 kwenye ukurasa wa 51 wa kiambatisho. Vile vijiji 5 vilivyonyeshwa chini ya Kata ya Magawa, vipo Mkuranga siyo Kisarawe. Lakini ninaamini kwamba vijiji vile 6 vilivyobaki navyo vitapitiwa na zoezi hilo litakuwa limekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, bado nina matatizo na Wizara kuhusu maeneo mawili. La kwanza, juu ya utoaji wa hatimiliki. Pamoja na msemaji aliyetangulia kusifu, lakini yanayotokea katika maeneo mengine ni kinyume cha hivyo. Nadhani bila shaka ule mfano wa Arusha ni kwa sababu Mheshimiwa Rais aligiza.

Sasa hatuwezi kukaa kila wakati Rais aagize ndiyo hatimiliki zitolewe. Makampuni mengi pamoja na mashirika ya umma na watu binafsi wamecheleweshewa hatimiliki kwa muda mrefu sana. Kuna mfano, ambao unanihusu mwenyewe sitaki niueleze hapa, lakini Mheshimiwa Waziri nimeshamwandikia na ninaamini ataufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini makampuni mengi hasa Mashirika ya Umma yanapata hati chafu za wakaguzi wa mahesabu kwa sababu hawawezi kuonyesha hatimiliki za maeneo wanamofanyia kazi, na hili limekuwepo kwa muda mrefu sana na nilitegemea kwamba jitihada zilizofanywa huko nyuma na wakati huu ambapo kijana wangu, Mheshimiwa John Magufuli ameingia pale ambaye alikuwa ameonyesha makali makubwa sana kwenye Wizara ya Miundombinu, basi angepangusa pangusa haya yakamalizika. Lakini hakuna kitu, hali bado ni mbaya!

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile wengi wetu tunakerwa na urasimu ambao upo ndani ya Wizara. Labda niseme kuwa Mheshimiwa Waziri ameghubikwa na jinamizi. Maana nilitegemea kabisa kwamba urasimu wa pale ndani angeweza kuumaliza.

Nataka nitoe mfano mmoja tu, nao ni katika kuunga mkono jitihada za Rais katika kuleta wawekezaji na kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Mbunge wa Kisarawe ametafuta wawekezaji akawapata watu wanaoitwa *Sun Bio Fuels* kutoka Uingereza wakaunda Kampuni ya *Sun Bio Fuels Tanzania Limited* ambayo inataka kupanda mkangara au "*getropha*" katika Wilaya ya Kisarawe na kuweza kutengeneza nishati itakayoweza kusaidia matumizi ya nyumbani na hata kwenye magari na vilevile kuuza nchi za nje, nchi ikajipatia fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwetu sisi mradi huu ulikuwa muhimu sana. Pwani na Wilaya ya Kisarawe hatujawahi kuwa na mradi au hatuna migodi. Lakini tunapopata mradi wa kuendeleza kilimo, basi tunauheshimu kweli na tunataka uende kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeuchelewesha sana mradi huu kwa sababu ambazo ninashindwa kuzieleza. Ni kwamba mradi huu utakuwa na faida nyingi, kwanza utatoa ajira ya zaidi ya watu 3,000 kwa Awamu ya kwanza tu.

Pili, waendeshaji watashiriki katika harakati za kujenga nchi, na tatu, utaleta hizo fedha za kigeni. Pia kwa sababu ni ardhi ambayo ipo vijijini mradi upo tayari kulipa fidia kwa wanavijiji na siyo fidia tu hata Serikali nayo itapata ada ya ulipaji wa fidia isiyopungua shilingi milioni 261 na itasimamiwa na Shirika la Uwekezaji ambapo watapata ada ya usimamizi wao wa shilingi zisizopungua milioni 26. Fidia kwa wananchi itakuwa siyo chini ya shilingi milioni 800, lakini mradi huu umesuasua kwa muda wa miaka mitatu.

Sababu mbalimbali zinatolewa ikiwemo sababu ya kutaka kuhakikisha kwamba wananchi wanapata fidia sawasawa. Naheshimu sana maneno yalikuwa katika ukurasa wa 62 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri na ninapenda kuyanukuu: "Natoa rai kwa mamlaka na Taasisi mbalimbali zinazotoa ardhi za wananchi hao kuheshimu sheria, kanuni, taratibu za utoaji ardhi ili wananchi walipwe fidia kwa mujibu wa sheria hizo." Namsifu sana Waziri na nampongeza kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kila kitu ukitaka kukifanya zaidi ya vile inavyotakiwa inakuwa bughudha, "*too much of anything is harmful*." Hapa Kampuni na Wilaya wamejitahidi kwenda kukaa na vijiji, kijiji kwa vijiji, na Kampuni ikatafuta

*consultants* kutoka *UCLAS* na pia wakafanya tathmini ambayo imetoa taarifa kwamba wangeweza kuwalipa wananchi hizo shilingi zaidi ya milioni 800 na ikathibitishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali *(Chief Valuer).*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado Wizara ya Ardhi hawataki kutoa kibali mradi uanze. Baada ya yote hayo Mbunge alilazimika kwenda Ikulu na Mheshimiwa Rais akaagiza, bado hakuna utekelezaji. Sasa tunauliza kulikoni?

Huyu Mheshimiwa John Magufuli ambaye alikuwa anavuma sana kila mahali, sasa katiwa ndani ya kufuli. Mimi ninaamini kwamba Mheshimiwa Waziri angeweza kujitahida akafanya kila liwezekanalo kuhakikisha kwamba mradi huu unafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wiki mbili zilizopita nilikwenda kwa Waziri Mkuu ili kusudi asaidie kusukuma. Waziri Mkuu alipozungumza na Katibu Mkuu akaambiwa kwamba sasa hivi dokezo limetayarishwa ili kusudi ardhi hiyo ihuishwe kutoka katika ardhi ya vijiji kuwa katika *general land.*

Nafikiri jibu lile lilikuwa la kumridhisha Waziri Mkuu, kuonekana kwamba, tayari matayarisho yamefanywa. Siku tano baadaye, nikaingia ofisini kwa Waziri na nampa pole kwa matatizo ya kuuguliwa. Lakini habari nilizozipata ni kwamba, dokezo lile halijatoka katika Ofisi ya Waziri kwenda Ikulu. Ningeomba Mheshimiwa Waziri, atakapojibu aniambie lini maombi yatapelekwa na lini kibali kitapatikana na kikirudi kutoka Ikulu lini Wizara itapeleka kule Wilayani, pamoja na wawekezaji ili mradi huu uanze? Bila ya hivyo, kama sikupata jibu la kuridhisha nasikitika, itakuwa vigumu kwangu kuiunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina haja nigongewe kengele, nilitaka niseme hilo tu na lingine analifahamu, naamini kabisa kwamba atanijibu. Hiyo kengele ya kwanza, ya pili haitonifikia, kwa hiyo, nataka majibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri; lini kibali kitatolewa ili wananchi wangu wapate ajira na ajira ya kujiajiri kwa sababu watapewa mbegu vilevile za kuweza kuwa *outgrowers* na niambiwe lini tutaweza kuwaruhusu wawekezaji ili waweze kuutekeleza Mradi huu? Serikali haikosi chochote kama nilivyosema, itapata ada ya shilingi milioni 261, *TIC* shilingi milioni 26, sasa huku kuchelewa kote kunatoka wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, ninaamini kwamba, Mheshimiwa Waziri atanijibu vizuri ili niweze kuunga mkono hoja yake. Asante.

**NAIBU SPIKA:** Asante sana, hata mimi nalijua hilo. Mheshimiwa Waziri ni vizuri mkafanya bidii.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi niweze kuchangia hoja ya bajeti ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, ambayo iko mbele yetu. Awali ya yote, naipongeza Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, vilevile nawapongeza wao wenyewe, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na

Wataalamu wake wote, kwa kazi nzuri ambayo inaonekana katika nchi yetu ya kutatua matatizo ya ardhi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuzungumzia kijiji kimoja kilichokuwepo Wilaya ya Pangani, kinachojulikana kama Kijiji cha Mivumoni. Niliuliza swali hapa Bungeni kwamba, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ilipeleka barua kuwasimamisha wanakijiji wale wasilime mpaka hapo watakapopata maelekezo mengine tofauti. Majibu niliyoyapata ni kwamba, usimamishaji wa wakulima hao katika kijiji kile ulikuwa ni wa muda mfupi, lakini mimi bado ninahoji Mamlaka ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, kuwasimamisha wanakijiji kulima katika ardhi yao, ambayo ni kijiji kilichomilikishwa na kina hati ya kumilikishwa. Kijiji hicho na hicho ni kijiji ambacho tayari kina uongozi wa kijiji, kimeshaingia katika mchakato wa kupiga kura.

Wamemchagua Rais, wamemchagua Mbunge, wamemchagua Diwani na wamechagua uongozi wao wa Serikali ya Kijiji na Vitongoji, lakini Ofisi ya Mkuu wa Mkoa inasema simamisheni msilime. Sasa najua Wizara ya Ardhi imetoa hati ya kuandikisha kijiji hicho kihalali kabisa, Wizara nyingine inatoa maamuzi ya kusimamisha. Sasa hapo sielewi, Wizara inayohusiana na masuala ya ardhi wakatoa vibali, wakatoa hatimiliki, wakatoa na hati za kuandikisha vijiji, halafu Wizara nyingine inasimamisha ni kwamba hawaheshimu zile Sheria za Wizara ya Ardhi!

Mimi nasema wananchi wale wameathirika kisaikolojia, wamesimamisha shughuli zao za maendeleo, wamerudi nyuma. Pale pana Shule ya Msingi, pana wawekezaji wamejenga hospitali, Mashirika ya Dini wamejenga *infrastructure* zao, kuna visima vya maji, gharama kubwa. Kigezo kikubwa ni kwamba kuna mwekezaji ametaka kuja kuwekeza katika kile kijiji akataka kuchukua na kile kijiji. Wanasema hiki kijiji wamevamia eneo la uwekezaji.

Nimewaomba watuthibishie kwa barua kutoka *PSRC* kama *PSRC* wamewapa hilo eneo, hakuna kitu kama hicho. Sasa Mheshimiwa Waziri, labda leo unaweza ukatufafanulia, Wananchi wa Kijiji cha Mivumoni na wao wasikie ni sababu zipi zilizopelekea kusimamishwa wasifanye shughuli zao za maendeleo na mimi naamini kwamba, Serikali imetoa hati ya kuandikisha kijiji kile?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Sheria Namba 5 ya Mwaka 1999, ambayo inawasaidia wanavijiji katika mambo mengi kumiliki ardhi yao, kupima maeneo yao ya mashamba, lakini vilevile Halmashauri imepewa jukumu la kusimamia kukusanya mapato ya ardhi katika Halmashauri zetu. Pesa hizi zinapokuja Wizarani ile kasma ambayo inatakiwa irudi kwenye Halmashauri haifiki. Tuna matatizo ya kutatua migogoro ambayo inajitokeza inayohamasisha kutoa semina ili wananchi waelewe wapate kumilikishwa ardhi yao kwa kutoa hati za kimila. Sasa Mheshimiwa Waziri, labda atusaidie ni kwa sababu zipi fedha hizi zinachelewa kufikishwa katika Halmashauri zetu na hatimaye ziweze kufanya kazi ya kuweza kusaidia kutatua matatizo na migogoro na vilevile kuhamasisha wananchi ili waweze kupima maeneo yao na hatimaye waingie katika utaratibu wa MKUKUTA na MKURABITA na hatimaye kukopa pesa kwa ajili ya maendeleo yao?

Lakini vilevile tuna matatizo ya vifaa kama vya kompyuta, kuweka rekodi sawa sawa kama mnavyofanya sasa Wizarani, lakini Wizara ya Maliasili imefanikiwa jambo kama hilo kwa kuweka *data* nzuri, kujua maeneo yanayohusika na rekodi ambazo wanaweza wakafuatilia kwa karibu. Mimi nafikiri kwa Wizara ya Ardhi, kuweka vifaa kama hivi katika Halmashauri zetu, itawasaidia na ninyi Wizara kuweza kutatua matatizo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nataka niongelee suala zima la ujenzi wa hoteli za kitalii katika fukwe za bahari. Kama mnavyoelewa, Pangani tuna fukwe nzuri, tuna hifadhi ya Saadan ni kivutio kikubwa ambacho watalii wanapenda kutembelea yale maeneo, lakini hakuna uwekezaji wa kutosha, ambao unaweza ukasaidia wawekezaji hawa kuwekeza. Kwa sababu kwanza kuna tatizo la barabara, hilo naamini Serikali inalifahamu na inalishughulikia. Lakini vilevile nataka kuzungumzia mipango mizuri ya kujenga hizi hoteli za kitalii. Hoteli hizi zinajengwa kufuata taratibu, wanajenga ndani ya mita 60 ambazo haziruhusiwi kujenga. Niliuliza swali hapa, sheria inakataza lakini hoteli hizi bado zipo, hakuna hatua zilizochukuliwa. Nimeshazungumza sana, narudia tena.

Mimi nimwombe Mheshimiwa Waziri, apate siku moja aje Pangani, awe mgeni wangu. Njoo Kiserikali uwe mgeni wangu, nikupeleke kwenye hayo maeneo ujionee hali halisi ya ujenzi wa hizi hoteli, ambazo hazifuati taratibu za kisheria. Kuna watu wamepewa maeneo, eneo lenyewe ni hatua 70 kutoka baharini, akiacha hatua zile 60 ana hatua 10 tu za ujenzi, atajengaje hoteli hizo katika hatua za mita 10. Kwa hiyo, kiutaratibu inatakiwa hicho kiwanja au eneo hilo lisipewe mtu yeyote kwa sababu ni eneo la hifadhi ya ardhi katika fukwe za bahari. Sasa nakuomba sana Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri, mkipata nafasi tutembeleeni ili mjionee hali halisi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujenga makazi ya wananchi na utaratibu mzuri wa Wizara ya Ardhi kutoa viwanja kwa wananchi wajenge, tunajua hali za wananchi wetu uwezo wa kila mmoja kuweza kujenga katika maeneo ambayo tunayakuta wananchi wamepewa, *low density,* lakini inaweza ikamchukua miaka mingi kuweza kujenga nyumba ya kuishi. Utakuta unapita muda wa miaka mitatu hajakiendeleza kile kiwanja. Sasa Serikali imetunga sheria, mtu asiyeendeleza kiwanja hicho kwa miaka mitatu, atanyang'anywa.

Mimi naishauri Serikali kupitia Wizara hii ya Ardhi, kwa nini sasa hivi msitenge maeneo maalum na wapo wawekezaji wa ndani na nje, maeneo ya kuweza kujenga *railway estates*? Wenzetu wanachukua maeneo makubwa, wanajenga nyumba zinazofanana na ni nzuri utakuta ule mji unakua haraka haraka, kwa sababu wana uwezo. Wanajua namna ya kupata fedha kwenye mabenki, wanawekeza katika ujenzi wa *railway estates* ili nyumba zile ziwe zinavutia na hatimaye wananchi waweze sasa kununua zile nyumba kutoka kwao na walipe kwa awamu, hatimaye wananchi wale watakuwa wana nyumba.

Vilevile mandhari ya mji ule au miji itakuwa inapendeza na hatimaye *infrastructure* zote; barabara, maji na umeme, itakuwa ni rahisi kuliko kwa utaratibu huu

wa kwetu. Sisemi kwamba wasipewe viwanja na kujenga, lakini Serikali sasa hivi iweke utaratibu maalum kwamba, mji huu hapa unataka uendelezwe kwa haraka, basi tupewe maeneo makubwa na wawekezaji wawekeze katika kujenga nyumba kwa utaratibu wa *railway estates.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni-*declare interest,* inanihusu mimi mwenyewe ni haki yangu na mimi kujishughulisha na mambo ya kilimo, kumiliki ardhi. Nataka kumwuliza Kamishana wa Ardhi kupitia kwako Mheshimiwa Waziri, mimi nina shamba nasubiri hatimiliki. Nina mgogoro, nafikiri umekwisha, leo ni miaka 15 suala hili halijapata ufumbuzi, sasa nakuomba unisaidie labda baadaye tukutane na Kamishna, hatimaye nipate majibu ya mwisho. Lakini naweza kukupa *reference* ya *L 171727 Farm No. 646* na *LO No. 171728 Farm No. 408*. Suala hili liko kwa Kamishna nasubiri kauli yake, maandishi yake, idhini yake, nipewe hatimiliki na mimi niweze kujiendeleza, sitoweza kulima wakati nashika mkongojo, angalau sasa hivi nina nguvu kidogo, naweza nikashughulika na mimi nikaacha urithi kwa watoto na wao wajiendeleze.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nasema naunga mkono hoja na asante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Asante sana. Mheshimiwa Mohamed R. Abdallah, ametumia kifungu kidogo cha saba, ana-*declare interest* zake.

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia katika Wizara yetu hii ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Temeke, ambao nawapenda sana sana, nataka kuwaambia tu kwamba, ile barabara ya kero sana ya Yombo Vituka - Makangarawe, tumepata fedha na itatengenezwa vizuri sana, wasiwe na wasi wasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kwa mapenzi makubwa, kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kaka yangu, Mheshimiwa John P. Magufuli, Naibu Waziri, dada yangu, Mheshimiwa Rita L. Mlaki, Katibu Mkuu, mama yangu, Mama Salome Sijaona na wafanyakazi wote wa Ardhi na Mashirika husika, chini ya Wizara hiyo hasa hasa Shirika la Nyumba la Taifa, ambalo Makao Makuu yake yako pale Temeke, jirani na Ofisi yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja katika eneo la fidia Kurasini. Wananchi wa Kurasini, kwa ridhaa yao walikubali baada ya viongozi wao wapendwa wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwenda kusema nao akiwepo Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Mbunge na Diwani, wakaridhia kwa hiari yao kuachia maeneo ya Kurasini ili liwe eneo la viwanda. Tathmini ilifanywa Novemba, 2006 wakaahidiwa Machi, 2007, watakuwa wamepata malipo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua unapowekewa X na kuambiwa unatakiwa upishe kwa ajili ya maendeleo mengine ya maana zaidi. Wananchi wale wengi nyumba zile walikuwa wamepangisha watu lakini wale watu kwa wasiwasi ikabidi wahame

kwenye nyumba zile, kutafuta nyumba nyingine za kupanga, matokeo yake wale wenye nyumba mpaka leo hawajapata fidia zao na wengine walikuwa wanaishi kwa kutegemea pango ya nyumba zao. Sasa wananchi wale wamenituma, Waziri ni kaka yangu, namheshimu sana na nampenda sana, anajua pamoja na Naibu Waziri. Wamenituma kwamba, jioni walikuwa wanaomba kusikia kauli ya Serikali ni lini watalipwa malipo yao? Lakini kulikuwa na ahadi ya kuwapatia viwanja Kibada. Kibada tumepima viwanja, tumegawa na vingine tunapima. Sasa itapendeza Mheshimiwa Waziri pia ahadi hiyo ya kutoa viwanja Kibada, nione akizungumza ili nitakaporudi nikasimamie wapate viwanja husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nilikuwa napenda kuchangia kwenye utaratibu wa upimaji viwanja katika Jiji la Dar es Salaam. Tulipima viwanja vya kwanza pale Kibada, tukatoa siku 14, bahati mbaya hata wale wengine walioomba kutokana na kipato chao cha kutafutatafuta, ilivyofika siku 14 wale walioshindwa kulipa viwanja vyote vilipelekwa Wizarani. Lakini katikati kulikuwa na mchezo unaendelea, watu wanakwenda wanapata viwanja kwa ujanja. Sasa nilikuwa nauliza pale kwenye Manispaa ya Temeke tulitoa tenda, watu waliomba kwa tenda wakapata viwanja na waliokosa viwanja vikaenda Wizarani na vikifika Wizarani; mbona hatusikii mkitangaza tenda?

Lakini si hivyo tu ebu Mheshimiwa Waziri tusaidie naamini mikoa yote viwanja vyote vinasimamiwa na Manispaa husika au Halmashauri husika iweje viwanja vya Dar es Salaam Wizara mnaviingilia kupita kiasi. Kwa nini hamtuachii wenyewe, mkishapima kama mmelipa fidia kwa hela zenu tuachieni tuuze na tutawauzia tunaowajua, wananchi wetu wa maeneo husika halafu tuwapeni fedha zenu. Lakini si hivyo, kuna kitu najua Mheshimiwa Waziri wala Naibu Waziri, haya hamyajui, mimi najua utendaji wenu na nawapenda kweli kweli, lakini nawaambia kwa kuwasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kitu kingine, vile viwanja vya *beach* hata Manispaa hatupewi kuvitoa, vinatoka huko huko Wizarani. Sasa mtuambie, Wizarani mnafanya utaratibu gani na sisi tunahitaji na watu wetu wanahitaji. Naamini hayo nitapata majibu jioni na hayo ni maswali ya Wabunge wote wa Dar es Salaam, bahati mbaya wale ambao hawakupata nafasi ya kuchangia, lakini nasema kwa niaba yao wote pamoja na Naibu Mawaziri na Mawaziri wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dar es Salaam tuna Shirika la *DDC* (Shirika la Maendeleo Dar es Salaam), linasimamia masuala ya burudani. Hata Mheshimiwa Kapteni John Komba, alianzia pale Magomeni *DDC,* ndiyo akafahamika mpaka hapo alipofikia. Pale Keko mwaka 1982, Mama Sijaona akiwa Mchumi wa Jiji, baada ya Jiji kujenga Keko pale, alimkabidhi Meneja wa *DDC Keko* kuendesha pale. Akiwa Mchumi wa Jiji, lakini akiwa Wizarani pale Katibu Mkuu, eneo letu lile la Keko limemegwa amepewa mtu *GAPCO Petrol Station,* ameweka Kituo cha Mafuta pale. Sasa najua Mama Sijaona halijui hili, lakini nataka kumwambia Mheshimiwa Waziri, lile eneo Mama Sijaona akiwa Mchumi wa Jiji, alilikabidhi kwa Meneja wa *DDC Keko.* Alipokuwa Katibu Mkuu, najua hafahamu, eneo lile lile limetolewa, limekatwa katikati amepewa mtu mwingine. Sasa kwa niaba ya Wananchi wa Dar es Salaam, Meya wa Dar es Salaam na Wabunge wote, tunataka lile eneo lirudi. Tena tunashangaa hati yetu

hatuna, lakini yule bwana ana hati ya kumiliki. Mheshimiwa Waziri, pia tunaomba jioni utueleze hilo. Tunaomba Wizara isimamie sera na sheria kama nilivyosema mwanzo, masuala ya kugawa viwanja waachiwe Halmashauri, Manispaa na maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikwambia tuna maombi kwa hati za Kariakoo, Magomeni Kondoa na Mlimani Park. Lengo letu tuige nyayo nzuri za *National Housing* sasa tutafute wawekezaji waweze kuwekeza pale, tupate vitu vizuri vyenye kulipa kwa ajili ya Jiji. Mimi nalipongeza sana Shirika la Nyumba la Taifa, chini ya Uongozi wa Mkurugenzi wake Mkuu. Kwa utaratibu wake mzuri wa kwenda na wakati; kwa kasi mpya, ari mpya na nguvu mpya; kuingia ubia na watu wenye uwezo; Mashirika yenye uwezo na kujenga nyumba nzuri; kubadilisha Jiji la Dar es Salaam na mikoa mingine Tanzania kwa ujumla. Sisi tunaomba kasi hiyo iendelee, pale kwenye nyumba za kuchokachoka Upanga, Chang'ombe na maeneo mengine, basi tuendelee kuboresha ili papendeze.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hisani yako, kwa sababu nina muda kama utaniruhusu, jana nilikuwa na jambo muhimu sikulisema, ukiniruhusu niseme kidogo muda wangu uliobaki.

**NAIBU SPIKA:** Utasema ikigongwa kengele basi.

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Asante Mheshimiwa Naibu Spika. Jana niliwasilisha tatizo kubwa sana la Kiwanda cha Alfa, kinachotengeneza viberiti pale Temeke, kimeajiri wafanyakazi 350 ambao wanahudumia karibu familia ya watu 1,400. Sasa kwa maneno mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri kwamba, tutahakikisha viwanda vyetu vya ndani tunaviwezesha kwanza, lakini Kiwanda kile kimeomba malighafi ya viberiti ambayo ni magogo, tena mpaka barua ya Waziri wa Viwanda kwenda kwa Waziri wa Maliasili na Utalii, iliandikwa tarehe 7 Machi, 2007, lakini cha ajabu mpaka leo kiwanda kile kimefungwa, wafanyakazi 350 wako nje ya ajira wakisubiri malighafi.

Sasa leo vyombo vya habari vimemrekodi vizuri Mheshimiwa Waziri akisema kwamba, tutahakikisha viwanda vyetu vya ndani kwanza, tunavipa malighafi. Jana niliandika hakunijibu na bahati mbaya sisi watatu; mimi, Mheshimiwa Mussa A. Zungu na Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi, tuliposimama kwenye vifungu, hatukupata nafasi muda ulikwisha. Kwa hiyo, kwa kweli naomba wale wananchi 350 ambao wana familia karibu watu 1,400, ndio walioniwezesha mimi na chama kipenzi cha CCM kufika hapa tulipo. Naomba wapate malighafi ni stahili zao ili kiwanda kile cha viberiti kiweze kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Suala hili Mheshimiwa Waziri atanijibu jioni kwa utaratibu wetu ule wa kila siku.

**NAIBU SPIKA:** Asante. Lile la malighafi hatajibu kwa sababu hahusiki, wamekusikia wanaohusika.

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Sawa sawa, ujumbe umemfikia Mheshimiwa Profesa Jumanne A. Maghembe na analijua, lakini jana kidogo hakulijibu.

**MHE EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kushukuru kwanza, kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Viongozi na wafanyakazi wote wa Wizara hii, kwa kutuletea bajeti nzuri na hotuba ambayo kwa kweli imetengenezwa kwa ufanisi mkubwa. Katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri, ametuelezea kwa kirefu kidogo, kazi nyingi sana ambazo wameweza kuzifanya katika kipindi hiki cha mwaka mmoja uliopita na pia katika kuelezea mipango yao ya muda ujao, tunafarijika kwamba hiyo kazi nzuri itaendelezwa. Nawapa pongezi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuzungumzia matatizo ambayo yanatokana na makazi holela ya hapa mjini Dodoma. Ni ukweli ambao uko dhahiri kwamba, ujenzi wa Makao Makuu umekuwa ukisuasua kwa miaka mingi sana iliyopita na hata sasa hivi ingawa kuna dalili za kuchangamka lakini bado unasuasua. Wakati Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu inaundwa kwenye miaka ya 1970, ari ilikuwa kubwa na ilikuwa inaonekana na wakati ule iliwezesha mipango kamambe kutayarishwa. Wakati ule *Master Plan* ambayo iliainisha maeneo mbalimbali na matumizi yake, ilitayarishwa na ikapitishwa. Kulikuwa na mwelekeo kwamba, hiyo *Master Plan* ingefuatwa kama ilivyokuwa imewekwa. Kwa bahati mbaya sana, miaka iliyofuata ari ikawa imepungua kwa sababu mbalimbali na hiyo ikasababisha matatizo ya makazi holela kuibuka. Makazi haya holela yaliibuka kwa sababu *CDA*, ambao ndio waliopewa Mamlaka ya Kusimamia Ujenzi wa Makao Makuu ama walizembea au waliyafumbia macho maendeleo ya makazi hayo holela. Kati ya vitongoji ambavyo vimekumbwa na tatizo hilo ni Chinyoya kwenye Kata ya Kilimani.

Mheshimiwa Naibu Spika, makazi yaliyopo Chinyoya kwa hivi sasa baadhi yake ni ya asili kwa maana ya kwamba, yalikuwepo hata kabla Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu haijaundwa na kabla ya Mpango Kamambe wa Mji wa Dodoma haujatayarishwa. Lakini pia kuna makazi ambayo yalijengwa baada ya *CDA* kuanza kazi na yalijengwa katika hicho kipindi ambacho nasema mambo yalikuwa yanasuasua. Walio wengi waliojenga Chinyoya kwa wakati huo ni Maafisa, ambao walikuwa wamestaafu toka kwenye Serikali na sehemu mbalimbali. Watu ambao kwa kweli kipato chao ni kidogo na hata zile nguvu za kuendelea kupata fedha na mali ili waweze kujiendeleza zaidi kimakazi ni kama vile zimeshapungua. Kwa hiyo, kile ambacho wamekiwekeza pale, ndiyo hicho hicho ambacho wanakitegemea kwa maisha yao ambayo wameyabakiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, makazi haya yameleta mtafaruku mkubwa sana. Mwaka 1994, amri ilitolewa kuyavunja haya makazi lakini wananchi wa kitongoji hicho kwa kweli siwezi kusema, walisimama imara lakini ilionekana kwamba, lilitokea tishio la amani kuvunjika. Busara zikatumika na hilo zoezi likawa limesitishwa. Lakini Serikali

tangu wakati ule na hadi hivi sasa, bado imetamka kwamba, hawa wakazi wa Chinyoya lazima wahamishwe kwa nguvu na bila fidia. Ahadi za kwamba, watapewa mahali pengine zilizotolewa lakini hata hayo maeneo mengine waliyokuwa wameahidiwa, inaelekea kama vile ile ahadi imekuwa ni hewa kwa sababu wakazi wa Chinyoya bado wako pale pale na tatizo lao bado linaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Chinyoya kwa hivi sasa wanaombi moja tu nalo linatokana na kwamba si wao tu wamehusika na matatizo ya makazi holela hapa Dodoma, kuna wenzao wa Chamwino na *Oyster Bay,* ambao pia makazi yao yalikuwa baada ya *CDA* kukamilisha ramani au mipango ya matumizi ya ardhi katika mji huu. Lakini wenzao sasa hivi wameshapimiwa upya hayo maeneo yameboreshwa na yameboreshwa pale pale ambapo walikuwa wamejenga kwa maana kwamba, miundombinu imeongezwa. Baadhi yao ilibidi wafidiwe ili kutoa nafasi kwa ajili ya barabara na miundombinu mingine. Lakini wamerekebishiwa makazi yao pale pale walipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyojua, Serikali kwa kweli haipendelei ujenzi holela. Lakini hali halisi ni kwamba, zaidi ya asilimia 75 ya ujenzi katika miji yetu ni ujenzi holela na Serikali imeshatamka mara nyingi kwamba, kinachofanyika sasa hivi ni kupanga upya au kupima upya ardhi ili watu wasishawishike kujenga kwenye *squatter areas.* Lakini kwa maeneo ambayo tayari yalishaathirika, wale waliopo pale wapimiwe ili yale makazi yaweze kuboreshwa.

Kama tunavyojua, kule Manzese Dar es Salaam, kwa msaada wa Benki Kuu na kwa fedha za Serikali, kazi kubwa imefanyika na yale makazi yameboreka. Kwa hiyo, wakazi wa Chinyoya na mimi nikiwa Mwakilishi wao, ombi letu ni hilo tu na ombi linajikita kwenye suala kwamba, Dodoma kwa kweli ardhi ipo na ni kubwa. Kwa sababu tunapozungumzia Dodoma, tunazungumzia Manispaa yote mfano mzuri ni kwamba, Chuo Kikuu wakati kilipoomba ardhi, wameweza kupewa hekta karibu 6,000, ardhi ambayo kwa sehemu kubwa ilikuwa haijakaliwa na watu.

Kwa hiyo, mimi na Wananchi wa Chinyoya tunasema kwamba, inawezekana kabisa kwa Serikali kubadilisha matumizi ya pale mahali ili mradi tuwanusuru hawa wananchi kwa sababu ni wananchi ambao kipato chao ni kidogo, ukiwaondoa pale ni kama umeshawaumiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ombi ni hilo na nina imani kabisa kilio cha Wananchi wa Chinyoya kitasikilizwa ili huu mtafaruku ambao umekuwepo kwa muda mrefu sana uweze kuwa umeondoshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la fidia ya Wananchi wa Msalato, ambao wanatakiwa kupisha ujenzi wa Kiwanja cha Ndege. Suala hili nililizungumzia kwa maandishi kwenye Bajeti ya Wizara ya Miundombinu, lakini nadhani pia hapa ni mahali pake. Ni suala ambalo limechukua muda mrefu, hawa wananchi wanashindwa kujiendeleza kwa sababu tathmini ya fidia ya nyumba zao ilishafanyika na hawaruhusiwi tena kufanya maendeleo yoyote katika sehemu zile ambapo wapo. Kwa hiyo, suala la

kuwalipa fidia ili wawe huru kuweza kwenda mahali pengine wakajiendeleze binafsi ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, yangu ni hayo tu na kabla kengele haijanigongea, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii, nami niweze kuchangia mchana huu. Awali ya yote, naomba kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Jaji Augustino Ramadhan, kwa kuteuliwa kwake kuwa Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini naomba kutoa pongozi nyingi na lukuki kwa mdogo wangu, Mheshimiwa John Pombe Magufuli, ikiwezekana jina la Pombe liondoke maana yake halina sifa nzuri na msaidizi wake, dada yangu, Mheshimiwa Rita L. Mlaki na mama yangu, Bibi Salome Sijaona. Hawa nawafahamu kama wachapakazi wazuri. Lakini pia naomba nitoe pongezi kwa baadhi ya watumishi wa Wizara hiyo, ambao kwa ufahamu wangu, sifahamu kama ni watendaji wazuri wa kazi lakini ni watendaji wazuri wa kazi ambao hapa na pale wametufikisha hapa tulipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa mimi binafsi sitaongelea vizuri sana Wizara hii na asilimia zangu nadhani nitakazounga mkono ni 55 na 45 siungi mkono. Maana yake mimi siwezi nikaunga mkono kwa asilimia mia moja, wakati kuna mambo ambayo nayakosoa, nitakuwa nasema uongo. Kila mtu analalamika, kila anayesimama na Wizara nyingi zinalalamikiwa na unapolalamika maana yake kuna upungufu na huo ndio mwanzo, tuanze kujitambua Watanzania wengi kwamba tunamapungufu mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, si katika Wizara hii tu katika kila Wizara. Atakaposimama Mheshimiwa Mbunge, katika Halmashauri zetu atakaposimama Diwani na hata ukitembelea kwa wananchi ni lawama, malalamiko tujiulize tuna tatizo gani. Akisimama mtu aliyewahi kuwa Waziri katika Serikali naye atalalamika na pengine atalalamikia hata Wizara aliyokuwa anaifanyia kazi. *(Makofi)*

Akisimama aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara fulani, kama vile akina Mheshimiwa Raynald A. Mrope, waliowahi kuwa Waheshimiwa Mawaziri kama Mheshimiwa Athumani S. Janguo na wengine wote watalalamika, kwa nini? Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, atalalamika naye aliwahi kuwa Waziri huko na wengineo kila mtu analalamika! Kwanza, ninyi mliopata nafasi mkaingia huko, mkapata nafasi huko mkatoka, leo mnalalamika; mtuambie mnacholalamikia ni nini? *(Makofi)*

Kwa mfano, Mheshimiwa Athumani S. Janguo, amesema hapa kwamba, kuna urasimu mkubwa katika Wizara ya Ardhi na si huko tu maeneo mengi kuna urasimu mkubwa lakini kuna wasomi wazuri wanaoongoza Wizara hizo, elimu hiyo inayowafanya waendeshe Wizara hizo na Idara hizo ni *competent?* Ni elimu iliyokusudiwa kufanya kazi hizo au ni elimu ile Mwalimu Nyerere aliyosema kwamba, sio elimu inayomsaidia Mtanzania ni elimu inayokusaidia wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuje kwa mfano katika upimaji wa viwanja, naweza nikamkumbusha Mheshimiwa Rita L. Mlaki pale katika eneo lake la Wazo Hill, kule kwenye kiwanda anapolalamikiwa na wananchi wake wa Madale. Kwa mfano, ile barabarabа inayoelekea kwa Mheshimiwa Rashid Kawawa, ambapo muda mwingi sana wananchi wamekuwa wakiitumia hiyo barabara na wananchi wanaoishi katika eneo hilo wamekuwa wakiipita muda mrefu. Wale wawekezaji bila kutegemea wamefunga barabara hiyo, mgogoro umekwenda Serikalini ikaamuliwa barabara ifunguliwe; ikafunguliwa. Mgogoro huu bahati nzuri ninaufahamu vizuri, lakini leo hii ukienda pale utaona mawe yamewekwa na baadhi ya magari makubwa yanapopita, wanahonga wale maaskari ndipo wapite. Baadhi ya Sheria zinaeleza kwamba, kama barabara imekuwa ikitumiwa na wananchi kwa muda mrefu na mhusika mwenyewe hayupo, basi barabara hiyo inabaki ya wananchi. Ninaomba wananchi wale muwasaidie ile barabara waweze kuendelea kuitumia na eneo hilo wanalolalamikia muweze kuangalia malalamiko yao tena. Huo ni mfano tu na bahati nzuri kwa sababu wewe mwenyewe upo kwenye Wizara ya Ardhi, nadhani hilo utaweza kulishughulikia kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu wa ardhi, nadhani tuone aibu. Huwa nafikiria wakati fulani hivi hawa watu wa ardhi, wanaopima hivi viwanja na kuweka *shape* ya mji, hivi huwa wanapata nafasi ya kutembelea nchi nyingine au wanasoma kwenye vyuo vyetu tu halafu wanabakia hapa hapa nchini na wazo analokuwanalo ni kwamba, kwa sababu mtumishi fulani kakaa miaka miwili pale, kajenga pale nyumba nzuri na mshahara wangu haunitoshi na mimi nikienda pale lazima nipate rushwa ili nijenge nyumba nzuri. Ndipo atagawa kiwanja kimoja kwa watu wawili, atakuwepo Nyami pale, atakuwepo Batenga, atakuwepo Ali, kiwanja kimoja. Ndivyo tunavyojenga miji yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapopima viwanja hivi ili ujenge nyumba ni lazima uwe na ramani ya nyumba, lazima upewe *permit* ya kujenga na lazima wahusika wajue. Mnafanya hivyo? Hamfanyi hivyo, matokeo yake mahali panapotakiwa kujenga nyumba ya mbele, zitaanza kujengwa nyumba za nyuma. Miji yetu inaonekana ni ovyo. Wapo Maafisa Ardhi wengine wazuri sana wanaofaa, lakini wanakatishwa tamaa na mipango holela, mibovu na urasimu uliokithiri na ambao haufai. Hivi kwa mfano, hamwoni aibu mnapoliita Jiji la Dar es Salaam ni Jiji, kwanza mimi sipendi kuishi Dar es Salaam, nenda Manzese kwa mfano, eti ni Jiji, nenda Mbagala, nenda Kigamboni eti ni Jiji! Wataalam mnafurahia kuita ni Jiji la Dar es Salaam! Tumesoma vizuri, tumemaliza elimu za vyuo vikuu, kwa ajili ya kuchora miji mizuri, je udhaifu na uchafu ndiyo mnafurahia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi wamepanda ndege na wale mliopata bahati ya kupita maeneo ya Kampala au Nairobi, miji kama vile ya Harale kwa mfano, hapa hapa karibu piteni miji kama vile ya Lilongwe, halafu ndege hiyo iwe inakuja Dar es Salaam kutua na ipite maeneo ya Magomeni, Manzese kwenda kutua uwanja wa Mwalimu Nyerere, unaanza kujiuliza mara mbili, tatu; je, tuna wasomi wanaojua kutengeneza miji au tuna mfano wa wasomi? Aibu. *(Makofi)*

Ni aibu kuliita Dar es Salaam Jiji ni uchafu. Njoo Mji Mkuu wa Tanzania. Nilipokuwa London mwezi uliopita, tumekaa katika eneo la *West Minister* pale Bunge

lilipo, nilikuwa nimealikwa na baadhi ya Wabunge kwenda kuhudhuria Bunge lao. Tulikwenda kwenye *pub* moja tukakaa, kuna Madiwani fulani walikuwa wanakuja kwenye Jimbo langu wiki kesho yake. Sasa wanabishana Mji Mkuu ni Dar es Salaam wale wanzao wanasema hapana, Mji Mkuu *is Dodoma but we think is Dar es Salaam*. Mimi siku-*comment,* wanasema *is Dodoma but we think is Dar es Salaam*. Juzi juzi nilipokuwa nakwenda kuhudhuria ile semina ya watu wa Bandari, tulipoanza kutua nilitazama Makao Makuu ya Tanzania, Dodoma ni kichekesho. Hakuna hadhi ya Makao Makuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna kwanza, *plan* unayofikiria kuna *future* ya Makao Makuu ya Dodoma. Ndiyo tutaiita Dodoma Makao Makuu, inawezekana ikapita miaka 100 hadi 300 tutaita tu Makao Makuu Dodoma; tuna *plan* gani ya kuiweka Dodoma Makao Makuu? Jana nilikuwa napita Dar es Salaam asubuhi, kabla sijaja mchana hapa, nilikuta katika baadhi ya Wizara, maghorofa yanajengwa ndani ya Wizara je, ni kukarabati na si kujenga, Dodoma huwa inabakia pale pale. Nikijaribu kutembea kwenda labda Maili Mbili au kule Mnadani, hata lile eneo wanalosema kuna Chuo Kikuu, maeneo ya Chimwaga, ipo *plan* gani unayoonesha kwamba sasa Mji Mkuu wa Dodoma unajengwa? Serikali lazima ifike sehemu fulani ielewe kwamba, ili upewe heshima ya nchi ni pamoja na kujenga na kuendeleza miji yenu na ku-*plan* miji yenu. Ili hata watu wakija wanasema *that town or city is well planned. (Makofi)*

Unaona hapa ni kichochoro hata kupitisha bomba hujui litapitaje, hata kupitisha mtaro wa maji machafu hujui utapitaje, hata kupitisha lori lenyewe la mchanga ili ukajenge nyumba ya tatu kule mbele hujui litapitaje, bahati mbaya ukitaka kupeleka umeme nalo hilo ni gumu sana. Halafu unakaa unajivuna unasema tuna wataalam wanaojua ku-*plan* miji. Tunachezea elimu yetu bure na tunatukanisha taifa letu.

Lakini uholela wa wananchi wanapojenga kwenye hizi *squatter areas,* kesho na kesho kutwa tunasema tunafumba macho tunahalalisha tu. Tunahalalisha madhambi yetu sisi wenyewe. Maana pengine mimi nikijiona nimekaa kwenye Wizara ile na ile na nilikuwa mtu wa rushwa na pengine nilishiriki katika rushwa ile, wananchi kutengeneza mazingira ya kutokupewa viwanja mwisho wakajenga holela, kesho na kesho kutwa nitahalalisha tu kwamba tupitishe sheria na kadhalika. Kwa hiyo, tunapitisha Sheria kwa makosa tuliyoyafanya na miji yetu iendelee kuwa mibovu. Hatujengi hata kidogo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninaomba Serikali yenyewe ihakikishe inatoa fedha za kutosha kwenye Wizara inayohusika ili Wizara inayohusika iweze kutengeneza ramani na michoro ya miji kikamilifu.

Mheshimiwa John P. Magufuli ni mchapakazi na nimtendaji mzuri sana. Lakini wanapotokea akina Mheshimiwa John P. Magufuli kama yupo mmoja, wawili au watatu watafanya nini? Mimi Nyami hapa nikiona Mheshimiwa John P. Magufuli anafanya vizuri, anapata sifa, nitaona wivu kwa sababu sijasifiwa ningependa nisifiwe. Nani asiyependa kusifiwa, lakini sifiwa kwa kazi nzuri uliyoifanya, mwenzako akisifiwa inakuwa nongwa kwa nini? Tulio wengi tunaogopa mambo mengi, hatutaki kuoenekana

kwamba wenzetu wanaotenda makosa tunawadhibiti kikamilifu. Tuna woga; hivi woga wetu utakwenda nao mpaka lini? Malalamiko yetu sisi Watanzania yatakwenda mpaka lini? Kila mtu kulalamika, Waziri alalamike, Katibu Mkuu alalamike, Watumishi walalamike, Wabunge walalamike, Madiwani walalamike na wananchi walalamike; tunamlalamikia nani?

Acheni malalamiko sasa tuanze kushikana mikono na huu umjomba, ushangazi, udada, mtoto wangu, nipachikie pale, ndiyo huo unaotuponza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapaswa sasa twende kwa viwango vya elimu yetu na kwa kufuata sheria. Sheria za Tanzania ni nyingi mno. Taratibu, sijui mikakati, mambo mengi na vipo vingi mno hatuvitekelezi. Ni mkakati wa leo, kesho na kesho kutwa tunasahau tuliyoanza tunaanza kingine kipya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 55. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Asante sana. Nashukuru dakika zetu tano haziwezi kutosha kwa mchangiaji mwingine. Kwa hiyo, tukirudi mchana tutakuwa na wachangiaji watatu; Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama na Mheshimiwa Juma H. Killimbah. Kwa hiyo, Mawaziri nao watakuwa na saa moja tu wote wawili, halafu tutakuwa na Kamati muda wa saa moja.

Waheshimiwa Wabunge, sina tangazo lingine, nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 06.55 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tulipositisha Shughuli za Bunge mchana, nilisema atapewa nafasi Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama na Mheshimiwa Juma H. Kilimbah atafuatia.

Mbele yetu tuna wageni wa Wabunge wa Mkoa wa Ruvuma; yupo Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Ruvuma, Wenyeviti UWT Wilaya, Makatibu Wilaya na Wajumbe Mkutano Mkuu wa Taifa. Naomba muwasalimie Wabunge. Asanteni, poleni na safari ninyi jamaa zangu, karibuni. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi jioni hii ili nami nichangie machache kwenye hoja hii ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Nashukuru pia kwamba, umeniweka jioni hii ili yale nitakayoyasema, Waziri asipate nafasi ya kuyasahau wakati atakapokuwa anahitimisha hoja yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba nzuri sana, yenye ufafanuzi mzuri wa kazi nyingi walizofanya mwaka uliopita na matumaini ya mwaka huu unaofuata. Lakini kabla ya

kuendelea na pongezi hizo, kuna mambo matatu niliyotumwa kutoka kwenye Manispaa ya Kinondoni na kutoka kwenye Jimbo langu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza linahusu tatizo dogo la mpaka lililopo kati ya Kinondoni na Kisarawe. Mheshimiwa Naibu Waziri, amepata kushughulikia tatizo hili na ikaelekea kama lilikuwa linafikia katika kufanyiwa uamuzi. Lakini, ningeomba kwamba, wakati anashughulikia tatizo hili, lishughulikiwe kwa utaratibu shirikishi, utakaowashirikisha wananchi wanaohusika wa Vitongoji vya Kisopwa, Kwembe na King'azi, pamoja na Manispaa ya Kinondoni, Halmashauri ya Kisarawe na Mikoa inayohusika ili tatizo hili limalizike, lisije likaleta hali ya kutokuelewana kati ya wanaohusika. Ningeomba hili Mheshimiwa Waziri, anikubalie na alifuatilie.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, linahusu hifadhi ya barabara. Katika eneo ninalozungumzia, hifadhi ya barabara ni pana sana, ni mita 120 kutoka kati kati ya barabara kwa kila upande. Kutokana na upana huo, watu wengi sana waliojenga katika eneo hilo, wamekumbwa na hili tatizo. Mheshimiwa Waziri, alipata kulishughulikia alipokuwa anaongoza Wizara inayohusika na ujenzi. Sasa hivi yuko katika Wizara inayoshughulika na utoaji wa hati za kumiliki maeneo haya na kuna wananchi ambao wana hati za kumiliki maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maombi matatu: La kwanza, kuangalia ni jinsi gani tutakavyoshughulika na wale wananchi walio na hati walizopewa na Wizara ya Ardhi ili kuhakikisha kwamba, zile hati walizopewa zinaheshimiwa kwa kuwa zimetolewa na Serikali, zimetolewa na Wizara yenye jukumu hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kuheshimu maagizo yaliyotolewa na Marais wetu kwamba, wananchi wanaoishi kwenye hifadhi za barabara ilimradi hifadhi hizo hazihitajiki sasa hivi kupanua barabara, basi wataachwa wakae mpaka kipindi hicho kitakapokwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, linahusu Manispaa ya Kinondoni. Kwa mujibu wa Sheria Na. 9 ya mwaka 1982 - *The Local Government Finances Act,* Kifungu cha 6(i)(5), kinasema kwamba: "Asilimia 20 ya fedha zote zitakazokusanywa na Serikali kutokana na *land rent*, itatolewa kwa Halmashauri ya Mji unaohusika." Kwa Kiingereza inasema hivi; *"20% of all money collected by the Central Government as land rent under the Land Act* itatolewa kama *revenue* kwa Halmashauri inayohusika."

Kwa miaka minne hizi fedha hazijatolewa na tunakisia kwamba, kwa Halmashauri ya Kinondoni peke yake, bado Ilala, bado Temeke, kiasi cha fedha ambacho tungekuwa tumepewa ni shilingi 1,600,000,000. Kwa hiyo, ningeomba sana Waziri alishughulikie suala hili ili kuhakikisha kwamba, fedha hizi zinapatikana. Kuna sababu zinazotolewa kwamba, hizi Manispaa siyo wakala, lakini hizo sababu hazizungumzwi kwenye sheria. Sheria inasema mapato ya Halmashauri ya Mji yatatokana na asilimia 20 ya *land rent*, hakuna suala la uwakala hapa ni suala la hizi fedha kutolewa. Nahisi kwamba tatizo hili liko zaidi Dar es Salaam, kwa sababu Wizara ipo pale na inashiriki katika kukusanya

mapato ya *land rent*. Kule Kigoma na kwingineko, sidhani kama tatizo hili lipo. Kwa hiyo, naomba sana Waziri ashughulikie suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende katika yale ambayo nilikuwa nakusudia kuchangia. Nianze na kumpongeza sana Waziri, kwa kuongeza sana viwanja vilivyopimwa kufikia 49,000. Hongera sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna tatizo moja kubwa sana, viwanja hivi vinauzwa kwa bei kubwa. Nimeulizia nikaambiwa kiwanja kimoja ni kati ya shilingi 900,000 kwa kiwanja kidogo na kwa kiwanja kikubwa kile mnachoita *low density,* inakwenda mpaka milioni nne. Sasa, mwanachi mwenye kipato cha kawaida wa Jiji la Dar es Salaam, hawezi kumudu kununua kiwanja. Kwa kuwa hataweza kumudu kununua kiwanja, atakwenda kujenga kwenye maeneo ambayo hayakupangwa, atakwenda kujenga kwenye makorongo ambako ni *hazardous land*, ni mahali pa hatari kwa sababu yakitokea mafuriko watapata matatizo. Watakaomudu kununua viwanja hivi ni wale ambao wana unafuu wa kipato. Kwa hiyo, tutakuwa sasa tunagawa makazi ya Dar es Salaam kuwa makazi ya wenye kipato chenye unafuu, ambao watakaa kwenye maeneo yaliyopimwa na walio na kipato kidogo, hawana ujanja, isipokuwa kwenda kukaa kwenye maeneo ambayo hayakupimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimshauri Waziri kwamba, katika kuuza viwanja hivi, tuangalie jinsi ya kushughulika na wananchi wenye vipato vidogo ili na wao wapate viwanja katika maeneo yaliyopimwa na kupunguza hili tatizo la wananchi walio wengi kuishi katika maeneo ambayo hayakupangwa. Kuwepo na upendeleo maalum kwa wananchi hawa, kama ikibidi Serikali iwape ruzuku ili waweze kupata viwanja hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili linalohusiana na viwanja hivi ni wale wananchi wanaokutwa katika maeneo yale, wanaoyamiliki kama mashamba ama kama maeneo yao. Naomba hawa nao wapewe kipaumbele katika kugawiwa viwanja hivi ili wapewe viwanja vya kukidhi mahitaji ya familia zao. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, alitazame suala hili maana inaelekea kwamba huko tunakokwenda linaweza kuwa ni chanzo cha mgogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo linaambatana na hili ni ukweli kwamba, miji yetu mingi haikupangwa. Tunasema asilimia 75 ya Jiji la Dar es Salaam ni makazi ambayo hayakupangwa. Mimi nafikiri ni zaidi ya asilimia 75, kwa sababu watu wameendelea kujenga sasa tumefika Bunju, tumefika mwisho kabisa wa Mkoa wa Dar es Salaam. Jiji la Dar es Salaam limepanuka na linapanuka bila kupimwa. Natambua kwa nini tatizo hili limekuwepo ni kutokana na matatizo yaliyopata kuwepo ya kutopima viwanja na ilikuwa inafanyika makusudi, kwa ushirikiano kati ya watumishi wa Serikali za Mitaa na Wizara, kupima viwanja vichache tu ili kuviuza kwa bei kubwa. Kwa hiyo, viwanja vikawa adimu, havipatikani na wananchi wakalazimika kujitafutia mahali watakapojenga makazi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ningeomba Waziri kazi yake ya kwanza kabisa iwe ni kudhibiti hili tatizo. Viwanja vipatikane kwa bei nzuri, vipatikane kwa wingi, wananchi waweze kujenga, tuwe na wananchi wanaoishi katika makaazi yaliyopangwa. Hili tatizo la watu kujimegea maeneo na kujenga wanavyoona inawafaa ni tatizo ambalo nafikiri linapatikana Tanzania tu, sidhani kama kuna nchi nyingine yenye tatizo kama hili. Lakini sheria zipo na sheria ni kali sana juu ya suala hili. Huruhusiwi kujenga katika eneo la mji bila kuwa na kibali cha mamlaka iliyoko katika mji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini, watu wanajenga na wanajenga kwa sababu hakuna usimamizi, wanajenga kwa sababu hatukuweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba mtu yeyote anayejenga bila kupata *permit* anasimamishwa mpaka apate hiyo *permit* na hiyo *permit* sasa inapatikana kwa mbinde, kwa hiyo wananchi wanalazimika kujitetea kwa kufanya lile wanaloweza. Kwa hiyo, naomba sana Waziri ahakikishe kwamba unajengwa uwezo wa kupima viwanja kwa wingi na ka bei nafuu ili wananchi waweze kuvipata kwa urahisi. Lakini, wakati huo huo tuhakikishe kwamba tunarekebisha upimaji wa miji yetu ili haya makazi yasiyopimwa yapungue. Asilimia zaidi ya 80 na ni miji yetu yote, hakuna hata mji mmoja wenye nafuu. Yote ni makaazi tu ambayo hayakupimwa na hili ni tatizo kubwa kweli kweli ambalo ningeomba sana Mheshimiwa Waziri alishughulikie na alishughulikie kwa bidii zake zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kupongeza Shirika la Nyumba la Taifa *(National Housing Corporation).* Wanajitahidi sana katika mazingira magumu kujaribu kupunguza tatizo la makaazi katika nchi hii. Lakini, ukiangalia kiasi wanachopunguza ni kiasi kidogo sana. Kwa Shirika ni kiasi kikubwa, lakini ukiliangalia Kitaifa, mahitaji ya miji yote ya Tanzania ni kiasi kidogo sana, nyumba 224 kwa mfano, ni kiasi kidogo sana. Mheshimiwa Waziri katika paragraph ya 76 anakiri kwamba tatizo kubwa la Shirika la Nyumba la Taifa ni kukosa mfumo wa kuwapatia mkopo. Hawawezi kupata mkopo wakajenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipata kuzungumza kwamba kuna haja ya kuanzisha Benki ya Nyumba, Benki ambayo ingeanzishwa ikatoa mikopo kwa Shirika hili, ikatoa mikopo kwa wananchi, Shirika likajenga, mwananchi akaenda kununua nyumba. Sasa, nilitegemea Waziri angelizungumzia suala hili na kutueleza ni lini Benki hiyo itakapopatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Felix C. Mrema, amezungumzia mambo ya *Mortgage Finance*, tulitegemea kwamba utaratibu ungekuwa umeshawekwa kwamba, sasa unaweza ukakopa, ukajenga nyumba yako, uka-*mortgage*, ukaishi mahali ambapo panastahili na ambapo pamepimwa. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, atueleze ni nini ambacho Serikali inafanya katika eneo hili ili kuhakikisha kwamba, huu utaratibu kwamba Mtanzania anajenga kwa fedha taslimu kutoka mfukoni ni utaratibu usiowezekana na hakuna nchi nyingine inayofanya mambo kama haya ni sisi Watanzania na lazima tujisifu sana kwamba nyumba nyingi tulizonazo tumejenga bila mkopo kutoka kwa mtu yeyote. Kwa hiyo, ningeomba sana hili nalo litazamwe. Iwepo Benki ya Nyumba na Benki hiyo itukopeshe pesa ili tuweze sasa kujenga nyumba za hadhi inayofaa na kwa wingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nizungumzie mambo mengine mawili, sijui kama dakika zilizobaki zinatosha. Lingine ni hili suala la kujenga miji upya. Wale ambao mmetembelea Dar es Salaam, mtakuwa mmeona Kariakoo inavyojengwa upya sasa hivi, vijumba vingi vidogo, virefu vinavyokwenda mpaka ghorofa ya 20. Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipata wasi wasi na vighorofa vile, akaunda hata Tume ya kwenda kuchunguza kama vinaweza kusimama bila kuangukia watu. Sasa sehemu nyingi za miji yetu zinahitaji kupangwa upya na kujengwa upya kwa utaratibu sasa utakaotupa miji ya kisasa. Naomba Waziri alitazame hili na atakapotujibu, alizungumzie kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo lingine la kujenga *Satellite Towns*. Tatizo letu sisi kwa mfano, pale Dar es Salaam ukitaka sindano, lazima usafiri kutoka Kawe mpaka kati kati ya Jiji, kwa kuwa hatukuweka utaratibu wa kuwa na huduma zote pale wanapokaa watu. Kwa hiyo, ningeomba hili nalo lizingatiwe na litazamwe na liwekewe utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naambiwa wameanza Luguruni kupima viwanja pale, nawashukuru sana kwamba wameanzia kwenye Jimbo langu. Lakini, kuna maeneo mengine kama Goba, Kibamba na kwingineko, tupime *Satellite Towns* zinazojitosheleza kwa kila kitu, mtu akiamka anapata mahitaji yake yote pale pale alipo, hana haja ya kusafiri kwenda kusababisha msongamano wa magari barabarani, ambao unamsababisha Waziri Mkuu aweke utaratibu wa njia tatu ili tuweze kufika kati kati ya Mji. Ningeomba sana hilo.

Lakini, katika hilo vilevile tuangalie miji inayotuzunguka, huwezi ku-*plan* maendeleo ya Dar es Salaam bila ku-*plan* maendeleo ya Kibaha, Bagamoyo, Kisarawe na Mkuranga. Lazima tu-*plan* hii miji kwa pamoja na tugawe baadhi ya mahitaji ya miji hii kwenda hivyo hivyo. Tusipofanya hivyo, tutakuwa na matatizo makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni kwamba, hii miji inahitaji kuwa na mpango mkubwa, *Master Plan* iliyoandaliwa inayoonesha Mji utakuwaje. Ukienda ukapima viwanja kwa ajili ya makazi bila kuzingatia kwamba, kuna huduma zingine zinazohitajika, unajitafutia matatizo. Mwaka 1971, Dar es Salaam ilikuwa na *Master Plan* ambayo haikufuatwa kabisa, kila mtu alijijengea alivyoona inafaa. Tunahitaji tena kuwa na *Master Plan* nyingine na sasa hivi ni rahisi zaidi kutengeneza *Master Plan* kuliko wakati ule kwa sababu unaweza kutumia *Satellite Pictures*, unaweza kufanya *Aerial Photography* wanayozungumzia. Lakini, wanazungumzia kwamba ukipata mawingu, hawapati picha, sasa yanakuwa ni matatizo. Sijui tutafanyaje mawingu yasitokee?

Lakini tunahitaji kuwa na *Master Plans* zitakazo-*guide* matumizi ya uendelezaji wa miji yetu. Tusipokuwa na *Master Plans* hizo, tutakuwa na miji ambayo hata kama tukipanga makazi, bado kutakuwa kuna uholela mkubwa sana ambao baadae itabidi tuje tukauondoe kwa kuondoa makazi hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nisingependa nipigiwe kengele ya pili, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nampongeza Mheshimiwa Waziri. Naomba majibu kwa hayo machache niliyomuwasilishia na kwa sasa naunga mkono hoja yake. Asante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante. Kwanza kabisa, naomba nimshukuru Mheshimiwa Charles N. Keenja, kanisaidia kunipunguzia yale niliyotaka kuzungumza, kwa hiyo muda wangu utakuwa mzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni rasilimali ya msingi katika kutekeleza Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini. Ili ardhi iweze kukidhi hilo, lazima ipangiwe mikakati ya uhakika. Isipopangiwa mikakati ya uhakika, ndio unakuta miji yetu inakaa katika hali ya uholela *(Shunt Towns)*. Kwa hiyo, mimi namwomba Waziri na nataka kuzungumzia suala zima la Kibaha, sizungumzii zaidi ya Kibaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti ya 2006/2007, katika Kamati ya Matumizi niliinuka, nikamwuliza Waziri, Rais aliahidi tena mbele ya hadhara kwamba, Mji wa Kibaha atahakikisha uwe ni Mji ambao unafanana na Makao Makuu ya Mkoa, atahakikisha analeta viwanda na akasema atahakikisha una barabara. Nikamwuliza Waziri, yeye kama Wizara yake ina mkakati gani? Akaniambia Ahadi ya Rais ni lazima itekelezwe na ataitekeleza. Lakini naomba kusema, inawezekana mwaka jana hakuwa na pesa, mwaka huu sijui imepangwa wapi, ataniambia katika kutekeleza Ahadi ya Rais na kama alivyosema Ahadi ya Rais ni amri, sasa anisaidie hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miji mingi Tanzania inaanza katika *Shunt Towns* na hii inaanza kwa sababu hatuna mtazamo wa mbele wa kuhakikisha tunaipanga miji yetu. Hivi sasa Kibaha na bahati nzuri Mheshimwa Waziri Mkuu, alipokuja kutembelea Kibaha aliuliza Mji uko wapi, mbona naona mapori? Alisema hivyo! Kwa kauli ile, alithibitisha kwamba Ahadi ya Rais haijatekelezwa na Tamko la Waziri wa Ardhi pia halijatekelezwa. Kwa kauli ya Waziri Mkuu na kweli alipita akakuta mapori, barabara tulizitengeneza tu ili Waziri Mkuu apite, lakini ni pori, ijapokuwa unaitwa Mji.

Sasa mimi naomba tusaidiane, najua Serikali haina pesa, lakini ina nia. Sasa mimi naomba nishauri, tayari kwa kupitia Mheshimiwa Mbunge wao na kwa kushauriana na Mkurugenzi na Madiwani, tumeandaa mkakati. Mkakati huo ni huu hapa, ili basi kauli ya Rais, maana usitegemee Rais akishasema yeye ndiye atatoa hela mfukoni, atatoa wataalamu, tuanze kumsaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkakati huu nimeupeleka TAMISEMI, wamekiri ni mzuri, bahati mbaya hawana fedha. Mkakati huu nimeupeleka Wizara ya Ardhi kwa kupitia Ofisi ya Naibu Waziri, sijapata jibu mpaka leo. Lakini watu wanaendelea kujenga kiholela, kwa hiyo, ile dhamira nzuri ya kuandaa Mji wa Kibaha uwe Mji unaokubalika wa kisasa, inaanza kupungua. Naomba Waziri kwa kushirikiana na TAMISEMI, kushirikiana na Waziri ambaye ameuona huo Mji, ingawa unaitwa Mji, lakini mapori, basi tutekeleze Ahadi ya Rais, asionekane Rais wetu si mkweli. Hilo ni ombi mojawapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachonisikitisha Maafisa Ardhi na Maafisa Mipango Miji, yaani hawana ule mwamko wa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya, hawana! Ingawa tunawasaidia kuwapa ushauri, lakini wao wenyewe wamelala. Sasa mimi ningeomba kabisa, kwa mfano, Kibaha, tumebembeleza watu wa *PPF* wamekubali wapewe eneo la kujenga nyumba nafuu kama 100. Wanangojea Mheshimiwa Mbunge ndiye ahangaike, wao wenyewe wamekaa hawafuatilii *PPF*. Watu wa *VETA* wameomba eneo, wamepewa kwa nia hiyo hiyo ya kuendeleza Mji. Lakini matokeo wao badala ya kuwafuata *VETA* ambao wameonesha nia, wamekaa, wanataka Mheshimiwa Mbunge ndiye aende. Watu wa *NSSF* walikubali, wako tayari kutukopesha pesa tutazolipa kwa miaka kumi, lakini Maafisa wale wamekaa, wanangojea Mheshimiwa Mbunge ndiye akamwone Ndugu Ramadhani Dau, inakatisha tamaa! Hii ni nia nzuri kwamba tumepata watu watakaotusaidia kuendeleza Mji, lakini Maafisa Ardhi wamekaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mipango ya mwaka huu, Wizara ina mpango mzuri wa matumizi ya ardhi ambao utafanywa Kitaifa, Kiwilaya na Vijiji. Basi mimi naomba mkakati huo usiache Kibaha, maana Kibaha hakuna mkakati wowote unaofanywa. Ninajiita tu Mbunge wa Kibaha Mjini, lakini ukienda ni mapori kama alivyoona Waziri Mkuu. Inasikitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kibaha ni eneo *strategic*. Tunapotaka kuandaa viwanja kwa ajili ya kujenga nyumba. ambao ni mpango wa Wizara, wamesema watajenga nyumba kuhakikisha Miji ambayo ukijenga nyumba kunakuwa na soko la uhakika. Kibaha sehemu ilipo ni mahali pazuri. Kwanza ni karibu na Dar es Salaam. Sasa hivi, robo tatu ya wafanyakazi wa Mkoa, wa Kibaha Mjini, wa Halmashauri, pia Halmashauri iko Kibaha Mjini, wanakaa Dar es Salaam. Kwa hiyo, inaonekana wakijengewa nyumba, badala ya kukaa Dar es Salaam, watakaa huku. Bado kuna watu wanafanya kazi Dar es Salaam, wanakaa Kibaha. Lakini Kibaha iko katika barabara ambayo inakwenda Bara katika Miji mbalimbali ya Tanzania na nje ya nchi.

Kwa hiyo, zikijengwa nyumba pale, patakuwa mahali pazuri. Bado katika mpango kama nakumbuka Mheshimiwa John P. Magufuli, wakati akiwa Wizara ya Ujenzi, alisema pale eneo la *Road Reserve* kunawezekana kukafanywa *Dry Port*. Sasa kukifanywa *Dry Port*, maana yake magari yatakuwa mengi na watu watakuwa wengi na eneo hilo litakuwa lina soko. Kwa hiyo, mimi ninaomba, basi kwa utaratibu huu, waisaidie Kibaha iwe Mji wa Kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Charles Keenja, kazungumzia mambo ya kuendeleza miji siyo kama ilivyokuwa inaendelezwa Dar es Salaam. Dar es Salaam kila kitu kilikuwa mjini, siku hizi mnaita Ilala, lakini sisi tuliozaliwa kule tunaita mjini. Kwa hiyo, huduma zote tulikuwa tunazipata kule. Ukitaka nini, unapata mjini, ukitaka hiki unapata mjini na hata sisi wa Kibaha tunasema tunakwenda mjini. Mimi ninasema tundeleze, kwa mfano, Kibaha ina Kata nane, basi kila Kata iwe na huduma. Ikiwa huduma ya soko iko Kata hii, huduma ya hospitali iko Kata hii, watu watajitegemea na Mji utaendelea. Kwa hiyo, mimi hilo ninaomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini, kwa sababu Serikali haina pesa, kwa nini tusiwape watu binafsi pia watusaidie katika kupanga Mji wetu? Kwa mfano, mimi nimezaliwa Ilala, lakini Bungoni ilikuwa ni eneo la mtu alikuwa Mhindi anaitwa Daya. Daya alipoamua kuuza eneo lake, alichokifanya alipanga viwanja, barabara, akawauzia watu viwanja. Kwa hiyo, Bungoni haikuanza kama *Shunt Town* na nashukuru mimi nilikuwa karibu na Bungoni, maana Bungoni wakati huo ilikuwa sehemu za miembe tu, tulikuwa tunakwenda kuokota embe. Kwa hiyo, Daya akasababisha Mji wa Bungoni uwe na mitaa na viwanja vipangwe kwa utaratibu. Kwa nini tusitumie watu binafsi kama ni wa ndani au wa nje kwa Mji wa Kibaha? Hilo ninaomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mipango ya Wizara, inasema hivi, watatoa elimu kwa wananchi kuhusu suala zima la sera na sheria. Mimi naomba waanze kutoa elimu kwa Maafisa Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalizungumza hili kwa uchungu, Maafisa Ardhi wangu sheria hawaijui na nasema sheria hawaijui, sitaki kuingia kwenye rushwa. Kwa mfano, kuna mtu anaitwa Mzee Rajab, kachukua eneo ambalo liliwekwa kwa ajili ya viwanda. Kachukua eneo lile, kaanza kujenga nyumba. Wamempa *notice* asiendelee kujenga, kaendeleea. Wamempa *notice* asiendelee kujenga, mpaka kamaliza nyumba na sasa hivi yumo ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoka hapo, akauza eneo karibu yake akamuuzia Daktari mmoja kutoka Muhimbili, bila amri ya Halmashauri. Wakatoa *notice*, usijenge, yule kaendelea, usijenge, kaendelea. Wakaweka alama, yeye akafuta ile alama yao, hawajafanya lolote. Akaendelea sasa hivi nyumba imemalizika na ninategemea atakaa. Je, sheria inasema nini?

Niliona Dar es Salaam, Kinondoni walivunja maghorofa, walitoa *notice*, lakini matokeo wakamwambia avunje kwa gharama yake, hakuvunja, wakavunja kwa gharama ya Halmashauri. Je, kwa nini Halmashauri ya Kibaha wanamchezea huyu mtu na yeye anasema hawawezi kunivunjia kwa sababu Maafisa Ardhi wananufaika kwake. Ukiwafuata Maafisa Ardhi na kuuliza kitu gani mnanufaika kwa huyu Mzee Rajab, wanasema sisi hatunufaiki, tunaogopa Mzee yule mchawi. Jamani, wataalamu tunazungumzia uchawi au wanaongopa? Wanasema tunamuogopa kwa sasabu ni mtu wa CCM. CCM haina maneno hayo!

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama mtu wa rushwa, ninaweka *query*. Inawezekana kuna rushwa. Sasa, namwomba Waziri akishirikiana na TAMISEMI na Waziri Mkuu pia, waende wakamwulize kitu gani wanapata kwa huyu Mzee?

Nimesema mwisho mimi ninaonekana *I am interested* na hilo eneo. Hapana, sheria iko, wala hajaomba kibali cha kujenga kwa sababu ni Mji, anajenga na ameanza kuuza viwanja vingi. Huyu Mzee hachukuliwi hatua. Ukiwaambia, tunamwogopa mchawi. Imeandikwa hata katika magazeti, jamani, sasa hivi tutakuwa hatufanyi kazi kwa kuogopa uchawi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimekwenda nikamwambia Mzee Rajab niroge, lakini utahakikisha unavunjiwa hapa, sijarogwa mpaka leo kwa sababu Mungu yupo. Ukikaa, ukisali na kumwomba Mungu, uchawi, hakuna. Sasa mimi naomba niulize kuna nini na kulikoni? Naomba hili lichukuliwe *serious.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nisipoteze muda wa kugongewa kengele ya pili, lakini nisingependa kabisa kuinuka katika mshahara wa Waziri. Naomba anijibu ahadi yake aliyoisema mwaka jana kwamba, Ahadi ya Rais ni amri kwa Serikali.

Je, amefanya nini kuhusu Kibaha? Hilo naomba nilisisitize, sisi wengine tunachoka, tumekuwa watendaji na mimi kama hana huu Mpango nitamkabidhi kusudi asiseme hapana hatujapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, naunga mkono hoja ya Wizara hii kwa asilimia mia kwa mia. Asante. *(Makofi)*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nami awali ya yote nitoe shukurani na pongezi kwa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana wa Wizara hii pamoja na Naibu wake, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii. Nawapongeza kwa maandalizi mazuri na kwa mikakati mizuri waliyoipanga kwa kipindi kinachokuja kwa mwaka huu cha mwaka wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaingia kuzungumzia masuala muhimu ambayo nitazungumzia sana yanaliyohusu jimbo langu la uchaguzi la Iramba Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ningeomba kitu kimoja kwanza, sisi Wabunge tunaposimama hapa na tukawa tunasema baadhi ya maneno ambayo tunaamini ndiyo maneno yanayotokana na maeneo yetu katika majibu yetu naomba sana kwamba kunakuwa na tabia moja ambayo tunajibiwa tunaambiwa kwamba hili halituhusu, linahusu TAMISEMI, linahusu Halmashauri zetu. Sasa tunafahamu na tunajua majukumu ya Halmashauri katika maeneo yetu. Lakini tunapokuja hapa ni mahali ambapo tunazungumzia Serikali Kuu. Wizara zote zinahusiana na masuala katika maeneo yetu. Kwa hiyo, tunaposema kuhusiana na maeneo yetu tusije tukaambiwa hili Mheshimiwa Mbunge tunashauri aende awasiliane na Halmashauri yake ili waliweke sawa. Ujue kwamba kule tutakuwa tumeshindwa na ndiyo maana tunakuja hapa tunasema. Tunasema hapa ili tupate ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hilo sasa mimi nizungumzie kuhusiana na hali inayojionyesha kuhusiana na migogoro ya ardhi pamoja na ujenzi holela. Nchi yetu kwa ujumla hususan vijijini maeneo mbalimbali, maendeleo ya ujenzi/maendeleo ya uhitaji wa ardhi yanakuwa makubwa sana kutokana na ongezeko la watu. Kila siku wananchi utakuta kwamba kunatokea mtu anakuwa anahitaji ardhi na inahitaji kwa ajili ya matumizi ya kilimo au anahitaji kwa ajili ya matumizi ya ujenzi. Hakuna eneo lolote ambalo mwananchi wa kawaida wa kada ya chini anachotegemea ni anategemea kupitia ardhi. Ardhi ndiyo msingi maalum na ndiyo pekee ambao unaweza ukamkomboa mwananchi aliye ngazi ya chini.

Ardhi, sasa hivi kuna taratibu mbalimbali ambazo tunapitisha katika Bunge hili lakini tunapitisha haya maeneo tunayopitisha ni kwa kiwango gani wananchi wetu wanafahamu kule majimboni? Kule vijijini wananchi wanafahamu hayo mabadiliko ya Sheria kwa kiwango kipi? Kwa hiyo, muda wote utakuta kwamba yule mwananchi asiye na ufahamu pale panapofanyika mabadiliko hakuna elimu ya msingi, matokeo yake unakuja kukuta kwamba yule mtu anakuja kuonekana hana uhalali na ile ardhi na matokeo yake ananyang'anywa na matokeo anabakia anahangaika kutafuta ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningeomba sana Wizara hii pamoja mambo mengine naomba kwamba jambo moja lililo kubwa wala hakuna sababu ya kujibiwa usemi wa kwamba hili kule kuna TAMISEMI. Halmashauri inapokea watalaamu kutoka kwenye Wizara mbalimbali. Sasa kama TAMISEMI inapokea watalaamu kutoka Wizara mbalimbali kazi yenu kubwa ni kuhakikisha kwamba wale watendaji mnaopeleka wale watalaamu kwamba wanafanyakazi kwa kiwango gani. Elimu hakuna vijijini na matokeo yake wananchi wetu tunasema kwamba tunahitaji waondoe umaskini lakini wataendelea kuwa maskini kama hatutawaelimisha na kama hawatajipanga kwa ajili ya kuweza kumilikishwa hizi ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tunakwenda kwenye Afrika Mashariki na tunakwenda kwenye Shirikisho lakini tuna tatizo kubwa kwamba tukiingia kwenye Shirikisho kwa staili hii tunayokwenda naamini wananchi wetu watakuwa hawana kitu na kwamba ardhi yote itakwenda na wajanja na watabakia hohehahe maskini ambao hawana kitu. Kwa hiyo, naomba sana tuandae wananchi wetu, tuandae vizuri na ni jukumu la Wizara hii ndiyo kazi yake, Wizara ina Waziri na Naibu Waziri na ina watendaji na tunapitisha leo fedha kwa ajili ya kufanyia kazi wananchi wetu ambao wako vijijini.

Kwa hiyo, naomba sana tunapokwenda katika mambo haya tunayozungumzia tunahitaji umakini wa kuandaa wananchi wetu kuhusiana na elimu. Kwetu Iramba inashangaza naweza nikazungumza sisi tayari migogoro ipo ya ardhi. Sasa tumeanza kupata migogoro, mwanzoni ilikuwa hakuna migogoro kwa sababu eneo lote lilikuwa liko wazi. Juzi nilizungumza nilipokuwa nachangia Wizara ya Mifugo, tayari ipo migogoro mikubwa ya ardhi kuhusiana na mashamba na ujenzi katika maeneo kadha wa kadha katika jimbo langu. Nani wa kutatua, tunaambiwa Halmashauri. Lakini Halmashauri pamoja na kuunda baraza hilo la Halmashauri inaonekana Halmashauri yenyewe ndiyo inakuwa kama mgogoro wa kuweza kuchochea zaidi ili wananchi waweze kugombania hiyo ardhi. Kwa hiyo, kutokana na kutokuwa na elimu sasa tunahitaji hiyo elimu itolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi nimesema ni msingi wa maendeleo hasa kuweza kumuondolea umaskini mwananchi wa kawaida. Ipo mikakati mingi ambayo Serikali ya Awamu ya Tatu na Awamu ya Nne na tunaendelea nayo ambayo kimsingi imepitishwa na kwamba pengine kwa kutumia ardhi, huyu mwananchi anaweza kuondokana na huu umaskini. Lakini kasi ya hii mikakati tunasema MKURABITA, huu MKURABITA ni wananchi wangapi wanaoufahamu huko vijijini? Kwa hiyo, MKURABITA unakwenda matokeo yake sasa hivi tutaondoka kwenye MKURABITA tutafuta mkakati mwingine

bila ya huo MKURABITA kufanyakazi na ukawa umeonyesha kwamba wananchi wanaweza sasa kukombolewa na huu mkakati. Kwa hiyo, naomba hii mikakati tunayokuwa nayo kwamba ifanye kazi kwa umakini ili wananchi waweze kurekebisha hali zao kimaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia kuhusiana maeneo ya miji midogo. Mimi jimboni kwangu nina maeneo ambayo yamepitishwa kwa kipindi sasa ya miji midogo. Mji mdogo wa Shelui, mji mdogo wa Kiomboi, mji mdogo wa Misigili, mji mdogo wa Kinampanda na mji mdogo mwingine ambao upo katika Iguguno ambapo pamoja na mji huu kuwa upo Iramba Mashariki, lakini kasi iko vipi ya kuwapimia wananchi wa pale viwanja? Ujenzi unaendelea na leo tunaambiwa hizi sehemu zote ni miji midogo, wananchi bado wanaendelea kujenga. Sasa hii ni lazima italeta mgogoro baadaye kwa sababu itafika wakati tutakuja kuwabomolea wananchi nyumba, tukiwabomolea ndiyo wanapotaka kudai fidia tunasema kwamba wewe nyumba yako haikuwa *planned* kwa hiyo hutalipwa kitu chochote kwa hiyo nakuondolea hiki kiwanja na wala hustahili.

Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri, niliwahi kukupigia simu siku moja na nikakueleza kuhusiana na matatizo, ukaniambia oh, mimi Mheshimiwa Killimbah nina watu wengi zaidi ya watu milioni 36 siwezi kuweza kushughulikia wote, hii ni kazi yako Mheshimiwa Waziri wala huwezi kujivua naomba wananchi wale ile miji midogo muwapimie. Wapimieni hivyo viwanja ili tuepusha hiyo migogoro. Sasa hata hii migogoro suala la ardhi ambalo limetolewa bure na Mwenyezi Mungu, sawa tunasema ardhi ni ya Serikali, lakini sasa huyu mtu amekaa pale kwa muda mrefu na yuko na ardhi pale kwa muda mrefu na yuko pale na hiyo ardhi ndiyo amekuwa akiitumia kwa muda wote. Sasa inakuwaje ugumu unatoka wapi, vitendea kazi mnasema hakuna. Sasa hivi vitendea kazi kama hakuna mimi nashindwa kuelewa kwamba mwaka jana tumeambiwa hakuna vitendea kazi na mwaka huu mnasema hakuna vitendea kazi. Sasa ni lini hii itafikia kwamba hatua hii tukamilishe? Tusiwavike wananchi vilembe vya ukoka tukiamini kwamba tunapoambiwa basi tayari wataendelea haitakuwa na tatizo, lakini wahakikisheni wapate haki yao na wao wapimiwe hivyo viwanja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia hiki kitabu tena bahati nzuri kuna hiki kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri na vile vile mkatuwekea hii orodha ya vijiji vilivyopimwa, mipaka na vinavyotayarishiwa mpango wa matumizi bora ya ardhi mwaka 2006/2007 na amejaribu ku-*highlight* ameweka katika hizo Wilaya mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Wilaya ya Iramba, mimi kama Mjumbe wa Baraza la Halmashauri tunayo maombi ambayo yako Wizarani kwa muda. Maombi ambayo tunaomba baadhi ya vijiji vipimwe kwa nia ya kuondoa migogoro tu kwa mfano kuna kijiji kinaitwa Luzilukulu. Kijiji hiki cha Luzilukulu kinapakana na magereza ya Ushora, pale pamekuwa na migogoro ya muda mrefu kati ya Magereza na kile kijiji.

Sasa kile kijiji ni kitongoji ambacho kinatokana na kijiji cha Songambele, tulikuwa tumeomba kwa sababu ya ukubwa wa eneo na tukaomba sasa wale watu wa Luzilukulu nao wapewe ili kitongoji wapimiwe na kiwe kijiji. Lakini hadi hivi sasa nasema kwamba maombi yako kule, yako muda mrefu lakini naamini mpaka sasa hiki

kijiji hakijapimwa. Lakini kipo kijiji kingine hiki cha *Msasawo Two* tunakiita kwa sababu ipo *Msansao One* ambacho kipo Kata ya Mtoa na *Msansao Two* ipo Kata ya Shelui, nacho tumeomba lakini hamna, si kwamba hamna kwa Wilaya ya Iramba tu pamoja na Singida yenyewe haipo.

Sasa naomba sana kwa jimbo langu mimi nasema hata hivi vijiji vinne ambavyo tumeomba basi naomba na hizo hela sijui utaniambia hazipo kwamba hata hivi vinne tu unipatie hivi vya Msansao na Luzilukulu. Vikiwezekana hivi kwa sababu kumekuwa na ukubwa wa eneo wananchi kupata huduma ya kawaida kwa sababu ukiweza kumtafuta Mwenyekiti wa Serikali ya kijiji, ukiweza kutoka kwa mfano Luzilukulu unakwenda kumpata Mwenyekiti ya Serikali ya Kijiji Songambele, ni eneo la mbali sana. Sasa naomba katika hili Mheshimiwa Waziri wakati akijibu na naomba aniambie hatma ya hili pamoja na kwamba ametutengenezea jedwali zuri ambalo linaonekana kwamba ndiyo la vijiji ambavyo vimeshapimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nizungumzie juu ya Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi wa Wilaya. Mimi nimezungumza hapa migogoro iliyopo ndani ya jimbo langu na Wilaya nzima ya Iramba. Lakini tatizo lingine tulilonalo pamoja na kuwa tumetoa ofisi kwa ajili ya kuwapo Mwenyekiti wa kuamua hii migogoro ya ardhi hatujawa na huyo mtu wa aina hiyo. Kwa hiyo, huyu mtu anafanyakazi kutoka Singida na anakuja mara mbili au mara moja kwa miezi mitatu. Sasa utakuta mrundikano wa kesi ni nyingi sana na huyu hafanyikazi pale Singida tu, anatoka Singida na anakwenda Manyoni. Tuna Kata 88 kwa Mkoa wa Singida sasa ndani ya kata hizi 88 na migogoro iliyopo inawezekana ukakuta kwamba kesi ya miaka ya nyuma kabisa isisikilizwe kutokana na ukosefu wa Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi. Kwa hiyo, naomba sana wakati Waziri akitoa majibu ili tuhakikishiwe kwamba ili tumpate huyu Mwenyekiti, awepo pale Makao Makuu ya Wilaya ya Kiomboi pale na afanye kazi zake zote kwa muda wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nisingependa nigongewe kengele lakini nimezungumzia haya na ninaamini Waziri kasikia, Waziri Mkuu kasikia na Mawaziri wote mmesikia kwa sababu Serikali inafanyakazi kama timu moja, tusaidieni hasa watu wa Singida tusaidieni katika matatizo haya ni aibu kila mara tunapozungumza unakuta kwamba tunaangalia tunazungumza matatizo Singida. Singida tukienda kwenye maji, tuna matatizo, ukienda kilimo matatizo, ukienda wapi matatizo. Tunaomba sana mtusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabla ya yote ningependa nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa baraka zake kwangu ambazo zimeniwezesha kusisimama hapa mbele yenu siku ya leo. Pia kwa namna ya peke namshukuru sana Waziri wangu Mheshimiwa John Magufuli, Katibu Mkuu Mama Salome Sijaona na watendaji wote wa Wizara ya Ardhi

walionisaidia sana katika kufanyakazi yangu na nadhani sasa nina hitimu sawa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa si mwingi wa fadhila kama sitawashukuru familia yangu kwa kunivumilia na kunipa moyo katika kufanya kazi hii, mume wangu mpenzi Tofulo Mlaki, watoto wangu Nambua, Mcharo na Lawrence ambao wapo siku hii ya leo. Kwa uzito kabisa napenda niwashukuru wananchi wa Jimbo la Kawe ambao wamenivumilia kwa kiasi kikubwa na kunisaidia sana katika kuleta maendeleo katika jimbo la Kawe. Nina waahidi sasa miaka miwili imepita, nitakuwa tayari kuwaonyesha tumefanya nini kwa kipindi cha miaka miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni muda mfupi nitaomba nitumie muda huu sasa kujibu hoja chache za Wabunge kama ifuatavyo:-

Kwanza naomba kusema ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nitaanza na hoja zinazohusu Mabaraza ya Ardhi. Ameongelea msemaji wa mwisho Mheshimiwa Juma Killimbah wa Iramba Magharibi pamoja na Mheshimiwa Savelina Mwijage na Mheshimiwa John Cheyo. Labda niseme kwa ufupi kuwa tumeunda Mabaraza ya Ardhi 33 nchi nzima. Haya mabaraza yanapaswa kuwa Mabaraza ya Wilaya, lakini kwa sasa yapo Makao Makuu ya Mkoa. Tumeanza katika kila Mkoa na hii ni kutokana na rasilimali ambayo tunayo kifedha. Mkakati wa Wizara yetu ni kuhakikisha kwamba kila Wilaya inapata baraza lake, kila kata na kila kijiji. Tunashirikiana na TAMISEMI japo msemaji aliyemaliza amesema tusiwaambie TAMISEMI, lakini Serikali ni moja, sisi tunafuata sheria ambayo tumeitunga halafu tunawasiliana na TAMISEMI kushirikiana nao waweze kuanzisha Mabaraza katika ngazi za vijiji pamoja na ngazi za kata ili mashauri mengi yasifike Wilayani. Mabaraza 33 yapo katika kila Mkoa kuacha Mkoa wa Dar es Salaam ambao una mabaraza kila Wilaya kwa sababu ya wingi wa watu na wingi na wingi wa matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoahidi tutaendelea kuunda na ninatamka kabisa kwamba shughuli hii Mheshimiwa Waziri amenikabidhi niifanye, nimetoa juzi tangazo na tutakwenda katika Mikoa mbalimbali kutazama maeneo hayo ya kata kwa kushirikiana na TAMISEMI pamoja na vijiji na kuhakikisha tumeweza kuyaunda. Tatizo la mabaraza limekuwa sugu, wanalalamika sana kwa sababu ya kesi nyingi na ndiyo sababu naona hapa Mheshimiwa Juma Killimbah ameongelea kabisa kwamba wamekwishatoa mpaka na jengo la kuanzisha Baraza hili. Tunawaomba Wakuu wa Wilaya na Halmashauri husika za nchi nzima waanze kututafutia majengo kwa sababu tatizo kubwa ni majengo. Kujenga jengo jipya ni milioni 75, kukarabati milioni 35. Lakini naomba nimhakikishie Mheshimiwa Juma Killimbah, kwamba kwa kuwa amekwishatupa jengo tutaendelea kuendelea kuunda sasa Wilaya mbalimbali tutaanza na Wilaya yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Savelina Mwijage ameongelea kuhusu rushwa katika mabaraza haya ni jambo la kusikitisha kwa sababu rushwa inapoingia kwenye haki inaumiza watu. Sisi tunamuomba Mheshimiwa Savelina Mwijage, atupatie ili tuweze kushirikiana na TUKUKURU ya pale Kagera kuhakikisha tumeweza

kuwakamata hawa na tutawatoa kwa sababu Mwenyekiti tunamchagua sisi kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Cheyo naye ameongelea hilo hilo na ameomba sana mabaraza yaundwe kutokana na matatizo ambayo yanakabili katika vijiji. Haya mabaraza ya vijiji siwezi kudiriki kutamka kwamba tuyarudishie Halmashauri ambayo Wabunge nyie ni wajumbe katika hizi Halmashauri, lakini nitawaomba sana tushirikiane basi kwa pamoja na kwa vile nimeahidi kuja katika majimbo yenu tuone jinsi ya kuyaunda, Mwenyekiti anachaguliwa pale pale katika ngazi ya Halmashauri, wajumbe wanachaguliwa na mkutano wa kijiji, kwa hakika tukishirikiana wote tutaweza kuhakikisha kwamba tatizo hili tumeliondoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Juma Killimbah bado umezidi kutushauri vizuri sana kuhusiana na sheria ya ardhi ambayo umekiri kabisa kwamba haifahamiki na umeomba tutoe elimu ili watu wazijue. Ni kweli kabisa na sisi tangu mwaka 2001 tumekuwa tukifanya jitihada ya kutoa elimu ya sheria hizo kuwafikia wananchi wengi kadri iwezekanavyo na tumekuwa tukitoa kwa njia mbalimbali kutumia magazeti, kutumia redio, kutumia *TV* na mikutano mbalimbali tutaendelea kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Felix Kijiko, ambaye ni Mbunge wa Muhambwe, kwanza ametupongeza, nashukuru sana vijiji ambavyo tumevipima katika Mkoa wa Kigoma. Isipokuwa amekuwa na wasiwasi kwamba kuna wageni kwa sababu eneo la Kigoma, Kibondo wanapakana na Burundi. Sasa kuna wananchi wengi pale wanakwenda kuvamia na kuchukua viwanja ambao si wananchi, hiyo, siyo sahihi. Tutamuomba ashirikiane na Halmashauri kusimamia matumizi ya ardhi katika maeneo yao na kuhakikisha kabisa kwamba anayepewa ardhi ni mwananchi na siyo hao wageni. Vile vile vijiji ambavyo umeomba kuhalalisha na ambavyo vina masoko tutahakikisha kwamba tumewasiliana na mamlaka husika ili viweze kuhalalishwa na kupimwa kwa sababu zoezi linalofuata sasa hivi katika mwaka wa fedha tutaendelea kupima vijiji katika maeneo yanayofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika dakika saba zilizobaki ningeomba nimjibu Mheshimiwa Charles Keenja, Mbunge wa Ubungo. Mheshimiwa Charles Keenja amewatetea sana wananchi wa kipato cha chini waweze kupata viwanja kwa sababu viwanja vyetu sisi tunavyovipima Wizarani vinauzwa vya *high density* kuanzia laki saba, laki nane, lakini tisa mpaka milioni nne inategemea na ujazo wa kiwanja kile au ukubwa wa ardhi. Mimi naomba kumfafanulia Mheshimiwa Mbunge kwamba hizi ni gharama za kupima kile kiwanja kuna fidia tunalipa, kuna barabara ambazo tunaweka na uendeshaji kwa ujumla. Kwa hakika ni asilimia 80 tu ambazo tunatoza ya gharama ya kile kiwanja. Hii inamwezesha mtu hata wa kipato cha chini kuweza kununua kwa sababu wengi wao wa kipato cha chini ni wale waliopo katika yale maeneo ambao wanalipwa fidia.

Kwa hiyo, analipwa fidia pale mwingine analipwa milioni tano, milioni kumi, milioni kumi tano inategemea na ukubwa wa shamba lake ambalo tumelichukua. Kwa maana hiyo anaweza akanunua viwanja, kwanza tunampa kimoja bure vingine tunamwambia avinunue kwa fedha ile aliyopata. Mimi naona Mheshimiwa Charles

Keenja kwa sababu pia mimi ni Mbunge wa Dar es Salaam ningeomba tushirikiane, tutazame kwa makini naye ni mwelewe mzuri sana kwa sababu ameifanya hii kazi si chini ya miaka kumi. Mitatu akiwa Tume ya Jiji ya Dar es Saalam. Tunaweza tukaelewana tukatazama na tukawaeleza wananchi na wakatuelewa. Kuhusiana na viwanja ambavyo vimepimwa naona umetushauri vizuri kwamba tuendelee kupima.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunaona hapo anapoelezea kwamba viwanja vinacheleweshwa kupimwa na wale wanaohusika ili wapime vichache na waweze kuviuza kwa bei ya juu. Mimi hapo naomba kusema siyo sahihi, kwa sababu kupima kiwanja kuna gharama zake na Mheshimiwa Charles Keenja amefanya hii kazi na anajua ugumu wake na gharama ambazo zinahitajika. Kwa hiyo, kwa hakika ni ufinyu wa fedha tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wabunge watupongeze Wizara katika kipindi cha miaka mitatu na nusu tumepima viwanja zaidi ya 49,000 kulinganisha na tangu tumepata Uhuru katika nchi hii. Tutaendelea kupima na tumechukua hilo jukumu kwa kuchukua mkopo kutoka hazina shilingi bilioni 8.9 ambazo tukishapima tunauza vile viwanja inakuwa kama ni mfuko unaozunguka na tunawapa pia Mikoa mbalimbali kama Mwanza, Morogoro, Mbeya na bado wengine Wilaya mbalimbali ambazo tumezikopesha tunaotegemea warudishe mikopo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kujibu swali la Mheshimiwa Charles Keenja au kutoa ushauri kuhusiana na mpaka wa Wilaya ya Kinondoni na Kisarawe. Naomba nikiri hapa kwa sababu mimi ni *interest part* na nimekuwa *interested part* kwa muda mrefu. Kwa mara ya kwanza nilipokuwa Wilaya ya Kinondoni ule mpaka nilipenda sana uminywe Wilaya ya Kisarawe ili Wilaya yangu iwe kubwa. Bahati mbaya nikahamia Wilaya ya Kibaha nikataka mpaka uminywe Wilaya ya Kinondoni ili Kibaha iwe kubwa. Kwa hiyo, mimi ningeomba hapa tusiangalie *interest* za watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Athumani Janguo alikuwa anaongelea akilalamikia mpaka, Wizara tulipoweka mpaka akafurahi sasa Mheshimiwa Charles Keenja analalamika. Tutazama sheria inasema namna gain, tutaongea na mawakili au wanasheria wa Wizara pamoja na Halmashauri tutatue tatizo hili tukiwa pamoja na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa nitapenda kuongelea suala la Mheshimiwa Abbas Mtemvu kuhusiana na fidia ya kule Kurasini. Sisi tumepima viwanja kule Kurasini na tukafidia nyumba 54 kwa shilingi milioni 956 mpaka sasa na wengine wanaendelea kulipwa kwa awamu. Wananchi wanaliofanyiwa tathimini walikuja mpaka Dodoma wiki mbili zilizopita, tumekaa nao na tumewajibu kabisa kwamba tukishauza sasa hivi ambapo tumevipima ndipo tutaanza kulipa fidia ambayo tunakadiria mwezi wa Septemba au mwezi Oktoba. Nitamwomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kuvuta subira, tutashirikiana tuweze kuwalipa hao watu ili wapangaji wao waweze kupata imani na kujua kwamba wenye nyumba wajue kwamba sasa wanaondoka na kwenda mahali pengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tatizo la eneo la *DDC* pale Keko kuwa limetolewa kwa *GAPCO* naomba kusema kwamba Halmashauri wanayo mamlaka kabisa ya kugawa ardhi na kuandaa hati kwa maana hiyo ningeomba Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na Halmashauri ya Wilaya ya Temeke kufuatilia hili suala wao ndiyo wanaopima wanatuletea sisi pale baada ya kutengeneza hati, kamishna anaisaini na baadaye tunaisajili. Kwa hiyo, suala zima siyo Wizara inagawa, ni Serikali ya pale pale ya mitaa ambayo ni ya Halmashauri ya Temeke. *(Makofi)*

Kuhusu la mwisho kabisa kwamba Wizara tusimamie utekelezaji na tunaendelea kugawa viwanja, jamani tumefanya kama mfano baada ya kutangaza katika sera kwamba Halmashauri zipime viwanja lakini tukaona bado hawana uwezo tukaamua tukope fedha sisi kama Wizara tukapima viwanja vya kwanza 20,000 tukavigawa na kuviuza ili Halmashauri zifuate mfano wetu, ilikuwa *pilot project* na tumeendelea namna hiyo na hatimaye Mikoa mingine imefuata na tumewapatia fedha. Sasa tunasema mikoa mingine pia iendelee kuiga huu mfano, siyo kwamba Wizara tumechukua ile kazi ya kugawa viwanja sisi bado tunafanya sera tunafanya *pilot project* halafu tunawapa mikoa mingine ifuatilie.

Kwa hiyo, hili, tusingeweza kupewa viwanja 20,000 tuwape mvigawe kabla hatujawaelekeza mtavigawa namna gani, mtaviuza namna gani. Kwa hiyo, ningemuomba Mheshimiwa Mbunge, japo alisema mwanzo kwamba tunakubaliana Wabunge wa Dar es Salaam na mimi nikiwemo, mimi naomba kusema nitawaelewesha wenzangu katika hili na kwamba hatuna wasiwasi kabisa Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam tutashirikiana na tutahakikisha kwamba maeneo yamepimwa zaidi. Tunaishukuru Wizara nikiwemo ndani kwamba pale *project* imefanyika Dar es Salaam tukapata viwanja vingi. Kwa hiyo, tutaendelea kufanya namna hiyo nikiwa kama Naibu Waziri katika Wizara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu baada ya kusema hayo naona muda wangu umekwisha, ningeomba nimalizie suala la Mheshimiwa Kabwe Zitto, ambaye ameuliza *TIC* kwa nini imeficha mambo ya *Land Bank. TIC* haijaficha, yapo wazi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kuna maeneo kadhaa ambayo *TIC* wanayo, mwekezaji akija anapewa *grant of right of occupancy* anaweza akaanza kujenga ama anaweza akatumia eneo hilo kwa viwanda na mambo mengineyo. Kwa hiyo, hakuna wasiwasi kutokana na hilo na vile vile anasikitika kwamba wawekezaji wanachukua ardhi kubwa kwa hila bila kufuata utaratibu. Mfano wa Rufiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kiwango kwa kijiji wanaruhusiwa kutoa ambazo ni ekari 250 zaidi ya hapo zinakuja kwa Kamishna na ndiyo sababu wengi wanalalamika kwamba wanacheleweshwa kuwapa wawekezaji. Hatuwezi kuwaruhusu vijiji wagawe ardhi zaidi ya kile waliopangiwa kisheria. Kwa hiyo, naomba kumfahamisha Mheshimiwa Kabwe Zitto kwamba Wizara tuko macho na tunadhibiti sana maeneo ambayo yanagawa zaidi ya ekari 250 na hakuna eneo tutakaloliruhusu lichukuliwe na wawekezaji bila kufika kwanza Wizara ya Ardhi ili tuwasiliane na *TIC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua nina dakika 45 tu ingawa hoja ni nyingi sana. Waliochangia kwa kusema ni Waheshimiwa Wabunge 12 na waliochangia kwa maandishi ni 58. Sasa kwa dakika hizo 45 ukijibu hata kwa dakika moja moja kila moja maana yake hazitoshi. Lakini hata hivyo nitajitahidi kwa kujibu kwa haraka haraka halafu wale waliochangia kwa maandishi tutawajibu baadaye katika *document* ambayo tunaweza tukaitawanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwatambua tu wale waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni ambao ni Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Felix Mrema, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Abbas Mtemvu, Mheshimiwa Ephraim Madeje, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Juma Killimbah pamoja Mheshimiwa Rita Mlaki, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. *(Makofi)*

Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Yono Kevela, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Masoud Salim, Mheshimiwa Dr. Omari Nibuka, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Mussa Zungu, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Mgana Msindai na Mheshimiwa Aziza Ally. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Ephraim Madeje, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Eng. Laus Mhina, Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Felista Bura, Mheshimiwa Thomas Mwang'onda, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Zaynab Vulu, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa Ezekiel Maige. Jumla ni 58 waliochangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri wangu kwa kunisaidia sana katika kutoa michango ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge hapa. Lakini pia napenda niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla kama mjadala ulivyoenda, Waheshimiwa Wabunge wengi wameipongeza sana Wizara ya Ardhi kwa kazi nzuri inazof anya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ulivyoona hata ndugu yangu Mheshimiwa John Cheyo amepongeza na kuunga mkono hoja ambazo zimetolewa na Wizara hii. Kwa kweli Wizara ya Ardhi imefanya kazi nyingi. Katika hotuba yangu ambayo nimeitoa hapa katika ukurasa wa 6 hadi ukurasa wa 9, tumeelezea masuala mengi ambayo yamefanywa. Tumeeleza kwa mfano, zaidi ya vijiji 6,662 vimepimwa katika kipindi cha mwaka mmoja. Lakini ukiangalia je, vijiji vingapi vilikuwa vimepimwa katika miaka ya nyuma ukianzia labda tangu tupate Uhuru vilikuwa vinapimwa vijiji 110 *average* lakini mwaka huu tumepima vijiji 2,662. Kwa hiyo, ni suala la kupongezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukiangalia tangu labda enzi za Wajerumani miaka 1884 akina Carl Peter's ukatafuta hiyo *average* utakuta *average* ni kwamba kila kijiji kilikuwa kinapimwa Tanzania chini ya vijiji 60 kwa mwaka. Kwa hiyo, ni mafanikio makubwa yaliyofanyika. Lakini utaona pia kwamba katika kusajili hatimiliki, hatimiliki zilizosajiliwa katika mwaka huu tu ambao umekwisha ni zaidi ya hatimiliki 24,647. Kitu hiki kilikuwa hakijawahi kufanyika. Hatimiliki zilizokuwa zinasajiliwa kwa mwaka ni 2,000/3,000 na hizi zimesajiliwa na mtu mmoja Kamishna wa Ardhi, kwa hiyo, ningeomba tumpongeze kwa sababu mkono wake umeweza kusajili hatimiliki zaidi ya 24,000 na kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukiangalia katika hotuba hii yote utaona kwamba tumefanya uthamini wa nyumba zaidi ya 2,800. Tumefanya ukarabati katika nyumba za *National Housing* zaidi 2,773, tumekusanya mapato kwenye *National Housing* zaidi ya bilioni 19.5 na hii ni baada ya kupitisha ile Sheria Na. 11 ya mwaka 2005. Haya yote ni mafanikio makubwa ambayo nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa kutupongeza Wizara ya Ardhi kwa kazi kubwa tunazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili limejidhihirisha wazi pia hata katika kitabu chetu ukurasa wa pili tumetoa picha ya ushindi ambapo Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, akikabidhi kombe la ushindi kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Ushindi huu ni wa kwanza katika Wizara zote lakini ni wa pili katika Wizara pamoja na Taasisi ambazo zilikuwa 77, hiki si kitu kidogo. Ni vigumu kusubiri kusifiwa lakini mahali unapotakiwa kujifagilia, jifagilie mwenyewe. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote ni mafanikio makubwa, lakini utaona pia tumetambua miliki zaidi ya 10,840. Haya yote tuliyoweza kuyafanunua hapa yanadhihirisha ni kwa namna gani Wizara ya Ardhi imekuwa ikijitahidi katika kutatua matatizo mengi. Lakini pia yale ambayo tumekuwa tunayaona yamekuwa ni magumu, tumejitahidi kuleta Miswada hapa. Ni hivi karibuni mwanzoni mwa mwaka huu tulileta Miswada mitatu, Miswada ya Matumizi ya Ardhi na ya Mjini pamoja na Miswada ya kuangalia utaratibu wa kuwahudumia wataalam wa mipango miji. Miswada hii ilikuwa

na lengo la kuhakikisha kwamba migogoro ambayo imekuwa ikipatikana katika masuala ya ardhi inakuwa inatatuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, tumekuwa tukisisitiza Sera ya Ardhi ya Makazi ya mwaka 2000 ambayo inazungumzia kuhusu ujenzi wa nyumba katika miji yetu na hasa kwa kuzingatia kwamba miji yetu karibu asilimia 75 watu wamejenga kwenye *un planned area,* yaani kwenye *scattered areas* na tumekuwa tukisisitiza sheria. Hiyo Sheria Na. 4 ya mwaka 1999 na Sheria Na. 5 ya mwaka 1999 inavyowatambua hawa watu waliojenga kwenye *un planned areas.* Tumekuwa tukisema kipengele Na.3(g) kinawatambua hawa watu na kwamba mamlaka zinazohusika haziwajibiki kwenda kuwabomolesha hawa watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa pia tukisisitiza katika hotuba zetu kwamba kwa sababu ardhi ni mali, mtu au chombo chochote kinapokwenda kuchukua ardhi ya mtu yeyote ni lazima ilipwe fidia, iwe hiyo ardhi ni kwa ajili ya kujenga shule ya sekondari, iwe hiyo ardhi ni kwa ajili ya mabwawa, iwe ardhi hiyo ni kwa ajili ya kujenga hospitali, iwe hiyo ardhi ni kwa ajili ya nini, Sheria Na. 5 ya mwaka 1999 na Sheria Na. 4 ya mwaka 1999 kipengele Na. 3 kinasisitiza kwamba mwananchi mwenye ardhi ile awe ameimiliki kimila au ameimiliki kwa mujibu wa Sheria Na. 4 ni lazima alipwe *compansation.* Haya yote tumekuwa tukiyafanunua na kuyatolea elimu ili wananchi wote waweze kufaidika na ardhi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tumekuwa tukilizungumzia suala la kwamba ardhi haitakiwi kutolewa kwa mtu ambaye siyo raia wa Tanzania. Kama si raia wa Tanzania anahitaji ardhi ya Tanzania, ni lazima apitie *Tanzania Investment Centre* na ndiyo maana utaona kwa siku za hivi karibuni wawekezaji wakati nyingine wamekuwa na tamaa ya kutaka kupata maeneo makubwa ya ardhi. Kwa hiyo, tumekuwa tukiwaambia ni lazima walete au wapate kibali kutoka *Tanzania Investment Centre* kulingana na Sheria ya *Tanzania Investiment Centre* ya mwaka 1997 inayosema mtu ambaye si raia wa Tanzania ni lazima apate kibali kutoka huko na ndipo anaweza akapata ardhi. Haya yote tumekuwa tukiyafanya lakini lengo kubwa ni katika kuhakikisha kwamba migogoro mingi ambayo imekuwepo inayohusu masuala ya ardhi inatatuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utaona katika migogoro mingi ambayo imefunguliwa ambayo inakadiriwa kufika zaidi ya 10,000 zaidi ya migogoro 4,100 karibu na 200 imeweza kutatuliwa katika mwaka huu tu, ukilinganisha na migogoro mingi ambayo imekuwa ikifungulikwa na hii ni kwa sababu tumekuwa na Mabaraza 23 tu katika nchi nzima. Lakini pia tumeamua katika mwaka uliopita kwamba tutaongeza mabaraza mengine 10 na tulifanikiwa kuunda mabaraza mengine 10 na kufikia 33 na katika mwaka huu tumeamua kuongeza mabaraza mengine matano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninachotaka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge ni kwamba Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imefanya kazi kubwa. Imefanya kazi kubwa ambazo kwa kweli ni ngumu lakini mimi ningependa nichukue nafasi hii kuwapongeza sana ninyi Waheshimiwa Wabunge kwa sababu

michango yetu ndiyo imesaidia katika kuhakikisha kwamba kazi zilizofanywa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, zimefanikiwa na hii hata katika nchi za nje zimeweza kutambua kazi nzuri za Wizara ya Ardhi na ndiyo maana katika kipindi cha miaka miwili Tanzania tulichaguliwa kuwa Mwenyekiti mwenza katika Mkutano wa *Third Forum* wa *UN Habitat* ambapo uenyekiti mwenza tutaukabidhi kwenye mwaka 2008 kule Najing.Kwa hiyo, hii ni katika kazi nzuri zinazofanyika na wenzetu wamekuwa wakitambua hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua muda wangu ni mdogo sana. Lakini nijitahidi basi kujibu hoja hizi ambazo zimechangiwa na Waheshimiwa Wabunge. Nikianza na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi. Kwanza ameanza na pongezi na mafanikio ambayo yamefanywa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Napenda kusema tu wazi kwamba ushauri uliotolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi tunauzingatia na tutautekeleza na hii ni changamoto kwetu sisi kama Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Msemaji wa Upinzani Mheshimiwa John Momose Cheyo, naye ametoa pongezi nyingi sana na kuunga mkono hoja ambazo zimetolewa na Wizara ya Ardhi, lakini pia amezungumzia juu ya sera mbadala ya ardhi. Sasa katika sera mbadala ya ardhi ninajua hii ilikuwa ni ya Chama cha *UDP,* lakini cha CCM kipo kwenye ukurasa wa 68 bahati nzuri nimekuja na Ilani ya Uchaguzi hapa ambayo inazungumzia katika aya ya 68 nitampatia kaka yangu kusudi aweze akaseme. Lakini ninachotaka tu kusema kwa kweli nampongeza sana Mheshimiwa John Cheyo. Mchango wake wa leo huu unaonyesha kweli ameanza kuiva. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ameanza kuiva vizuri na mimi kwa kweli ningeomba Chama cha Mapinduzi kama siku yoyote Mheshimiwa John Cheyo ataomba kurudi CCM basi arudi moja kwa moja kwa sababu ni mtekelezaji mzuri wa chama hiki. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri mwingine alioutoa kwa kweli tutauzingatia kwa sababu lengo kubwa ni kuboresha maslahi ya Watanzania kwa ujumla na lile suala la kulipwa *compansation* kwa kweli hilo naungana nalo wananchi lazima walipwe *compansation* kwa sababu ardhi ni yao na wamepewa na Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, amezungumzia kuhusu migogoro ya ardhi inatokana na kulimbikiza madaraka kwa watu wachache. Sifahamu sana kama hili linaweza likawa kweli. Lakini migogoro ya ardhi kwanza imejitokeza mingi kwa sababu watu sasa wametambua ardhi ni mali. Lakini pia migogoro ya ardhi imeanza kujitokeza mara baada ya kutokupima ardhi kwa sababu tuna kilometa za mraba 949,000 katika nchi nzima ambapo asilimia 70 ndiyo eneo linalofaa kwa ajili ya malisho ya mifugo pamoja na kilimo. Asilimia mbili ndiyo eneo la miji yetu, asilimia 28 ni hifadhi za Taifa. Wananchi tumekuwa tukiongezeka wakati tukipata Uhuru tulikuwa watu kama milioni 10 na sasa tuko milioni 37.

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana baada ya miaka baada ya miaka 100 tutakuwa ni watu milioni nyingi zaidi. Ardhi ni ile ile kwa hiyo, kwa vyovyote migogoro

itakuwa imeongezeka na ndiyo maana tulileta Miswada mitatu hapa ambayo lengo lake ni kuhakikisha kwamba kila kipande cha ardhi tulicho nacho Tanzania ni lazima kipimwe ili kupanga matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudi hizi kitengo kinachoshughulikia masuala ya matumizi bora ya ardhi tumefanikiwa kupima zaidi ya hekta milioni moja katika Tanzania ambazo kwa bahari nzuri zile zitahusisha kwa ajili kuwapeleka wafugaji na kadhalika. Lakini ndiyo hivyo hivyo tumeamua kupima vijiji vyetu na kumilikisha na ndiyo maana mpaka sasa hivi tangu tupate Uhuru tulikuwa tumepima vijiji 6,000 sasa tumeshapima vijiji 2,662. Nina uhakika katika kipindi cha miaka miwili kama mtiririko utaendelea kuwa ni huu tutahakikisha vijiji vyote tulivyonavyo katika Tanzania vimepimwa ili kusudi watu waweze kupata hati miliki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningependa nitoe ushauri kwa Waheshimiwa Wabunge na Halmashauri zinazohusika basi zianzishe Masjala ya Ardhi katika maeneo yao ili wananchi hawa waweze kupata hati ambazo wanaweza kuzitumia katika kuondoa umaskini, ikiwa ni pamoja na kukopa benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Felix Mrema, ametoa pongezi nyingi sana na ametoa pongezi pia kwa Mheshimiwa Rais na mimi naungana naye, lakini pia amezungumzia kuhusu wajasiriamali ambao walipewa eneo, walikuwa zaidi ya 800 na katika kipindi cha mwezi mmoja chini ya mwezi mmoja, walikuwa wameshapata hati na anaomba kwamba ameshapata wajasiriamali wengine zaidi ya 1,200 nao wangependa hiyo hiyo *speed* ambayo tulitangaziwa na Mheshimiwa Rais iweze kutumika.

Mimi napenda kumhakikishia Mheshimiwa Felix Mrema kwamba *speed* ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi sasa ni kubwa sana. Wapo wanaopata hati ili mradi wanamaliza masharti yao hata ndani ya wiki mbili. Nataka kukuhakikishia kama mipango mizuri mtaipanga katika Manispaa ya Arusha hawa wahusika 1,200 tuko tayari kuwapa hati, inawezekana hata chini ya mwezi mmoja kama ulivyopendekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, amezungumzia pia juu ya umuhimu wa Wizara hii kiuchumi na ajira na mimi nakubaliana na wewe ingawa bahati mbaya kidogo Bajeti yetu mwaka huu imepungua, mwaka jana ilikuwa shilingi bilioni 18.2 mwaka huu ni shilingi bilioni 14.7 hivi. Lakini nataka kukuhakikishia hizi shilingi bilioni 14 tutazitumia vizuri katika kuhakikisha kwamba yale malengo ambayo tumeyaweka yanatimizwa kulingana na *speed* hiyo ambayo ameizungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, amezungumzia pia juu ya Sheria ya Ardhi hasa pawepo na benki. Hili suala ni zuri na bahati nzuri kwa sasa hivi sisi kama Serikali kwa kuwasiliana na wenzetu wa Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Zakia Meghji panaandaliwa Muswada ambao utawawezesha mabenki yetu yaanze kutoa mikopo katika mpango wa *mogage system.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba ni Tanzania tu ndipo wananchi wake wanaojenga nyumba kwa kutumia fedha zao. Nchi nyingi duniani na

hata Marekani kwa mfano, uchumi wake umeweza kukua kwa zaidi ya asilimia 70 kwa sababu waliingia kwenye mambo ya *finance.* Waliingia kwenye mambo ya *mogage system* katika nyumba zao waliingia katika masuala ya kukopesha wananchi katika kujenga nyumba. Ukishajenga nyumba kwa ajili ya kuwakopesha na mkopo wenyewe uwe wa muda mrefu na bahati nzuri riba iwe chini ya asilimia 10 hapo tutaweza kujenga uchumi wa kweli na ku-*create employment* kubwa kwa Watanzania. Kwa hiyo, hili suala linashughulikiwa na Serikali na nina uhakika hivi karibuni tu litaweza kukamilika. *(Makofi)*

Pia amepongeza chombo kama *National Housing* na mimi napenda nitoe pongezi kubwa sana kwa *National Housing* na ndiyo maana unaweza ukaona wanaandikwa andikwa sana ni kwa sababu wanafanya kazi. Siku za nyuma *National Housing* walikuwa wanakusanya mapato yao kwa mwaka karibu shilingi bilioni 2 hadi 3. Mwaka huu wamekusanya shilingi bilioni 19.5 na hii ni baada ya kuzingatia ile sheria Na. 11 ya mwaka 2005 ambayo inamtaka kila mpangaji alipe kodi yake na asilipolipa basi anapewa *notice* ya siku 30 na kuondolewa na kuuzwa vifaa vyake na baadaye anatafutwa mpangaji mwingine.

Napenda nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mheshimiwa Rais kwa *support* kubwa waliyoitoa katika kushughulikia hawa wapangaji ambao walikuwa wanakwepa kulipa kodi katika *National Housing.* Lakini *National Housing* imekuwa ni dira nzuri na ndio maana katika Bajeti ya mwaka huu wamepanga kujenga nyumba zaidi ya 222. Lakini hadi sasa hivi wameshamaliza kujenga nyumba zaidi ya 314 na katika nyumba hizo zinauzwa. Kwa hiyo, mtu anayehitaji kununua nyumba, nyumba za *National Housing* zipo msiogope mnaweza mkalipa pole pole baadaye mkawa na nyumba na hii ndiyo sera ya CCM ukiisoma katika Ibara ya 68. kipengele cha (k) kinazungumzia kuhusu hili. Kwa hiyo, na mimi napenda niwapongeze *National Housing* kwa kazi kubwa wanazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia *National Housing* wamekuwa wakiingia ubia na watu binafsi. Hadi sasa kuna majengo yanajengwa mengi kwa Dar es Salaam, Mwanza na sehemu zingine za nchi ambazo wanaingia na watu binafsi kwa mazungumza kwa kupata *share* angalau ya asilimia 25. Hakuna sababu ya *National Housing* kukaa na kiwanja na linyumba gofu wakati liko katikati ya mjini, wakati ungeweza kuingia ubia na mtu akajenga gorofa 30 hadi 40 katika kubadilisha mandhari ya jiji letu. *National Housing* wamejenga hilo, na wameitikia kwa wito mzuri ile sera ya makazi ya kujenga *vertically* badala ya kujenga kila siku *horizontal. (Makofi)*

Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe ametoa pongezi nyingi kwa Wizara na amesisitiza kuhusu suala la mgogoro wa suala lake ambalo amelizungumza la wawekezaji ambao wanatakiwa kulima katika eneo la Kisarawe. Ni kweli kabisa kwamba Mheshimiwa Janguo alifika pale ofisini akiulizia kuhusu hili suala na bahati nzuri alivyoniona nilimweleza kwamba kitu kikubwa ambacho kinahitajika kwa sababu wale watu wanaohitaji ardhi kubwa ni zaidi heka 10,000 na kwa bahati mbaya eneo la Kisarawe lilikuwa halijapimwa. Mkoa wa Pwani wote wenye vijiji zaidi ya 400 na kitu vilikuwa havijapimwa na eneo la Kisarawe kuna wananchi, kwa hiyo, tukamwomba Mheshimiwa Athumani Janguo, kwamba ni vyema angalau tupate barua ya

kutoka *Tanzania Investment Centre.* Bahati nzuri Mheshimiwa Athumani Janguo alifanya hiyo kazi na ikapatikana hiyo barua kutoka *Tanzania Investiment Centre* ambayo ilikuwa inawaruhusu *Sun Bon Fuel Limited* katika kupata ardhi hiyo. Lakini cha pili kilichotakiwa ilikuwa sasa ni kuangalia eneo la vijiji vyenyewe vilivyokuwa vinahitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni siku nyingi tumekuwa tumepata migogoro ya wananchi. Wanakuja wawekezaji wanachukua eneo halafu wanadai wamepata hati, halafu baadaye mkishampa hati wale wananchi wanaanza kwenda kulalamika na hiki ni mfano mzuri ambao bahati nzuri tulipewa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete katika eneo la Chamakweza, Bagamoyo, kijiji chote kiliuzwa na mwekezaji ambapo baadaye pakatokea mgogoro mkubwa ambao uliwezesha mpaka kutengua hiyo hati. Sasa tukaona kwa njia hiyo ni lazima tuchukue tahadhari katika maeneo yote ambayo wawekezaji wanahitaji kuweka mawekezo yao ili kusudi tusilete migogoro ya ardhi kwa wananchi ambao wamezaliwa huko na kuwa omba omba na wahamiaji, wakaja wazungu kwa maneno mazuri ya uwekezaji na wakaweza kupata ardhi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tuliwahusisha Halmashauri ya Kisarawe na vijiji ambavyo vilihusika, kwa taarifa tu ningependa nivitaje, ni vijiji vya Virambwa ambacho kina wakazi zaidi ya watu 757, kijiji cha Chakenge wakazi 985, kijiji cha Mtakayo wakazi 852, Kijiji cha Kidunguro wakazi 641, kijiji cha Marumbo wakazi 1,168 na kijiji cha Muhanga wakazi 1,018. Kwa hiyo, jumla wakazi 5,421 ambapo hekta zilizokuwa zinahitajika katika kijiji hiki wanavijiji wenyewe wana-*occupy* kijiji zaidi ya hekta 12,437 na 237 na zilizokuwa zinahitajika ni heka 11,226 na 541 kwa hiyo, ilibidi tufanye utafiti na kuwasiliana vizuri na wenzetu Halmashauri inayohusika.

Napenda tu nitamke kwa sasa hivi kwa mujibu wa sheria Na. 5 ya mwaka 1999 Sura ya 114 baada ya tarehe 1 Mei, 2001 ardhi yoyote ya kijiji inatakiwa imilikiwe kwa kimila. Kama inaweza kuwa imilikiwe kwa sura Na. 113 ni lazima kwanza ihaulishwe na mamlaka hayo ya kuhaulishwa huwa yako chini ya Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, napenda kumjulisha ndugu yangu, mzee wangu Mheshimiwa Athumani Janguo kwamba barua hii tumeshaipeleka kwenye mamlaka ya juu kwa ajili ya kuhaulishwa na ilitoka kwangu tarehe 18 Julai, 2007 na tulipeleka kwa *dispatch* kwa hiyo, akitaka kuja kuona anaweza akaja akaona na hii *document* naweza nikamwonyesha. Kwa hiyo, nataka kumhakikishia Mheshimiwa kwamba wawekezaji wake sasa hawana tatizo, tunasubiri haya mamlaka ya juu yatakapotoa maamuzi mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani amezungumzia juu ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa imewasimamisha wanakijiji wasilime, kigezo kikubwa kwamba kuna mwekezaji kijiji cha Mivumoni. Kwa hiyo unaweza kuona hili suala la Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah linapingana na la Mheshimiwa Athumani Janguo, huyu anasema wamilikishwe, huyu anapinga wasimilikishwe kwa sababu wanazuiwa kulima. Kwa hiyo, unaweza kuona kwamba Wizara hii ni migogoro tu, huku mgogoro unafanana hivi, huku mgogoro unaenda hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa anasema watu wamezuiwa kulima. Sasa ninachoweza kuahidi kwa Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah kwa sababu huu mgogoro ndio nimeujua sasa hivi, ningeomba atupe muda katika Wizara yetu tujaribu kuufuatilia, tuwasiliane na wenzetu wa Mkoa ili tujue ni nini tunaweza tukazungumza katika hili suala. Kwa sababu kama kweli kuna mwekezaji ambaye amekuja tuangalie *document* hizo zinahusuje, nina uhakika tunaweza tukalitafutia ufumbuzi suala hili. Amezungumzia pia juu ya sheria Na. 5 ya mwaka 1999 Halmashauri inapokusanya mapato fedha hizo huchelewa kufikishwa kwenye Halmashauri husika. *(Makofi)*

Napenda kumjulisha kwamba Halmashauri husika ya Pangani kwa fedha ambazo imekusanya imeshapelekewa, kitu kinachotakiwa ni kwamba unapokusanya ni lazima ulete ripoti huku kwenye makao makuu kuonyesha umekusanya kiasi gani, ili kusudi asilimia 20 yako uweze kupata. Amezungumzia pia juu ya hoteli zinazojengwa ndani ya mita 60 hakuna hatua zozote zinazochukuliwa, kwenye hoteli zinazojengwa ndani ya mita 60 wanaotakiwa kuchukua hatua ni Halmashauri ya Pangani, wala si Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa sababu *building permit* zinatolewa na Halmashauri ya Pangani. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nitoe wito kwa Halmashauri ya Pangani kama wapo watu au wenye hoteli ambao wamevunja sheria kwa kujenga ndani ya mita 60 basi waweze kuchukua hatua. Kwa sababu zile mita 60 zinaachwa kwa makusudi kwa ajili ya matumizi ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, amezungumzia pia papangwe maeneo maalumu kwa ajili ya kujenga *estate*. Hili nakubaliana naye kwa asilimia mia na kwa sasa hivi tumekwisha aanza kwa mfano Dar es Salaam yapo maeneo mbalimbali ambayo yamepangwa ajili ya *Rio estates,* wapo watu ambao wameshachukua zaidi ya heka 8 kwa ajili ya kuanza kujenga. Wapo wengine sasa hivi wa *Mutual Developers* kule Kigamboni wanajenga nyumba zaidi ya 130 lakini pia tuna maelekezo kwenye eneo la Kigamboni tutalipanga upya ili pawe na mji wa kisasa, lakini pia maeneo ya Luguruni kule kwa Mheshimiwa Charles Keenja, napo tumeshaanza kupanga ya *satelite re-towns* na kadhalika. Kwa hiyo, hili liko ndani ya sera ya makazi na mimi nakupongeza sana Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa mtazamo huo nina uhakika hata maeneo yako ya Pangani ambayo ni muhimu sana kwa utalii yanaweza yakajengwa katika mpango huo, ni jukumu tu la Halmashauri na Manispaa zinazohusika kuanza kuchukua majukumu hayo.

Mheshimiwa Abbas Mtemvu, ametoa pongezi na amezungumzia kuhusu fidia za Kurasini. Napenda kumthibitishia na bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumza hapa. Ningemshauri Mheshimiwa Abbas Mtemvu asome ukurasa wa 39 na wa 10 wa hotuba yangu, mpaka sasa hivi tumeshalipa zaidi ya wakazi 183 zaidi ya shilingi bilioni 2.7 na kwa sasa hivi tuko kwenye maandalizi mengine ya wakazi zaidi ya 100 ambapo tukishauza viwanja tutaendelea kuwalipa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, huo ni mpango endelevu, mnauza kiwanja fedha zinazopatikana ndizo mnaweza kulipa *compensation*. Wananchi wote wa Kurasini wanahitaji *compensation* ya zaidi ya shilingi bilioni 20, kwa hiyo, tunafanya hivyo kama *revolving fund* katika kuhakikisha kwamba wananchi hao wanapata fidia zao, lakini napo napenda nitoe wito kwa Mheshimiwa Abbas Mtemvu, wale watu ambao wamekwishalipa fidia 183 wahame, *otherwise* tunatabomoa kwa sababu hawawezi wakakaa na fedha ya fidia halafu wakakaa na nyumba, na wakakaa hivyo hivyo wakati viwanja husika tumeshamaliza kuvitangaza kwa ajili ya wawekezaji na kujenga maeneo ya bandari. Hawawezi wakakaa na vyote, kwa hiyo, kila mwananchi anapolipwa *compensation* yake, ningependa nitoe wito wahame, waache eneo kwa ajili ya maendelezo ya eneo hilo. *(Makofi)*

Mengine ya Mheshimiwa Abbas Mtemvu yamefafanuliwa vizuri na Mheshimiwa Naibu Waziri ikiwa ni pamoja na *issue DDC* - Keko na kadhalika hayo yote ni masuala ya Manispaa. Manispaa ndiyo inatakiwa kueleza, Manispaa ndiyo inatoa *building permits* na kadhalika. Lakini pia ametoa pongezi nyingi kwa *National Housing* kwa kuingia ubia na wawekezaji na mimi napenda kumpongeza Mheshimiwa Abbas Mtemvu ni matumaini yangu kwamba haya yote ataunga vizuri mkono hoja za Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ephraem Madeje, Mbunge wa Dodoma nan mtani wangu ametoa pongezi kwa Wizara, ametoa matatizo mengi ya mikakati ya wananchi wanaojenga kiholela katika Makao Makuu ya Dodoma na amezungumzia juu ya kijiji cha Kinyoli katika kata ya Kilimani, amesema hawa wamejenga kwenye maeneo ambayo ni *planned* lakini wameambiwa wahame na bila fidia. Suala la fidia ni la sheria kwa hiyo, mimi ningemuomba Mheshimiwa Madeje awasiliane na *CDA* kwa sababu haya yako ndani ya *CDA*.

Lakini pia amezungumzia kuhusu wananchi ambao wameambiwa kuna uwanja utajengwa kule Msalato na bado hawajalipwa fidia sasa suala la viwanja vya ndege liko chini ya Wizara ya Miundombinu. Kwa hiyo, ningeomba awasiliane na Wizara ya Miundombinu katika kufuatilia malipo ya fidia kwa wananchi hao. Wizara ya Ardhi inachosisitiza ni kwamba ukichukua ardhi ya mtu yeyote iwe hiyo ardhi inachukuliwa na mtu binafsi, iwe hiyo ardhi inachukuliwa na Serikali, iwe hiyo ardhi inachukuliwa na mwekezaji, iwe hiyo ardhi inacukuliwa na chama cha siasa, iwe ardhi inachukuliwa na nani, *compensation* lazima ilipwe kwa mujibu wa Sheria Na. 4 ya mwaka 1999 kipengele 3(g) na Sheria Na. 5 ya mwaka 1999 kipengele namba 3(g). Kwa hiyo, kama hawa watu wa Msalato wanastahili kulipwa fidia na pale panajengwa uwanja, nina uhakika Wizara inayohusika itakuwa imeandaa fidia kwa ajili ya wahusika hawa kabla ya kuhamishwa, lakini yale masuala mengine *CDA* inahusika kikamilifu na nina uhakika inaweza ikapata majibu mazuri. Lakini nakubaliana na yeye kwamba miji mingi ya Tanzania imejengwa kiholela, zaidi ya asilimia 75 imejengwa kwenye *un planned areas*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mbunge wa Nkansi amezungumza malalamiko mengi na amezungumza mengi tu na ushauri mkubwa ambao ameweza kuutoa na ameelezea kuhusu uzembe unaofanywa na baadhi ya watendaji wa Wizara ya Ardhi. Mheshimiwa Nyami ndugu yangu, napenda kukuthibitishia kwamba ni hivi karibuni tu tumepitisha sheria tatu hapa Bungeni, moja ni sheria ya mipango miji, nyingine ni sheria

ya mipango katika vijiji, nyingine ni ya kusimamia wanataaluma wa mipango miji. Sheria hizi zilipitishwa na lengo kubwa lilikuwa ni kuhakisha kwamba miji inapangwa vizuri. Katika sheria ya kusajili wanataaluma wa mipango miji, moja ya vipengele vinasema mwanataaluma wa mipango miji anapovunja taratibu anaweza akafungwa hata miaka mitano. *(Makofi)*

Lengo la kupitisha sheria hizi ilikuwa ni kuweka nidhamu kwa *professionals* wanaohusika na masuala ya mipango miji. Kama walivyo *professional* wengine ma-*engineer*, ma-*contractors*, madaktari, ma-*lawyer* na kadhalika. Kwa hiyo, ni kweli kwamba miji yetu imepangwa vibaya lakini ndivyo tulivyo hivyo hakuna mtu anayetakiwa kulaumiwa wewe Mheshimiwa Nyami, Nkansi unatakiwa ulaumiwe, mimi nilaumiwe sisi sote humu tunatakiwa kulaumiwa na wananchi wote tunatakiwa kulaumiwa na ndiyo maana tumewajibika kutunga sheria mpya hizi tatu pamoja na Sheria ya Ardhi Na. 4 na Sheria Na. 5 na Sheria Na. 2 ya mwaka 2002 lengo kubwa ni katika kuhakikisha kwamba tunaleta mabadiliko ya kweli ili miji yetu iendane na hali ya kisasa. Kwa hiyo, jukumu hili lote ni letu sisi sote na tunawajibu wa kutoa elimu kwa wananchi wetu ili miji yetu ifanane fanane na miji ya kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Charles Keenja, Mbunge wa Ubungo amezungumzia juu ya tatizo la mipaka kati ya Kisarawe na Kinondoni, nashukuru Mheshimiwa Naibu Waziri amefafanua vizuri, amezungumzia juu ya hifadhi ya barabara kwamba ni mita 120 sasa itakuwaje watu wengine wamepata hati, napenda tu kumshauri Mheshimiwa Charles Keenja, bahati nzuri wakati tukishughulikia suala la hifadhi ya barabara chini ya Sheria Na. 167 ya Mwaka 1967 ambayo ilikuwa *gazetted* mwaka 1967 Juni na imeanza kutumika tangu mwaka 1938. Ni kweli eneo la Ubungo mpaka Kibaha ukubwa wake unatofautiana, kuna sehemu ambako ni futi 75 kila upande mpaka pale *TANESCO,* baada ya hapo upana wa barabara unakuja inakuwa ni mita 300 kila upande, baada ya hapo panakuja mita 400 kila upande mpaka eneo la Kibaha. *(Makofi)*

Katika eneo la Kibaha zinapungua zinakuwa futi 75 kila upande, baada ya kilometa kama mbili tena mpaka kwenye daraja la Ruvu upana unakuwa futi 300, hiyo ndiyo sheria na hiyo ndiyo sheria iliyopo ni lazima tuitekeleza. Lakini kama kuna umuhimu wa kubadilisha sheria hii ili kusudi Dar es Salaam tuwe na njia moja tu ya ukanda mdogo tu, ili siku nyingine ni maamuzi sisi wenyewe tunaweza tukafanya. Lakini ukweli ni kwamba sheria hiyo ndiyo ipo na iliwekwa kwa makusudi katika kuhakikisha kwamba mji wa Dar es Salaam, kwa sababu ndiyo ulikuwa mji wa kibiashara na ni mji mkuu lazima barabara zake ziwe kubwa, ziwe na *filter* kubwa katika kupunguza *conjunctions*. Lakini hata hivyo bado mapendekezo yanaweza yakaletwa na Mheshimiwa Charles Keenja kama kuna umuhimu wa kurekebisha sheria hii. Amezungumzia pia kuhusu suala la asilimia 20 wapewe *revenue year collection* ya *land rate* katika Dar es Salaam. Kwa sasa hivi katika takwimu nilizonazo Wizarani ni kwamba Ilala walikusanya shilingi milioni 68, Temeke walikusanya shilingi milioni 122 na Kinondoni walikusanya shilingi milioni 74, jumla ni hilingi milioni 264. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa 20% ya fedha hizo ndizo watapewa wahusika kulingana na kukusanya, lakini ningependa nitoe wito kwamba Halmashauri ya Manispaa

zilizotajwa zinatakiwa kama zinataka sheria hii itumike pia kwao basi walete mapendekezo ni kwa namna gani wanaweza wakaweza kukusanya mapato. Kwa sababu tulijaribu kuwapa kazi ya kukusanya vile viwanja 230 vilivyotambuliwa vyenye makazi holela kwamba angalau wajaribu kukusanya tuone ni kiasi gani wanaweza kukusanya, wamekusanya fedha kidogo sana. Kwa hiyo, tunaona bado hawajajipanga vizuri, lakini bado nashauri Mheshimiwa Charles Keenja kama Manispaa hizi husika zitaamua kukusanya na zenyewe basi zilete mapendekezo mazuri ya kuweza kuleta kweli kuonyesha kwamba wataweza kukusanya fedha za kutosha ili waweze kupata hizo *percentage* kama walivyoomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanja vimepimwa vingi lakini viwanja hivi vinauzwa kwa bei kubwa, sasa hapa kuna masuala mawili unapochukua kiwanja kwa ajili ya kukipima lazima ujue kiwanja kile ilikuwa ni mali ya mtu na yule mtu lazima mlipe *compensation*, ukishamlipa fidia maana yake fedha utakayoi-*collect* ndiyo lazima ufidie katika kumpimia kiwanja kingine, kwa sababu tumeshasema ardhi ni mali. Lakini ningependa kutoa wito kwa Mheshimiwa Keenja, kama Manispaa yao ya Kinondoni ina uwezo wa kupima viwanja na wakaviuza kwa bei ya chini basi wafanye hivyo. Mimi nawaruhusu kabisa hata kesho wakapange mipango yao waanze kupima viwanja vyao ambavyo watalipa fidia halafu wataviuza kwa bei ya chini, kwa Sababu tumesema ardhi ni mali watu wanatakiwa kulipwa kwa fidia, kwa hiyo fedha hizi tunazozipata ndizo zinatakiwa kufidika kwenye hivyo viwanja. Yule ambaye hawezi kuchukua viwanja basi asijenge kwanza asubiri mpaka atakapopata fedha. Tunafanya hivi kwa sababu tumekuwa na matatizo makubwa ya kutokuwa na viwanja katika nchi hii, mpaka sasa hivi tumeshapima viwanja zaidi ya 49, elfu na mia mbili na mia tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tulichukua mkopo hazina wa zaidi ya shilingi bilioni 8.9 zile fedha ndizo tukaanza kupima viwanja tukaona tuzichukue ili zoezi la kupima viwanja kwa Dar es Salaam kama mfano tumepima viwanja 34,000 fedha zile zimeweza ku-*accumulate* na kuweza kupata faida na zile fedha tumeweza kuwakopesha Manispaa zingine, Mwanza wameshapima sasa hivi zaidi ya viwanja 9500, Morogoro wameshapima viwanja zaidi ya 2300 pamoja na Mbeya wameshapima viwanja zaidi ya 2400 baada ya kukopeshwa shilingi milioni 600. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kama Manispaa za Dar es Salaam nazo zinataka kuingia katika zoezi hilo waje wakope wakapime viwanja waviuze, sisi hatuwezi tukachukua fedha za mkopo ambazo bado tunadaiwa Wizara tukapime halafu tuwape watu wengine kuuza wasiporudisha fedha hizo mtafanyaje? Tunawapa watu fedha kwa wale ambao wanakopa na sisi tumekopa na ardhi ni mali, kwa hiyo, ningependa nitoe wito kwa Manispaa za Dar es Salaam kwamba hakuna kiwanja cha bure lakini hakuna mtu aliyewazuia kupima viwanja watumie fedha zao walizonazo au hata wakope kwenye Wizara ya Ardhi ili waweze kupima viwanja vingi zaidi na ndiyo maana leo wakati nikizungumza hapa, nimeeleza kwamba kuna zaidi ya shilingi milioni 400 na kitu ambazo zimetolewa kwa Halmashauri katika kuwakopesha ili wapime viwanja na katika Halmashauri hizo nimetaja baadhi ya Halmashauri 16 ambazo hazijarudisha fedha katika mikopo hiyo, zile fedha zinatumika *revolving fund.*

Katika Bajeti ya mwaka huu tumepanga kukopesha Halmashauri zingine 19 ikiwepo Halmashauri ya Kibaha kwa Mheshimiwa Dr. Zainab Gama ambako tutatoa zaidi ya shilingi milioni 37, ili waweze kupima viwanja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Charles Keenja amezungumzia juu ya *satellite town,* nakubaliana naye tunahitaji *master plan* nyingine, hiyo ni sawa, lakini tuna *master plan* ya mwaka 1997 lakini kuna *master plan* nyingine ya mwaka 1971, lakini tutaendelea kuhuisha mji kadri mji unavyobadilika. Mshauri mwingine mzuri nakubaliana nao Mheshimiwa Charles Keenja alioutoa.

Mheshimiwa Dr. Zainab Gama amezungumzia kuhusu Rais aliyeahidi kuwa mji wa Kibaha uwe wa kisasa, uwe na viwanda na barabara, anataka maelezo toka kwa Waziri. Sasa sijui nimpe maelezo gain, mimi nilimueleza ahadi ya Rais iko pale pale na katika Bajeti ya mwaka huu kuna fedha ambazo tumezitenga kwa ajili ya kuwakopesha mji wa Kibaha katika kupima viwanja. *(Makofi)*

Lakini mji wa Kibaha, Mji wa Kibaha una mpango wa muda mrefu wa *master plan* ambao unaitwa *CUPD,* lakini katika mwaka uliopita tulikuwa tumeupangia fedha kwa ajili ya kupiga picha, bahati nzuri mawingu yalikuwa mengi yaliletwa na Wandengereko, kwa hiyo nina uhakika mwaka huu mawingu hayatakuwepo, tutapiga picha za mji wa Kibaha na hii ni katika kutimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Dr. Gama, mimi nakuomba usihangaike kutoa hela, tuachie tufanye kazi na kuupangia *master plan* mji wa Kibaha ambao ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Juma Killimbah amezungumzia juu ya Wilaya yake ya Iramba, anasema katika kitabu ambacho tumetoa hakuna vijiji ambavyo vimepimwa katika mkoa wa Singida. Mheshimiwa Juma Killimbah, napenda kukuhakikishia kwamba katika kitabu ambacho tumekitoa ni vile vijiji 2662 vilivyopimwa katika mwaka huu, lakini si kweli kwamba katika mkoa wote wa Singida hakuna vijiji ambavyo vimeshapimwa. Katika mkoa wa Singida kuna zaidi ya vijiji 161 ambavyo vimepimwa, *Singida rural* vimeshapimwa vijiji 167, Iramba vimepimwa vijiji 14, Manyoni ndiko bado havijapimwa vijiji na katika Bajeti ya mwaka huu na pamoja na kwamba tumepata fedha kidogo mkoa wa Singida utahusika katika kupima vijiji vyake pamoja na mkoa wa Tanga. Tunajitahidi kufanya hivi katika kuhakikisha kwamba tunawaletea uchumi wa kweli wananchi wanaohusika. Amezungumzia juu ya kupata Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi Mheshimiwa Naibu Waziri ameshaelezea na masuala mengine kwa sababu muda unaenda haraka haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshagongewa kengele ya kwanza, lakini ninachotaka tu kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, sisi kama Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wangu wote wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi tumejitahidi kadri ya uwezo wetu katika kuhakikisha kwamba tunapunguza kero. Yapo matatizo mengine ambayo yamechangiwa na Waheshimiwa Wabunge, lakini ukweli matatizo hayo yako chini ya Halmashauri zetu kwa sababu maafisa ardhi wa Halmashauri za Wilaya hawako chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, wale wapo chini ya Halmashauri zetu na tunawajibu wa kuwashughulikia sisi wenyewe, nilienda wakati fulani Tabora,

katika mji wa Tabora nilikuta ofisa ardhi wa pale amekaa zaidi ya miaka 25, nikawa nimeandika barua kwa Mheshimiwa Mizengo Pinda, kwamba huyu nafuu ahamishwe tu kwa sababu amezoea mno anasubiri ku-*retire* hapa, nina uhakika hatua zimeshachukuliwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, matatizo katika Halmashauri za Wilaya na hasa watendaji wa ardhi hawako chini ya Wizara ya Ardhi, Wizara ya Ardhi tumejitahidi kweli na ndiyo maana hata hizi kupata zawadi pongezi na makombe haya yote yanadhihirisha ni kwa namna gani Wizara ya Ardhi tumejitahidi katika kutekeleza kazi zetu.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, mimi ningeomba sana katika Bajeti ya mwaka huu mwaka jana tulitengewa shilingi bilioni 18 mwaka huu tuna shilingi bilioni 14 sasa mkitoa hata hiyo shilingi zimepungua asilimia 19 mtu ulipewa kutembea barabara ukiwa na ndala mwaka huu hata ndala umenyang'anywa unaambiwa tembea kwenye miba, bado wanataka wakunyang'anye na miguu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba Waheshimiwa Wabunge tutakapofikia wakati wa Kamati basi pasitokee hata mmoja wa kusimama mtuachie tu, tupite na hizi shilingi bilioni 14 zetu ili twende tukatekeleze haya ambayo tumeyapanga na mimi napenda kuwaahidi Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea kufanya kazi kwa ushirikiano mkubwa, ushauri wenu ni muhimu sana, yapo mengi yamezungumzwa, kwa mfano, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally amezungumzia kuhusu hati, mpaka sasa hivi hati zimeshasainiwa zaidi ya 55 zimepelekwa kusajiliwa Mwanza. *(Makofi )*

Mheshimiwa Mgana Msindai amezungumzia kuhusu mipaka, tumeshatoa *Government notice* nyingi tu kwa wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya kwa ajili ya kusimamia kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na kadhalika. Masuala ni mengi ambayo yamezungumzwa lakini kwa sababu nimeshagogewa kengele, mimi ningewaomba Waheshimiwa Wabunge tupitishe hizi fedha ili kusudi haya majibu yaliyobaki ambayo yamechangiwa na Waheshimiwa Wabunge tutayajibu.

Mheshimiwa Aggrey Mwanri kwa mfano amezungumzia anahitaji, tumeshatoa kwa *RAS* kifaa kwa ajili ya kupima lile eneo, kila mahali tumetekeleza na ninawahakikishia kwamba karibu kila mmoja aliyechangia humu tumetekeleza majumu yake. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru sana wewe, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango mizuri, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

Kifungu 1001…

**NAIBU SPIKA:** Wageni wetu saa hizi huwa hatutembei tunaomba mkae.

Kifungu 1001 – *Administration and General*… … Sh. 3,300,374,800/=

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote 48* programu ya 10, *sub-vote 1001 item 250100,* pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri ni mgeni kidogo, lakini amezoea sasa hivi katika Wizara ya Ardhi, nilikuwa napenda pia kufuatilia suala ambalo nilikuwa nimemuuliza katika Bajeti iliyopita. Sasa hivi wakati wa kutengeneza mahesabu ya Serikali *asset* ambazo ni pamoja na ardhi ni kitu muhimu sana. Shirika la *TIRDO* mpaka leo pamoja na kugawa kile kiwanja kumpa *CCBRT* hawajaweza kupata hati yao. Naomba tu aniambie ni lini hao watu wataweza kupewa hati yao ili nao waweze kuwekeza na pia kuweka mahesabu yao vizuri.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimpongeza Mheshimiwa Stella Manyanya kwa kufuatilia kwa karibu sana hili suala la *TIRDO* na kiwanja cha *CCBRT.* Lakini kabla hujatoa hati na hasa katika Wizara yangu ili kuepuka matatizo ya hati pandikizi tuliamua kuwahusisha wenzetu wa Halmashauri au Manispaa ya Kinondoni kwa hiyo, bado tunawasiliana na wenzetu wa Manispaa ya Kinondoni ili tuweze kuona ni kwa namna gani tunaweza tukawapatia *TIRDO* hiyo hati yao. Kwa hiyo, mara mawasiliano hayo na mchakato mzima utakapopatikana tutaweza kumjulisha Mheshimiwa Stella Manyanya kuhusu ombi hilo na hii ni kwa sababu ya kuogopa migogoro ambayo inaweza ikajitokeza katika kutoa hati badala ya hati nyingine.

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi ya kusimama kutaka ufafanuzi zaidi kutoka kwa Waziri inaelekea ugomvi wetu juu ya ule mradi wa uwekezaji umepungua lakini nataka Mheshimiwa Waziri anihakikishie kwamba mimi sina wasiwasi kule Ikulu alichochelewa, anihakikishie kwamba baada ya kupata kibali suala hili litakuwa limeelekezwa haraka kwa wakezaji na watu wa Kisarawe waone kwamba mradi umeanza.

Pili, sikuridhika na maelezo ya Naibu Waziri juu ya majibu kwa Mbunge wa kule Ubungo jirani yangu Mheshimiwa Charles Keenja, suala hili la mpaka baina ya Kisarawe na Kinondoni, iliamuliwa mwishoni mwaka jana au mapema mwa mwaka huu mbele ya wakazi wa pale, uongozi wa wilaya zote mbili na ukafikiwa uamuzi wa mwisho.

Sasa suala la kusema kwamba waenda kwa wanasheria na nini watu wa Kisarawe hawatoelewa na wanakijiji pale hawatolielewa. Nafahamu hii ni hadithi ya bedui na ngamia, mkoa wa Pwani umetoa sehemu nyingi sana za ardhi kwa ajili ya Dar es Salaam kupata nafasi kama vile ngamia alivyotaka kuingiza pua yake ndani ya hema halafu kisha akamtoa bedui akaingia kwenye hema na bedui yuko nje anapigwa na baridi. Sasa nasema ni kwamba tumefikia mahali ni kwamba mipaka ambayo imekwishakubalika

iheshimike kwa hiyo, naomba tamko la Waziri kwamba suala hili limeamuliwa na limeamuliwa mbele ya wanakijiji na mamlaka za Wilaya zote mbili kwa hiyo limekwisha, naomba ufafanuzi huo, ahsante.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hili suala la *Sanibu Bio Fuel Ltd*., nafikiri nimetoa ufafanuzi wa kutosha kwamba tulitakiwa kujiridhisha ni kwa namna gani hawa wawekezaji wataweza kupata hiyo ardhi yenye ukubwa wa karibu zaidi ya ekari 11,000 kutoka kwa wanakijiji ambao wanaeneo la zaidi ya ekari 19,000 na wanakijiji ni zaidi ya 5,000 na kitu na hii ni katika kujiepusha na migogoro ya ardhi ambayo imekuwa ikijitokeza katika sehemu kubwa. Lakini hata hivyo kutokana na ufuatiliaji mzuri wa Mheshimiwa Athumani Janguo, na kuzingatia kwamba Mheshimiwa Janguo tunamwamini sana katika masuala ya uendelezaji na kuendeleza wananchi wake, hili suala limefikia mwisho na mimi nimemweleza kwamba limetoka mezani kwenda kwa Mheshimiwa Rais tarehe 18. Sasa sifahamu kwa nini anataka kuuliza tena zaidi na wakati nimeshamweleza hapa na nimemuahidi kwamba ninaweza nikamuonyesha hata hilo dokezo. *(Makofi)*

Lakini la pili chini ya sheria namba 4, kifungu cha 2 hadi 8 Mheshimiwa Rais akishakubali kuaulisha kuna taratibu za kufuata, kwanza Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi atatangaza kusudio la kuwaulisha ardhi katika Gazeti la Serikali, nakala ya tangazo hilo litapelekwa kila Halmashauri na vijiji husika ili kupata maoni ya Halmashauri hizo pamoja na yeyote atakayeathirika na ualishwaji huo atapata nafasi ya kuwasilisha hoja yake.

Kamishina na Afisa wa Ardhi anayethibitishwa atawajibika kuhudhuria mkutano wa Halmashauri ya kijiji na mkutano wa kijiji atakaokuwa ameitishwa kujadili taarifa ya kusudio la kuaulisha ardhi ili kufafanua sababu ya uaulishaji iliyokusudiwa na kujibu maswali yoyote yatakayojitokeza.

Tatu, kufanya makubaliano na kufikia muafaka juu ya masuala ya fidia, kwa mujibu wa sheria Na. 5 na Na. 4 ya mwaka 1999 kifungu Na 3(g). Sasa haya yote ndiyo yanasubiriwa, kwa hiyo, mimi ningemuomba Mheshimiwa Athumani Janguo, hii ndiyo sheria na sheria haikuundwa na Magufuli, imeundwa na Wabunge, ni lazima tuifuate katika kulinda maslahi ya wananchi wa Kisarawe, tunauihitaji sana mradi huu lakini pia sheria lazima tuzizingatie ili wananchi hawa wasidhurumike kwa misingi ya kwamba kuna wawekezaji. *(Makofi)*

Kuhusu suala la mipaka…

**MWENYEKITI:** Tuwe *brief* eh.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Kuhusu suala la mipaka sisi Wizara ya Ardhi jukumu letu ni kutoa *government notice* tu, nimeeleza hapa kwamba tulitoa *government notice* katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Wakuu wa Wilaya wote. Lakini kama panajitokeza mgogoro ni jukumu la

TAMISEMI kufafanua ni kwa namna gani wanataka kurekebisha hiyo mipaka, kwa hiyo, tutawasiliana na wenzetu wa TAMISEMI kuona kama hilo suala limekwishamalizika au nini ili tuweze kuchukua hayo yatakayokuwa yamekubaliana na wenzetu, kwa sababu Serikali ni moja.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, mimi ninaomba tu nipatiwe ufafanuzi wa kisera, kwa sababu katika ukurasa wa 34 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameomba wadau mbalimbali washirikiane naye ili kuweza kuzungumzia suala zima la mipaka baina ya nchi yetu na nchi zinazopakana na sisi zikiwemo nchi nyingi lakini nitazungumzia mpaka wa Tanzania na Msumbiji na mpaka wa Tanzania na Malawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi Mheshimiwa Kapteni John Komba lakini pamoja na sisi Wabunge wa Mkoa wa Ruvuma tumekuwa tukiomba sana msaada wa Serikali ili watusaidie kutafsiri mpaka wa Tanzania na Malawi kupitia Ziwa Nyasa. Sasa katika maelekezo ambayo yametolewa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri naona amekazia zaidi mpaka wa Tanzania na Malawi kupitia Mto Songwe, hajazungumzia kupitia Ziwa Nyasa, ningeomba atusaidie kujua nini kinachoendelea katika mpaka huo. Halafu labda nimuombe tu kwa kuwa ni suala la kisera mpaka wa Tanzania na Msumbiji utajadiliwa kupitia Bahari ya Hindi nadhani katika mpango wa mwaka ujao basi waangalie pia kupitia Mto Ruvuma ambao unakatisha kwenye majimbo ili kuweka hiyo hali katika utaratibu mzuri na unaotakiwa.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwamba wakati tutakapokuwa tunajadili kuhusu mpaka wa Tanzania na Msumbiji tuangalie pia mpaka uliopo katika Bahari ya Hindi pamoja na Mto Ruvuma. Lakini kuhusu suala la mpaka wa Tanzania na Malawi katika Ziwa Nyasa sisi Wizara na sisi kama Serikali tunajua mpaka uko katikati ya maji. Kwa hiyo, katikati ya Ziwa lile unatenganisha nusu kwa nusu huo ndiyo mpaka na ndiyo maana wananchi wa sehemu hizo huwa hawazuii hata kwenda kuvua samaki kwenye maeneo hayo kwa sababu huo ndiyo mpaka. Lakini kinachozungumzwa hapa tume-*concentrate* katika suala la *Songwe Development Project,* kwa sababu yale ni majadiliano ya pamoja yanayozihusisha nchi ya Tanzania pamoja na Malawi katika kuzungumzia tatizo la Mto Songwe ambao huwa na tabia ya kuhama hama na ndiyo maana tumekuwa tukiomba fedha kwa ajili ya kujenga *reserve* ya maji kubwa na kuweka *investment* kubwa katika maeneo hayo katika kuleta uchumi mzuri wa nchi katika maeneo husika.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kuhusu kifungu hicho hicho, mimi nilichangia kwa maandishi na tatizo tulilonalo ni mpaka wa Mkoa wa Singida, Mkoa wa Manyara na Mkoa wa Arusha. Mwaka jana tulikuwa na tatizo hilo kwa upande wa Wilaya ya Mbulu, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwani tatizo hilo wameshalimaliza, tunaomba tu waweke *beakons*, sasa tatizo kutoka Mto Endagunda kwenda Namba Sita na kupita Wilaya ya Karatu na Wilaya ya Iramba kwenda *Lake Eyasi.* Mimi nataka maelezo ni lini watatuma wataalamu wao wakakamilishe hiyo kazi? Nakushukuru.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika majibu ya msingi masuala ya mipaka huwa tunashirikiana sisi Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na wenzetu wa TAMISEMI. Lakini kuhusu suala la mipaka kwa ujumla sisi tulichofanya ni kwamba tulitoa *government notice* kwa Wakuu wa Mikoa wote na Wakuu wa Wilaya wote na bahati nzuri nakumbuka tulitoa *government notice* kwa Wakuu wa Mikoa wa Singida, Manyara pamoja na Arusha na ndio maana katika maelezo yake amesema tatizo la Wilaya wa Mbulu tumelimaliza, sasa ningemuomba Mheshimiwa Mgana Msindai, ambaye pia anahusika sana na mambo ya Halmashauri za Wilaya na yeye ndio Mwenyekiti wa Halmashauri zote katika nchi hii basi akalisimamie hili suala la mipaka na mapendekezo watakayoyaleta kwetu tutayatekeleza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Yeye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge inayohusika na Halmashauri kwani vipi Mheshimiwa Msindai?

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru ndio maana niliposimama nilisema huu ni mpaka wa mkoa na mkoa ni mpaka ambao unashughulikiwa na Serikali Kuu ambayo kitengo kipo ofisini kwake, sasa mimi ningeomba ni jukumu lake yeye na kitengo kilichopo kwake kushirikisha Halmashauri wakaangalia, tunalotaka ni kuonyesha tu huo mpaka unapita wapi na lingine tungeomba hizo *government notice* wawe wanatupa na sisi Wabunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** *Government notice* zinagawiwa hapa kila tunapoanza kikao cha Bunge, zinaambatanishwa hapa na Waziri wa Nchi, ndio kazi yake, kwa hiyo, zipo zinagawiwa, lingine ni *comment* tu kwa hiyo tunaendelea. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kuhusu kifungu hicho hicho, nilikuwa napenda kupata maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri juu ya mpango wa Serikali ambao unaziwezesha Halmashauri zilizo tayari kuanzisha na kutekeleza miradi ya upimaji wa viwanja. Katika Halmashauri yangu ya Wilaya ya Nzega tumeomba kupewa fedha hii ya mkopo toka mwaka 2004 lakini hadi leo hatujapewa jawabu la kwamba tutapata au hatupati na katika kitabu chake ukurasa wa 30 ameeleza kwamba kwa mwaka huu ujao wa fedha, kwa makadirio haya ya mwaka huu kuna Halmashauri zipatazo 19 zitakopeshwa jumla ya shilingi milioni 416. Sasa sisi ambao tulishaomba siku nyingi hususan Wilaya ya Nzega ambao tuna viwanja tunataka kupima kwenye mji wetu wa Nzega mji mdogo wa Ndala, Puge pamoja na Bukene tuko miongoni mwa hizi Halmashauri 19 ambazo zitapewa katika mwaka huu wa fedha? Nashukuru sana.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Halmashauri ya Mji wa Nzega imo kwenye orodha hiyo ya Halmashauri 19 zitakazopewa mkopo wa mwaka huu. Lakini ningependa kutoa wito kwa Mheshimiwa Lucas Selelii, mara watakapopata huo mkopo wakahakikishe basi wanazirudisha mapema isije ikawa kama zile Halmashauri 16

ambazo mpaka sasa hivi zimeshindwa kurudisha hizo fedha na hivyo mfuko huo kutupunguzia muda wa kuweza kuwasaidia na kuwakopesha wengine. *(Makofi)*

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii, kuhusu kifungu hicho hicho wakati nachangia kwa maandishi nilitaka ufafanuzi kwamba Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake amesema kwamba kasi ya upimaji wa viwanja na mashamba ni ndogo kwa sababu Halmashauri hazina wataalamu pamoja na vifaa vya kisasa kwa ajili ya kupima. Lakini kuna Halmashauri yangu ya Wilaya ya Meatu ina wataalamu na ina vifaa vingi tena vya kisasa kwa ajili ya kupimia viwanja na mashamba lakini kwa mwaka uliopita 2006/2007 ni viwanja vichache sana na hakuna hata shamba moja ambalo lilipimwa sasa labda kuna sababu gani nyingine zinazosababisha kukwamisha kupimwa kwa maeneo haya na kukwamisha wananchi kuweza kupata mikopo na kuwawezesha kuyafikia bora kwa kila Mtanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Mheshimiwa Waziri amesisitiza juu ya hati za kimila ambazo kimsingi ziko sawa sawa na hati ambazo zinasainiwa na kamishna wa ardhi lakini taasisi za fedha zilikuwa bado hazijaanza kuzitambua hizi hati za kimila, sijui kuna mkakati gani mahususi sasa wa kuziwezesha hizi taasisi za fedha kuzitambua hizi hati za kimila?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Wilaya ya Meatu kuwa na wataalamu pamoja na vifaa na kwamba kwa nini hawapimi, mimi nilifikiri hili suala wakaulizwe huko kwa sababu nimeeleza hapa kwamba watendaji wa ardhi waliopo kwenye Halmashauri hawako chini ya Wizara ya Ardhi, wale wapo chini ya mamlaka ya *DED*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilifikiri hili suala wakaulizwe *DED* kwenye vikao, wambane vizuri kwa nini wawe na vifaa pamoja na wataalamu na bado hawapimi viwanja na ikiwezekana waanze kuchukua hatua ikiwa ni pamoja na kuwafukuza kama watu wanaona hawafanyi kazi walizoajiriwa, mimi nafikiri tukifanya hivyo tutawasaidia Watanzania wengi katika maeneo yetu kupimiwa viwanja vingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hati za kimila kwa mujibu wa sheria Na. 5 ya mwaka 1999 zinawajibika kutolewa hati za kimila na bahati nzuri kwa sasa hivi zipo taasisi za kifedha ambazo zimeanza kutambua hati za kimila, wapo watu ambao waliokuwa na hati za kimila ambao wameweza hata kupata mkopo kwa ajili ya kusoma Chuo Kikuu, wapo ambao walikuwa na hati za kimila ambao wameweza hata kukoposhwa fedha na mabenki yetu. Kwa hiyo hati za kimila zinatambulika kwa mujibu wa sheria na ukizipeleka kwenye benki na benki wakazikataa kwa makusudi wana wajibu wa kuchukuliwa hatua kwa sababu ni hati na ni halali kwa mujibu wa sheria za nchi. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 *Finance and Account*… … … … … ...Sh.1,699,655,200/=
Kifungu 1003 *Policy and Planning*… … … … … ... .Sh.341,182,000/=

Kifungu 1004 *Management Information System* … …Sh.264,088,000/=
Kifungu 2001 *Land Development*… … … … … ... Sh.1,013,335,500/=
Kifungu 2002 *Surveys and Mapping*… … … … … Sh.1,494,373,500/=
Kifungu 2003 *Registrar of Titles*… … … … … ... ... Sh.405,041,000/=
Kifungu 3001 *Human Settlements Development* … Sh. 2,235,445,000/=
Kifungu 3003 *District Land and Housing Tribunal*..Sh.1,962,496,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

Kifungu 1001 *Administration and General* … … … Sh.172,000,000/=
Kifungu 2002 *Surveys and Mapping*… … … … … Sh.1,504,000,000/=
Kifungu 3003 *Human Settlements Development*… ….Sh.300,000,000/=

*(Bunge lilirudia)*

**TAARIFA**

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa na kama Kamati ya Matumizi na kupitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2007/2008, kifungu na kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko hivyo naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa liidhinishe Makadirio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2007/2008 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Naomba nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri na tunataka waendelee kufanya kazi hii ili mwaka ujao hata shilingi moja isitoke, Waheshimiwa Wabunge sina matangazo na napenda kuahirisha shughuli za Bunge.

Kesho tuna Mkutano Mkuu wa Taifa wa *UWT,* kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge kina mama wengi watakuwa wametoka kwa hiyo, nadhani utaratibu tutapanga

itakavyokuwa ni Wabunge wa CCM siyo wote, akina mama wa *UWT* wa CCM wote watakuwa na mkutano wa uchaguzi kesho kwa hiyo, mkiwaona hawapo ni kwa sababu hiyo. Sasa naomba niahirishe Kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.15 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa,*
*Tarehe 27 Julai, 2007 saa tatu asubuhi)*